


# UNABII WA HABARI ZA BIBLIA

*Umoja wa  
Eurasia  
Ujao*

**Imani: Je, Ni Kitu Gani?  
Imani Yawenza Onyeshwa  
Namna Gani?**

**Je, Wakristo wa Nyakati za  
Leo Wanapaswa  
Kuishika Sikukuu ya Baragumu?**


# HABARI ZA UNABII WA BIBLIA



8



20



31

## KATIKA TOLEO HILI:

- 3 **Umoja wa Eurasia Ujao (The Eurasian Union):** Yapo makubaliano ya kuunda Umoja wa Nchi za Ulaya Mashariki na Asia (Eurasia) hapo itakapofika 2015. Ni kipi ambacho Biblia inaashiria kwamba Umoja huu ujao wa Eurasia utakifanya?
- 8 **Kozi ya Jifunze Biblia Somo la 3: Kristo Atakomesha Maangamizi ya Ulimwengu**  
Hili ndilo somo la tatu la Kozi hii ya kuwasaidia watu wajifunze na kuilewa vema Biblia.
- 20 **Je, Wakristo wa Nyakati za Leo Wanapaswa Kuishika Sikukuu ya Baragumu?**  
Wayahudi huiita "Rosh Hoshanah". Wengi wa wajitao kuwa ni Wakristo siku hizi hawaishiki! Je, wewe unapaswa uishike? Je, inafundisha kitu gani?
- 27 **Imani: Je, Ni Kitu Gani? Imani Yawenza Onyeshwa Namna Gani?** Imani ni mojawapo ya mambo makuu ya sheria, lakini hasa Imani ni nini?
- 31 **Ni Kwanini Watu Hupungukiwa Imani:** Marehemu Herbert W. Armstrong analifafanua hili.
- 32 **Hatua ya Mwisho ya Kazi: Kuifikia Africa** Hatua ya mwisho ya kazi inayo maeneo mengi. Kanisa la Continuing Church of God liliedesha mkuutano kwa viongozi huko Nairobi unaohusu kazi hii. Je, Africa inafanyika kielelezo cha kuiga kwa Wana-Philadelphia?

**Jarida la Nyuma: Tovuti na Radio** Hili linaonyesha ni wapi watu wanaweza kuupata ujumbe kutoka Kanisa la Continuing Church of God.

**Kuhusu Jarida la Mbele:** Je, 'Umoja wa Eurasia' unakuja? Je, Biblia inaonyesha ni nini wale watakaokuwemo kwenye umoja huu wa 'Eurasia' watafanya nyakati za mwisho?

Unabii wa Habari zaBiblia huchapishwa na Kanisa la Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420. <http://www.ccog.org>  
©2014 Continuing Church of God. Limechapishwa katika U.S.A. Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakiri makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi. Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi, kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu. Endapo haungependa kuendelea kupokea gazeti hili, wasiliana na office yetu iliyo kwa Arroyo Grande. Maandiko yamenekuriwa toka New King James Version (@Thomas Nelson, Inc., Publishers, used by permission) Isipokuwa pale tu tumeelekeza vinginevyo.

Unabii wa Habari za Biblia-HUWEZESWA KWA MICHANGO YENU  
Bible News Prophecy has no subscription or newsstand price. This magazine is provided free of charge by the Continuing Church of God. It is made possible by the voluntary, freely given tithes and offerings of the membership of the Church and others who have elected to support the work of the Church. Contributions are gratefully welcomed and are tax-deductible in the U.S. Those who wish to voluntarily aid and support this worldwide Work of God are gladly welcomed as co-workers in this major effort to preach and publish the gospel to all nations. Contributions should be sent to: Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420.

Mhariri Mkuu: Bob Thiel  
Mpigachapa/Mhariri Msaidizir: Joyce Thiel  
Masahihisho na: Kayla Morgan  
Maandalizi &Uchapaji: Burdine Printing  
Picha: Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na vyano vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia (iliaka chanzo hakikutajwa, itakuwa ni kwa sababu inaaminika kwamba chanzo husika kiliachia picha iwe kwa matumizi ya umma pasipo masharti yeoyote).

# KUTOKA KWA MHARIRI MKUU: BOB THIEL

## Umoja wa Eurasia Ujao

Je, kutakuwepo Umoja wa Ulaya ya Mashariki na Asia (Eurasian Union) utakaoanzishwa? Je, muungano kama huo tayari umo katika maandalizi kwa sasa? Je, wako viongozi wowote wanaohangaikia swala hili katika karne hii ya 21? Je, Biblia inafundisha popote kwamba kutakuwepo na Umoja wa Eurasia hapo baadaye? Iwapo aina kama ya Umoja wa Eurasia ukianzishwa, ni nani wanaweza kunufaika nao na ni nani wanaweza kuathiriwa nao?

### Putin wa Urusi Anahitaji Umoja wa Eurasia

Wazo la aina kama ya Umoja wa Eurasia awali lilipendekezwa na Rais wa Kazakhstan, Nursultan Nazarbayev, wakati wa hotuba yake mwaka 1994, alipohutubia katika Chuo Kikuu cha Moscow.

Mnamo Octoba 2011, Rais wa Urusi Vladimir Putin akatangaza rasmi azima ya kuanzishwa kwa shirikisho litakaloitwa Umoja wa Eurasia - The Eurasian Union (EAU).

Tarehe 18 Novemba 2011, Maraisi wa Belarus, Kazakhstan and Urusi walitia sahihi makubaliano, wakiazimia kwamba taratibu za kuanza rasmi kwa shirikisho hilo zikamilishwe na Umoja wa Eurasia uweze kuanza rasmi ifikapo 2015. Makubaliano waliyotia sahihi yalihusisha maelekezo ya hatua watakazopitia kufikia muunganiko, na hapo wakaanzisha Jumuia ya Eurasia (Eurasian Commission, iliyoundwa kufuata muundo wa Jumuia ya Ulaya (European Commission) na pia wakaanzisha Jumuia ya Kiuchumi ya Eurasia (Eurasian Economic Space), ambayo ilianza kazi rasmi tarehe 1 Januari 2012.

Tangia hapo, jitihada za kuanzishwa kwa EAU zimeshika kasi. Baadhi ya mataifa jirani nayo pia yameonyesha nia ya kujiunga.

Ifuatayo ni taarifa aliyoitoa Rais Vladimir Putin juu ya umoja huo:

"Kuundwa kwa Jumuia ya Ushuru (Customs Union) pamoja na Shirikisho la Eneo la Kiuchumi (Common Economic Space) vinaweka msingi wa kufikia kuanzishwa kwa Jumuia ya Kiuchumi ya Eurasia ijayo. Wakati huohuo itapanua mipaka yake ya Jumuia ya Ushuru (Customs Union) pamoja na Shirikisho la Eneo la Kiuchumi (Common Economic Space) kufikia unganiko kamili kwa kuziingiza Kyrgyzstan na Tajikistan.

Hatujifungi katika kuishia hapo tu bali tumeweka kusudi kuu zaidi: Kwenda kwenye hatua ya juu zaidi ya shirikisho – Umoja wa Eurasia.

Kwa hiyo ni nini kile tukionacho na ni nini matarajio ya mradi huu?...

Tumekusudia aina ya shirikisho lenye nguvu la muunganiko

wa mataifa mengi liwezalo kufikia kuwa moja ya nguzo kuu za ulimwengu wa kisasa litakaloweza kutoa mchango wa kuwa "kiunganishi muhimu" kati ya Ulaya na eneo linalopanuka kiuchumi la Asia ya Pasifikasi... kuunda jumuia ya kiuchumi yenye mafanikio.

**...Umoja wa Eurasia utafanyika kuwa ni kituo cha kuwezesha kupanuka zaidi kwa shirikisho".**

Hivyo, Vladimir Putin anaitaka EAU, na pia anategemea itaelekea kufikia kuwa ni mamlaka kuu ya kikanda na ya kimataifa. Wengi wanaamini kwamba kujihusisha kwa Urusi katika Ukraine pamoja na Crimea kulitokana na mipango yake ya jumuia ya EAU. Malengo ya Vladimir Putin katika Ukraine ya mashariki, Moldova, pamoja na mataifa mengine jirani yanatokana na hamu yake ya kuyaingiza yawe sehemu ya jumuia yake ya EAU.

Vipi kuhusu vikwazo toka nchi za Magharibi? Ebu jionee yafuatayo:

ST. PETERSBURG, Aprili 17 (RIA Novosti) – Vikwazo toka nchi za Magharibi dhidi ya Moscow vinaweza kuzisukuma nchi za ukanda wa Asia ya Pasifikasi ziamue kuijunga na jumuia ya uchumi ya nchi za Umoja wa Kisoviet wa kale iliyopendekezwa, inayochukuliwa na wengi kuwa imeanzishwa na Urusi itoe ushindani kwa jumuia ya Uchumi ya Ulaya, EU; alieleza mse maji wa Serkali ya Urusi, Sergei Naryshkin...

Naryshkin alieleza kwamba jumuia ya kiuchumi ya Eurasia iliyombioni kuanzishwa (Eurasian Economic Union, au EAU) ni "Mshindani muhimu wa siasa za Kikanda" ambayo hapo baadaye itakuwa ndiyo daraja baina ya Ulaya ya Magharibi, ambayo kwa sasa katika miaka saba iliyopita imekumbwa na kuperomoka kwa uchumi wake, na ukanda wa Asia ya Pasifikasi unaokua kwa kasi kiuchumi.

Hatua hii inakuja katika wakati ambapo Moscow imo katika jitihada za kujipima mchango wake katika uchumi wa dunia na kuweka umuhimu katika mradi wa Eurasia. (Imenukuriwa toka makala iitwayo: Western sanctions to push integration of Eurasian Union and Asia-Pacific – Russian official. The Journal of Turkish Weekly, April 17, 2014. <http://www.turkishweekly.net/news/165766/western-sanctions-to-push-integration-of-eurasian-union-and-asia-pacific-russian-official.html>).

Vikwazo vya nchi za Magharibi yaonekana vinachoea kuimariika kwa Umoja wa Eurasia (The Eurasian Union). Kama mfano mmoja, pale Ulaya ilipofikiria na kutangaza azima yake ya kupunguza utegemezi wake wa kununua nishati toka Urusi kama onyo kutoptana na Urusi kuichukua Crimea, Urusi palepale ikatangaza kuingia makubaliano ya kuiuzia nishati China.

## **Shirikisho Lijalo la Eurasia Litahusisha China na Yawezekana pia hata India**

Yafuatayo ni maelezo aliyoyaandika marehemu Herbert W. Armstrong mapema hata kabla ya pendekezo la hivi karibuni la mipango ya kuanzishwa kwa Umoja wa Eurasia, Eurasian Union:

“Gogi” katika nchi ya “Magogi” ni maeneo makubwa mno ya U.S.S.R. katika kaskazini mwa Eurasia yakineea kutoka eneo la bahari za Baltic hadi Pacific. “Mesheki” ni Moscow, “Tubali” ni Tobol’sk.

Tambua wafuatanao nao katika vita hii ijayo. Utakuta kuna: “Gomeri,” “Togarmah,” “Magogi,” “Mesheki,” “Tubali” ambao wametambuliwa katika kitabu cha Mwanzo sura ya 10 kuwa ni wana wa Yapheth, baba wa wa-Eurasia. (Toka makala ya Armstrong HW. Kwanini Urusi Hataishambulia Marekani, chapa ya 1980, uk. 8).

Ole ya pili, ikiwa na vielelezo vyake vyta farasi na wapanda farasi...ambayo pia inatajwa kuwa ni tukio katika SIKU YA BWANA katika Yoeli 2:4. Hii inaashiria mamlaka ya kijeshi yenye uwezo mkuu—pia kuelekea KASKAZINI—kwenda kaskazini! Wanakuja na jeshi la askari millioni mia mbili! Tafakari juu ya Hilo—jeshi la askari millioni mia mbili! Matukio ya ulimwengu yanatia kasi kuelekea kuwezesha kuundwa kwa jeshi la Kikomnisti la Eurasia lenye idadi ya askari wengi kiasi kisichotegemewa! (Imenukuriwa toka: Armstrong HW. Kitabu cha Ufunuo Hatimaye Chawekwa Wazi! Toleo la 1972. Uk. 38-39).

Wazo la kuundwa kwa Umoja wa Eurasia linapatana kabisa na unabii wa Biblia, na pia na baadhi ya uelewa wa unabii wa marehemu Herbert Armstrong. Inatakiwa ieleteke kwamba jeshi la Ki-Eurasia si lazima liundwe kikamilifu ama na baadhi ya askari wa kikomnisti (ijapokuwa nchi nyingi mionganoni mwa zile ambazo Herbert Armstrong alizitaja kuwa zitaunda Umoja wa Eurasia, hapo mwanzo wakati Armstrong anaandika makala tuliyoinukuru hapo juu, zilikuwa ni sehemu ya himaya ya Kikomnisti chini ya Urusi).

Hatua nyingi za kuwezesha jumuia iliyopendekezwa ya EAU ianze zimekwishachukuliwa:

Wataalamu toka Strategic wanadai Umoja wa Eurasia ni meno ya serkali ya Moscow ya kuiwezesha kuzing’ata katika kulipiza kisasi USA na kujitanua kwa NATO katika Ulaya ya Mashariki; jambo litakayoyafanya baadhi ya mataifa ya eneo la kati yapime ama kuijunga na Ulaya ama na Umoja wa Eurasia kuona ni wapi yatajipatia manufaaa ya juu kiuchumi na kibiaresha (Imenukuriwa toka: Alam SS. Why Dream of Eurasian Union? 29 July 2013. <http://blogs.thenews.com.pk/blogs/2013/07/why-dream-of-eurasian-union/>).

Urusi, Belarus na Kazakhstan yamekubaliana kuanzisha Umoja wa Kiuchumi wa Eurasia, ulioundwa kufuatisha Jumuia ya Uchumi ya Ulaya-EU, wakikubaliana ianze rasmi mwaka 2015. Nchi hizi tatu tayari zinaumoja ya forodha lakini sasa zimeazimia kusonga mbele na kuondoa kabisa

vikwazo vyta biashara (Imenukuriwa toka: Russia sees union with Belarus and Kazakhstan by 2015. BBC, November 18, 2011. <http://www.bbc.co.uk/news/world-europe-15790452> viewed 08/12/13).

“Azimio letu la kuijunga katika Umoja wa Forodha pamoja na Jumuia ya Kiuchumi (Common Economic Space), na Umoja wa Eurasia ujao, una malengo muhimu ya kijeshi-kisiasa pamoja na kiulinzi pia”. Sawa na linavyotaarifu “Armenpress”, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Armenia, Tigran Sargysan alieleza haya... (Imenukuriwa toka: Armenia’s decision to join Eurasian Union has military-political content: Armenia’s PM. Armenpress.am, March 29, 2014. <http://armenpress.am/eng/news/755965/armenia%E2%80%99s-decision-to-join-eurasian-union-has-military-political-content-armenia%E2%80%99s-pm.html>).

Pamoja na kwamba hilo halitajitokeza sana mwanzoni, Jumuia ya Ulaya (the European Union) nayo pia ilianza kama chombo cha mkataba wa kibiaresha tu mionganoni mwa nchi ndogo za Ubelgiji, Uhlanzi, na Luxembourg (wakati huo ikiitwa Benelux), na sasa tayari umekua na kufikia nchi 28.

Umoja huu wa Eurasia pia unategemewa uwe na ushirikiano zaidi wa kijeshi. Urusi inajitahidi kuyahuishisha mataifa mengine kadhaa, moja kwa moja ama kiushirikiano yakiwemo China na India. Kusema kweli, India tayari imekwisha kupendekezwa kuwa ni mwanchama wa mara kwa mara wa chombo hiki kinachoundwa cha EAU.

Ziko sababu kadhaa zinazoifanya China nayo ihitaji kujumuishwa. Moja wapo ni kwamba Urusi na China zinahitaji kuongeza thamani ya pesa zao “Rouble” na “Yuan” katika soko la pesa. Wote wanahitaji kuongeza utendajikazi wa pesa zao katika biashara ya kimataifa. Wote wanakusudia kuzipendekeza pesa zao ziwe sehemu ya sarafu za ubadirishanaji wa kidunia (Global Reserve Currency). Wote wanalengo la kuiondolea mbali sarafu ya Dola ya Marekani, pamoja na kupunguza uwezo wa Marekani katika maswala ya kidunia.

Kadharika, tusishau kwamba Marekani imekuwa ikijirundikia madeni na hivyo kuzidi kuishusha thamani ya sarafu yake kuitia mipango mibovu ya kifedha. Wataalamu wa mambo ya fedha wanatakiwa watambue kwamba kile ambacho Marekani imekuwa ikikifanya ni kushusha thamani ya fedha yake. Kibiblia Marekani imekuwa ikiongeza “takataka” kwenye fedha yake hivyo kuishusha thamani, jambo lisilo sahihi (Isaya 1:22,25; Mithali 25:4a). Muda unakuja ambao hauko mbali, hili litailetea Marekani janga kuu kulingana na unabii wa Biblia (Habakuki 2:6-8).

Yale yanayotokea kule Asia, pamoja na maeneo mengine, yanaonyesha kwamba ulimwengu umeanza kuondoka toka katika kuitegemea sarafu ya Marekani (Dola) kama fedha ya dunia. Maandalizi mengi yamefanywa na Wachina, Warusi, pamoja na wengine (kama vile mataifa ya Ulaya) yatakayopelekea kuachana na matumizi ya Dola ya Marekani yatakayotupeleka kwenye wakati wa mwisho wa watu wa mataifa.

## Biblia Inaelezea Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kijeshi

Biblia inatumia maelezo kama vile ‘mfalme wa mashariki/ machweo ya jua (Ufunuo 16:12), wafalme wa Wamede (Yeremia 51:11), na pia “wafalme wengi” kutaja juu ya falme zipatikanazo maeneo ya kaskazini mwa Eurasia (Yeremia 50:41). Biblia inafundisha kwamba zaidi ya taifa moja yatahusika kuunda umoja wa kijeshi utakaokuwa wenye nguvu—na umoja huu utatokana na mataifa ya Eurasia.

Vladimir Putin amekuwa akitaja mara kwa mara kuimashirwa kwa jeshi la Urusi na pia kuliunganisha jeshi la nchi hiyo na mataifa mengine mengi katika Asia na hata baadhi ya Ulaya.

Urusi tayari ni nchi isambazayo vifaa vingi vya kijeshi kwa mataifa ya Asia, ikiwemo India, wakati India nayo pia inazidi kubuni na kutengeneza silaha zake yenye. China nayo pia hununua silaha toka Urusi wakati nayo pia inazidi kubuni na kutengeneza silaha zake yenye. Urusi na China zenyewe tayari zina mikataba kadhaa tofauti ya ushirikiano wa kijeshi. Zote ziko kinyume na nchi za magharibi.

Miaka kadhaa iliyopita, nilisoma makala toka India ambapo mwandishi wake alidai kwamba Urusi, China, pamoja na India zinaamini kwamba Wamarekani pamoja na nchi za Ulaya hakika hawawezi kuwachukulia kuwa ni sawa na wao na hivyo wameamua kwamba wachukue hatua za ziada za kuendeleza ushirikiano mionganoni mwao. Na pia wawe kinyume na Magharibi katika kila njia inayowezekana.

Ona yafuatayo:

Mipango ya kuunda Umoja wa Eurasia ni baadhi ya vitendo vya mbinu za kiulinzi zinazoelekezwa kiasi fulani kwa NATO pamoja na nchi za Magaharibi kiujumla na zaidi zikielekezwa katika umuhimu wa Umoja wa Ushirikiano wa Shanghai - Shanghai Cooperation Organization (SCO).

SCO ni chombo kinachodhaminiwa na China. Na, wakati haijulikani kabisa iwapo China inayo mipango yoyote ya kuimiliki Asia ya kati kwa namna yoyote, ndio nchi yenye uwezo na nguzu zaidi za kiuchumi, kijamii na kijeshi katika eneo hilo. Imekuwa sasa ni kawaida kusikia msemo kwamba soko la Asia ya Kati limetapaka bidhaaa na wafanya biashara wa Kichina. (Imenukuriwa toka: Peterson A. Central Asia unlikely to become another unstable Middle East. Global Times, August 13, 2013. <http://www.globaltimes.cn/content/803601.shtml#.Ugqr96z8az4> viewed 08/13/13).

Hivyo, China ni mdhamini wa SCO na kulingana na mwandishi mmoja, mazingira ya SCO ndicho ambacho hasa Umoja wa Eurasia unachotaka. Hivyo, wengi wanaona wazi kwamba Umoja wa Eurasia uliopendekezwa unalengo hasa la kujenga ushirikiano wa kiuchumi, na kijeshi. Tukisha sema hilo, Rais wa Urusi Vladimir Putin anawaza hasa kwamba EAU ni chombo kitakachomsaidia kuzidhibiti nchi za Magharibi pamoja na NATO.

Kijeshi, Biblia inaonyesha kwamba namna ya umoja wa kijeshi wa ki-Eurasia utatoka utakaohusisha wale walio Kaskazini na

Mashariki na umoja huu utamwogopesha Mfalme wa Kaskazini:

...mfalme wa Kaskazini ... 43Atamiliiki hazina za dhahabu, fedha na utajiri wote wa Misri, pamoja na Walibia na Wakushi kwa kujisalimisha. 44Lakin taarifa kutoka mashariki na kaskazini zitamshtua, naye ataondoka kwa ghadhabu nydingi ili kuangamiza na kuharibu kabisa wengi. 45Atasimika mahema yake ya kifalme kati ya bahari na mlima mtakatifu wa kupendezza. Hata hivyo, atafikia mwisho wake, wala hakuna ye yote atakayemsaidia (Dan 11:40,43-45).

Maeneo kama Armenia (hapa chini yakiitwa Ararat) yametabiliwa kuhusika na Mamlaka ya Kaskazini (ikijulikana kama ‘wafalme wa Wamedi hapo chini):

27“Twekeni bendera katika nchi! pigeni tarumbeta katikati ya mataifa! Andaeni mataifa kwa ajili ya vita dhidi yake, iteni falme hizi dhidi yake: Ararat, Mini na Ashenazi. Wekeni jemadari dhidi yake, pelekeni farasi wengi kama kundi la nzige. 28Andaeni mataifa kwa ajili ya vita dhidi yake, wafalme wa Wamedi, watawala wao na maafisa wao wote, pamoja na nchi zote wanazotawala.

29Nchi inatetemeka na kugaagaa, kwa kuwa makusudi ya BWANA dhidi ya Babeli yanasmama, yaani, kuangamiza nchi ya Babeli ili kwamba pasiwe na ye yote atakayeishi humo (Yeremia 51:27-29).

Nchi ya Armenia kwa sasa iko katika maombi ya kuijunga na Umoja wa Eurasia. Iweze ama isiweze kufaulu kuijunga kwenye EAU, imetabiriwa kuwa itakuwa upande wa mamlaka ya Eurasia itakayopigana dhidi ya mamlaka ya Mnyama wa Ulaya.

Agano Jipyia linaonyesha kwamba kundi la mataifa lijulikanalo kama Wafalme wa Mashariki litaundwa:

12Malaika wa sita akamimina bakuli lake kwenye mto mkubwa Eufrati, maji yake yakakauka ili kutayarisha njia kwa ajili ya wafalme watokao mashariki. 13Kisha nikaona roho wachafu watatu waliofanana na vyura wakitoka katika kinywa cha lile joka na katika kinywa cha yule mnyama na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. 14Hizo ndizo roho za pepo wachafu zitendazo miujiza. Nazo huwaendea wafalme wa ulimwengu wote na kuwakusanya tayari kwa ajili ya vita katika siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.

15“Tazama, naja kama mwivi! Amebarikiwa yeye akeshaye na kuziweka tayari nguo zake ili asiende uchi na kuonerekana aibu yake”. 16Ndipo wakawakusanya wafalme pamoja mahali paitwapo “Armagedoni” kwa Kiebrania (Ufunuo 16:12-16).

Gundua: Andiko la Ufunuo 16:12 awali liliandikwa: “wafalme toka mawio ya jua” na hivyo hii itahusisha pia nchi kama vile China, Japan, Korea, Indochina (ikiwemo Vietnam), Indonesia, pamoja na nchi zingine pia (kwa kuwa Indonesia ni nchi ya kiislamu, yaonekana itahitaji kuwa na mahusiano zaidi na China katika siku za mwisho ikipingana na Mfalme wa Kaskazini pale atakapokuwa amemshinda Mfalme wa Kusini aliye nchi za Kiislamu, sawa na (Danieli 11:40-43). India hali kadharika yaonekana itakuwa mionganoni mwa wafalme hao.

Urusi, iliyo na mpaka ueneao hadi bahari ya Pacific, ni dhahiri itakuwa ni mionganoni mwa wafalme hao wa Mashariki. Kutakuwepo na mwunganiko wa nyakati za mwisho wa mataifa ya Asia pamoja na baadhi ya mataifa ya Ulaya utakaouna umoja huo wa wafalme wa mashariki.

Maeneo mengine pia ya Biblia yanaonyesha kwamba milki hii ya "Babeli/ Ulaya" itaangamizwa na mamlaka toka Kaskazini.

Katika kitabu cha Yeremia, kwa mfano, imeonyeshwa kwamba watu kutoka Kaskazini (ambayo kimsingi ni kutoka Urusi) watakuwa ni sehemu ya jeshi litakaloifadhaisha na hatimaye kuivamia milki ya Babeli ya siku za mwisho (ambayo itakuwa ni mamlaka ya Ulaya):

41 "Tazama! Jeshi linakuja kutoka kaskazini, taifa kubwa na wafalme wengi

wameamshwa kutoka miisho ya dunia. 42 Wamejifunga pinde na mikuki,

ni wakatili na wasio na huruma. Wanasi kika kama bahari inayonguruma

wanapoendesha farasi zao, wanakuja kama watu waliojipanga kwa

vita ili kukushambulia, Ee Binti Babeli. 43 Mfalme wa Babeli amesikia habari kuwahuusu hao, nayo mikono yake imelegea. Uchungu umemshika, maumivu kama yale ya mwanamke aliye katika utungu wa kuzaa..." (Yeremia 50:41-43).

3Ee Gogu, mimi ni kinyume nawe, mtawala mkuu wa Roshi, Mesheki na Tubali.. 6 kaskazini ya mbali pamoja na vikosi vyake vyote, mataifa mengi wakiwa pamoja nawe.. (Ezekiel 38:3, 6).

Hivyo, Milki ya Ulaya ("binti wa Babeli") itaangamizwa na jeshi toka kaskazini (yaonekana likiongozwa na Urusi). Jeshi ambalo yaonekana litakuwa limeungana na kushirikiana na majeshi toka mataifa ya Mashariki, ikiwemo pia pengine Iran, na hata Ukraine. (Wakati kutimizwa kwa Ezekiel 38 kutatokea baadaye, ukweli kwamba unataja juu ya watu toka KASKAZINI YA MBALI inasaidia kuonyesha kwamba kuna mamlka ingine iliyoko kaskazini zaidi mwa mamlka ya mwisho ya Ulaya ambayo ndiyo mafalme wa Kaskazini, inayopatana na Danieli 11:44).

Elewa, pia kwamba Biblia yaonyesha kwamba Babeli iliangamizwa kwa maumivu ya uzazi na kundi kutoka nchi ya mbali:

1 Neno kuhusu Babeli ambalo Isaya mwana wa Amozi aliliona: 2 Inueni bendera juu ya mlima usio na kitu, wapaziensi sauti, wapungjeni mkono waingie katika malango ya wenye heshima. 3 Nimewaamuru watakatifu wangu, nimewaita mashujaa wangu waitimize hasira yangu, wale wanaoshangilia ushindii wangu. 4 Sikilizeni kelele juu milimani, kama ile ya umati mkubwa wa watu! Sikilizeni, makelele katikati ya falme, kama mataifa yanayokusanyika pamoja! BWANA Mwenye Nguvu anakusanya jeshi kwa ajili ya vita. 5 Wanakuja kutoka nchi za mbali sana, kutoka miisho

ya mbingu, BWANA na silaha za ghadhabu yake, kuangamiza nchi yote. 6 Ombolezeni, kwa maana siku ya BWANA i karibu, itakuja kama uharibifu kutoka kwa Mwenye Nguvu. 7 Kwa sababu ya hili, mikono yote italegea, moyo wa kila mtu utayeyuka. 8 Hofu itawakamata, uchungu na maumivu makali yatawashika, watajinyonganyonga kama mwanamke aliye na utungu wa kuzaa. Watatazamana kwa hofu kila mtu na mwenzake, nyuso zao zikiwa katika hali ya kuwaka kama moto (Isaya 13:1-8).

Hivyo, maelezo yote, lile toka kitabu cha Yeremia na lile toka Isaya yaonekana kuelezea wavamizi walewale. Haya ni maelezo ya muungano wa nyakati za mwisho, namna ya umoja wa mamlaka kutoka mashariki utakaoihusisha Urusi, ambayo ndiyo mamlaka kuu ya kaskazini ya mbali.

Na aina hii ya mwunganiko ndicho chombo ambacho Vladimir Putin amekuwa akikitaja mara kwa mara. Hili ndilo swala atakaloendelea kulitetea na kujibidisha nalo. Japo hata kama atakuwa ndiye mkuu wa chombo hicho ama la, bado muungano huo utaanzishwa.

Umoja wa kaskazini (uonekana kuwa utaongozwa na Urusi na yamkini unaonekana kuhusisha kaskazini ya mbali na mashariki ya mbali/sehemu ya pwani ya Pacific ya Asia) utaangamiza Babeli ya Kiulaya. Mafungu yafuatayo nayo pia yanafafanua juu ya swala hili:

9 Kwa maana nitaamsha na kuleta dhidi ya Babeli muungano wa mataifa makubwa kutoka nchi ya kaskazini. Watashika nafasi zao dhidi yake, naye kwa kutokea kaskazini atatekwa. Mishale yao itakuwa kama mishale ya mashujaa walio hodari ambaeo hawawezi kurudi mikono mitupu (Yeremia 50:9).

Hivyo, japo wengi wanawasiwasi kwamba Urusi itakuja kuwa tishio kubwa la kijeshi kwa Marekani, ukweli halisi ni kwamba Biblia yaonyesha kwamba ni watu wa Ulaya ndio watakaokabiliwa na uvamizi mkubwa toka kwa mataifa yaliyo na Urusi. Na pengine siyo miaka mingi tangia sasa (kadri ya miaka  $3\frac{1}{2}$  baada ya kuanza kwa Dhiki Kuu). Huu Umoja wa Eurasia ndicho chombo ambacho Vladimir Putin anakiteteta na anatarajia kuendelea kujibidisha katika kuhakikisha kinafanikiwa.

Jionee yafuatayo:

13 Malaika wa sita akaipiga tarumbeta yake, nami nikasikia sauti ikitoka katika zile pembe nne za madhabahu ya dhahabu iliyoko mbele za Mungu. 14 Ille sauti ikamwambia yule malaika wa sita mwenye tarumbeta, "Wafungulie wale malaika wanne waliofungwa kwenye ule mto mkubwa Eufrati." 15 Basi wale malaika wanne wakafunguliwa ambaeo walikuwa wamewekwa tayari kwa ajili ya saa hiyo na siku hiyo na mwezi huo na mwaka huo ili wawaue theluthi ya wanadamu. 16 Idadi ya majeshi wapandao farasi ilikuwa 200,000,000. 17 Hivi ndivyo nilivyowaona hao farasi na wapanda farasi katika maono yangu: Wapanda farasi walivaa dirii vifuanini zenye rangi ya moto na yakuti samawi na kiberiti. Vichwa vya hao farasi vilikuwa kama vichwa vya simba. Moto, moshi na kiberiti vilitoka vinywani mwao. 18 Theluthi ya wanadamu wakauawa kwa maafa hayo matatu, yaani,

huo moto, moshi na kiberiti, vilivyotoka kwenye vinywa vya hao farasi (Ufunuo 9:13-18).

Jeshi kubwa namna hii laweza kupatikana wapi?

Ni kutoka majeshi ya nchi za Asia pekee, nchi kama vile China ama India napengine nchi zingine pia zitakazoshikamana nazo, huko ndiko pekee tuwezako kupata askari wengi kuweza kufikisha jeshi la watu milioni mia mbili. India, China, na nchi zingine za Asia yaonekana watashikamana na Urusi katika muungano dhidi ya Milki ya Ulaya.

Jionee kile ambacho Yoeli 2 inaashiria ni nini baadhi ya hao askari milioni mia mbili watakachokifanya:

2....jeshi kubwa na lenye nguvu linakuja. Jambo kama hili halijakuwapo tangu zamani wala halitakuwapo tena kamwe. 3Mbele yao moto unateketeza, nyuma yao moto unawaka kwa nguvu. Mbele yao nchi iko kama bustani ya Edeni, nyuma yao jangwa lisilofaa, hakuna kitu kinachowaepuka. 4Wanaonekana kama farasi, wanakwenda mbio kama askari wapanda farasi. 5Wanatoa sauti kama magari ya vita, wanaporukaruka juu ya vilele vya milima, kama mlilo wa miali ya moto ilayo mabua, kama jeshi kubwa liliojipanga kwa ajili ya vita. 6Wanapoonekana, mataifa yanakuwa katika maumivu makuu, kila uso unabadijika rangi. 7Wanashambulia kama wapiganaji wa vita. wanapanda kuta kama askari. Wote wanatembea katika safu, Hawapotoshi safu zao. 8Hakuna anayemsukuma mwenzake, kila mmoja anakwenda mbele moja kwa moja. Wanapita katika vizuizi bila kuharibu safu zao. 9Wanaenda kasi kuingia mjini, wanakimbia ukutani. Wanaingia ndani ya nyumba, kwa kuingilia madirishani kama wevi (Yoeli 2:2-9).

Jeshi hilo kuu litasababisha kitisho na uangamifu mkubwa.

## **Umoja wa Eurasia Utaanzishwa**

Vladimir Putin anataka Umoja wa Eurasia uundwe. Urusi imechukua hatua kadhaa kujaribu kushirikiana na yale mataifa ambayo hapo zamani yalikuwa sehemu ya Muungano wa Kisovieti. Lakini hata zaidi ya hapo, Urusi pia imechukua hatua za kujaribu kuboresha ushirikiano na Korea ya Kaskazini, China, India, Pakistan, na mataifa mengine mengi.

Ukweli kwamba Biblia inayataja mataifa haya kama "Wafalme wa Wamedi" au "Wafalme wa Mashariki" inaashiria kwamba hatua ya mwisho ya umoja huo itakuwa ni aina ya muunganu/ ushirikiano na wala si taifa moja.

Biblia inaelezea juu ya wakati ambapo wafalme hao wataunganika na kufanya umoja na hatimaye wataangamiza sehemu kubwa ya Milki ya Babeli ya mwisho ambayo wazungu wa Ulaya wataijenga.


Jumuia ya Eurasia ambayo inaundwa kwa sasa inaweza kuwa ndiyo utangulizi wa kupelekeea kwenye ushirikiano wa mwisho utakaoyahusisha mataifa mengi ya eneo la Eurasia.

Lakini hata iwapo vyombo vilivyopendekezwa kuanzishwa kwa sasa kama EAU ama SCO vikishindikana, ukweli ni kwamba Biblia

ikowazi kwamba katika nyakati za mwisho, muungano wa nchi za Eurasia utaanizishwa na utahusika na uangamifu wa mamlaka ya Babeli ya nyakati za mwisho ambayo wazungu wa Ulaya wako katika harakati za kuijenga.

Matukio ya habari yanathibitisha kwamba Urusi, China, na wengine wanajibidisha kuwezesha kuongeza uwezo na mamlaka ya eneo la Eurasia katika ulimwengu. Hili ni eneo ambalo Biblia inalitabiri litahusika na vita kubwa mwishoni mwa zama hizi.

# KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA



## Somo la 3: Kristo Atazuia Kujiangamiza Kwa Dunia

Bob Thiel, Mhariri Mkuu

Imechapishwa 2014 na Kanisa la Continuing Church of God

Utangulizi: Kozi hii kwa kiasi kikubwa inatokana na kozi kwa mawasiliano ilioanzishwa mwaka 1954 ilioanza chini ya usimamizi wa marehemu C. Paul Meredith enzi za Radio Church of God. Maeneo kadhaa yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo sehemu kubwa ya mafundisho ya awali imebaki kama ilivyo). Pia tumeongeza nukuru za Maandiko, taarifa na maswali ambavyo havikuwemo katika kozi ya awali.

USTAARABU UMEFIKIA NJIAPANDA! MWANADAMU akiachwa ye ye mwenyewe ATAJIANGAMIZA na kujifutilia mbali toka uso wa dunia endapo Mungu atashindwa kuingilia kati (Mathayo 24:22)! Lakini sasa, MUNGU HAWEZI KUSHINDWA! Mungu hatauachia ulimwengu huu uendelee kama ambavyo umekuwa ukijidesha. Hata hivyo, chakushangaza kusema, wengi wa wale waaminio uwepo wa Mungu, wanakataa kuamini kwamba atajiingiza kwa uwezo wa kiMungu katika maswala ya ulimwengu.

Ni juu ya kipindi hiki chenyeh mashaka cha siku za mwisho, punde tu kabla Kristo hajarudi, ambacho Petro anazungumzia: "3Kwanza kabisa ni lazima mfahamu ya kwamba SIKU ZA MWISHO watakuja WATU WENYE DHIHAKA wakidhihaki na kuzifuata tamaa zao mbaya. 4na KUSEMA, "IKO WAPI ILE AHADI YA KUJA KWAKE? TANGU BABA ZETU WALIPOKUFA, KILA KITU KINAENDELEA KAMA KILIVYOKUWA TANGU MWANZO WA KUUMBWA." (2 Petro 3:3-4).

Lakini Kristo atarejea kuja kuzuia ulimwengu kujiangamiza wenyewe!

MATAIFA WATAKASIRIKA wakati huo. Mapambano mionganoni mwao kwa ajili ya umiliki wa ulimwengu yatakuwa yamefikia kiwango cha hatari! UHARIBIFU MKUBWA NA UANGAMIVU MKUBWA WA UHAI WA WANADAMU UTAKUWA UMETOKEA.

Vita itakuwa KALI SANA! Kisha—ghafla—KRISTO ATATOKEA akiwa pamoja na malaika zake watakatifu, naye atajiingiza kwenye mapambano yao. MATAIFA HAWATAJITO A KWA KUMTII KAMA KONDOO kama wengi wadhaniavyo pasipo ushahidi!

Wao watadhani kwamba jeshi la Kristo pengine ni ama kundi jingine la wanadamu wa kawaida ambao wamebuni teknolojia ya kisasa zaidi ya kivita ya kutaka kuitawala dunia ama ni kundi liongozwalo na Ibilisi sawa na majeshi ya Mpingakristo! Yesu atalazimika kuyashughulikia majeshi ya watu wa mataifa kupitia katika lugha pekee wawezayo kumwelewa—kipigo kikubwa, cha jeshi la malaika lenye nguvu. Mataifa watajikuta hawana njia ya kugeukia.

Watajikuta fahamu zao zimeathirika kiasi cha kugeukiana wao kwa wao kwa kushambuliana na kuangamizana! Mpambano huu utamalizikaje?

KRISTO ATAYAANGAMIZA MAJESHI NA SILAHA ZAO NA KUWAACHA MATAIFA BILA YA UWEZO WOWOTE WA KUUUPINGA UTAWALA WAKE! NI YEYE, SIYO MWANADAMU, NDIYE ATAKAYEKUWA MKUU JUU YA DUNIA! Kristo anakuja kuzuia wanadamu kuangamizana na kuufuta uhai wote toka juu ya nchi jambo ambalo limezungumzwa sana na Biblia. Huu ni sehemu ya mpango muhimu wa KUSUDI la Mungu.

Lakini ni jinsi gani KRISTO ATAFANYA KATIKA KULETA UTULIVU KWENYE ULIMWENGU HUU, ULIOJAA VURUGU?

### Utaratibu wa Kuondolewa Machafukoni

Kristo, mwenyewe, alitangaza: "NITAKUJA TENA" (Yohana 14:3). Jinsi atakavyorudi ni swala ambalo limefanywa na maneno ya malaika liwe ni jambo lisilo na mashaka. Walitokea kwenye Mlima wa Mizeituni wakiwatoka Mitume ambao walikuwa wakishuhudia Bwana wao akipaa mbinguni. Malaika hao wakasema: "Huyu Yesu yuleyule, aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda Mbinguni, ATARUDI TENA JINSI HIYO HIYO mliyomwona akienda Zake Mbinguni" (Matendo 1:11). Yesu atarejea kwa mtindo uleule SAWA NA ALIPOENDA!

Hivyo Kristo atakuja KIUHALISIA na KWA KUONEKANA wazi, kuja kwenye dunia hii. Pale ajapo tena, atakuja, siyo kama atesekaye, wala si kama mtu mwenyewe simanzi, bali anakuja kama MFALME na kama MSHINDI, kuja kuketi juu ya taji la utukufu. Maneno yake mwenyewe alisema: "Mwana wa Adamu atakapokuja katika utukufu wake na malaika wote watakatifu pamoja naye, NDIGO ATAKAPOKETI JUU YA KITI CHA ENZI CHA UTUKUFU WAKE" (Mathayo 25:31).

Utabiri ni mwingi sana katika Biblia ukisema kwamba Yesu Kristo atamiliki KITI CHA ENZI, na kutawala akiwa kama Mfalme juu ya kiti hicho. Mungu ametangaza: "Siku zinakuja, nitakapomwinulia Daudi Tawi lenye haki, MFALME ATAKAYETAWALA KWA HEKIMA na kutenda lililo haki na sawa KATIKA NCHI" (Yeremia 2 3:5).

Kristo atamfanya SHETANI, MFALME ATAWALAYE KWA SASA MIONGONI MWA WANADAMU, akamatwe na afungwe (Ufunuo

20:2). Kisha, katika muda huo, "BWANA atakuwa MFALME JUU YA DUNIA YOTE. Katika siku hiyo atakuwepo BWANA mmoja na jina lake moja" (Zekaria 14:9).

## Maelekezo Muhimu ya Mwisho

Sasa tuko tayari kwa ajili ya somo lenyewe. Je, Biblia yako iko mbele yako? Kama haiko, tafadhari usiendelee kusoma zaidi kozi hii! SIMAMA HAPA! NENDA KALETE BIBLIA yako.

Vilevile kumbuka kuandaa karatasi kadhaa, pamoja na penseli ama kalamu, ili uweze KUCHUKUA NOTISI zitakazokuwezesha kukumbuka kile unachojifunza.

Kozi hii imejikita kwenye nakala ya Bibilia iitwayo New King James Version (NKJV) kwa kuwa imekusudiwa iwe ni tafsiri ya neno kwa neno na inatumia aina ya lugha ya Kiingereza ambayo inazungumzwa katika karne hii ya 21. Kwa mengi katika somo, waweza kutumia nakala zingine za tafsiri ya Biblia, lakini maswali na majibu hususani yanalenga tafsiri ya NKJV labda pale tu patakapoelekezwa. Hivyo, kwa wengi, nakala ya NKJV ndiyo chaguo bora la kutumia katika Kozi ya Kujifunza Biblia.

Sasa tuko tayari kuanza kujisomea kozi hii. KUMBUKA unapaswa uifungue Biblia yako ili kujithibitishia kila aya tunayotoa kama kieleelzo cha kile tunachosema katika kozi hii. Usiamini tu kile tukisemacho (timu ilioongozwu na marehemu C. Paul Meredith na/ama Bob Thiel)—amini kile ambacho Biblia inakifundisha.

Unapaswa USOME, na kurudia tena kusoma, na kwa kweli ujifunze KILA AYA KATIKA BIBLIA YAKO. Hii ni kozi ya KUJIFUNZA Biblia—ni kujisomea Biblia, siyo tu kujisomea haya maneno tunayokutumia. Maneno yetu yamekusudiwa tu yakuongoze kufika pale unakotakiwa kuangalia katika Biblia yako—ni kukusaidia ujue namna ya kujifunza Biblia.

Sasa, ukiwa na Biblia yako, KAMUSI (DICTIONARY) kama unayo, na karatasi zako za kuandika na penseli ama kalamu zote juu ya meza yako mbele yako, mfumo wa kujisomea utakuwa kama ifuatavyo: Andika kwa ufasaha kwenye karatasi yako, kichwa cha somo: "Somo la 3, Sehemu ya 1," na upapigie mstari chini yake. KIANDIKE KICHWA CHA SOMO pamoja na kila kichwa cha sehemu ya maswali. Kisha, chini yake andika namba ya kila swali, na uandike jibu kwa kila swali, kwa mwandiko wako mwenyewe (baadhi yenu mwawenza kuamua kuandika kwa computer ama typewriter).

Kama MFANO, kwa ajili ya kipengele cha swali, hiki ndicho kichwa cha somo utakachoandika kwenye karatasi ama notebook yako: Kristo Atakuwa Akiwa na Ghadhabu:

1. Danieli 2:28—"Lakini yuko Mungu mbinguni afunuaye siri. Amemwonyesha Mfalme Nebukadneza kitakachotokea SIKU ZIJAZO..."

Vilevile andika mawazo yoyote ama vipengele unavyohitaji kuvikumbuka. Jisomee na kujitahidi kulielewa swali, na ndippo uende kwenye swali linalofuata.

Yahifadhi masomo haya pamoja na notisi zako zenyе majibu

kwenye faili ama binder. USITUTUMIE MAJIBU YAKO KWA MASWALI HAYA ya SOMO. Yahifadhi kwa ajili ya kujikumbusha. (Inawezekana pengine tutatoa cheti (certificate) kwa wale watakaokamilisha kozi yote au hata sehemu kubwa ya kozi hii, ila hili litakuwa ni baada ya mwaka 2014, na tutalitangaza hili kupitia mtandoa na sehemu zingine. Endapo tutafikia kufanya hivyo, basi tutakuomba ututumie nakala za masomo uliyokamilisha).

2. Swali la pili la Somo la 3 linapaswa lifanyike sawa na swali la kwanza, isipokuwa tu hauhitaji unakili aya zote. Aya ya 42 na ya 44 ndizo zilizo muhimu zaidi kwenye kipengele hiki na ndizo unazopaswa kuzinakili ama kuzi-type.

Kwa kuyaandika majibu kwa maswali haya, na pia kwa kuandika notisi zitokanazo na aya za Biblia unazojifunza kwa kila swali, utakuta kwamba inakuwezesha KUKUMBUKA yale uliyojifunza. Inachukua muda zaidi kidogo kwa kufanya hivyo, lakini hii ndiyo itakusaidia KUJIFUNZA masomo yako vema, na kuyakumbuka baadaye.

Kwa kuandika kile unachojifunza itakusaidia kukumbuka vema.

Halikadharika, ITAKUWEZESHA KUFANYA MAPITIO YA MASOMO YAKO KWA HARAKA, kila ihitajikapo, endapo utakuwa nayo katika mtindo huu. Vilevile, itakusaidia sana katika kuifafanua Biblia kwa wengine.

TUNAKUPATIA DONDODA ZA BIBLIA ZA UKWELI KWA UFUPI NA KWA UFASAJA. Utahitaji kufanya marejeo kwenye masomo haya na MAELEZO YAKE ukitumia sasa ufanuzi wako mwenyewe kwa miaka mingi ijayo kila utakapo yatumia kufafanua vipengele mbalimbali katika Biblia. Kumbuka, utahitaji kutumia angalau nusu saa kila siku ukijisomea BIBLIA YAKO ukitumia hii Kozi ya Kujifunza Biblia.

## SOMO La 3

### Kristo Atarejea Akiwa na GADHABU

1. Ni kwa nani Mungu ALIFUNUA kile KITAKACHOTOKEA KATIKA SIKU ZA MWISHO? Danieli 2:28.
2. Je, kilitakiwa kuwe na milki za ulimwengu zitakazofuatana mara nne, zikitawala falme? Danieli 2:31-40. (Somo la baadaye litafafanua umuhimu kamili wa kila milki hizi nne). Katika siku za wafalme wa mwisho kumi (wakiwakilishwa na vidole kumi vya aya ya 42), ambao bado hawajainuka kutohama na milki ya nne, je, Mungu ATAUSIMIKA UFALME/ MILKI AMBAO KAMWE HAUTAANGAMIZWA? Danieli 2:44.
3. Jiwe litawaangamiza hawa wafalme kumi wa mwisho. Jiwe hili ni nani? Matendo 4:10-11. Je, LILIGONGA ile sanamu kwenye vile vidole kumi vya miguu? Danieli 2:34.
4. Ni wapi pengine ambako tukio la mwisho wa ufalme huu limefafanuliwa? Ufunuo 17:12-14. Je, hapa pia wafalme Kumi wametajwa?
5. Huyu aliyatajwa katika Ufunuo 19:11 ATAFANYA VITA?

Anaitwa Mfalme wa Waafalme na Bwana wa Mabwana (Aya 16). Huyu hasa ni nani? Ufunuo 17:14. Mwana Kondoo wa Mungu ni nani? Yohana 1:29. Je, Aya hizi zinaonyesha kwamba ni Kristo na ndiye atakayeku na jeshi la malaika kuja kufanya vita na majeshi ya dunia?

6. LENGO la kuja kwake litakjuwa ni nini? Ufunuo 19:15. Ni nini kitakachotokea kwa watu mashuhuri ambao watampinga? Aya za 17-18.

MAELEZO: Msemo “nyama ya watu WOTE”, upatikanao katika Ufunuo 19:18 haumaanishi watu WOTE walioko duniani, bali WOTE ambao wamo katika majeshi yaliyojikusanya dhidi ya Yeruselemu. Linganisha na Zekaria 14:12-15.

7. Je, Ufunuo 11:15-19 inazungumzia juu ya kipindi kilekile? Tunawezaje kujua? Aya ya 15. Je, malaika huyu ni wa mwisho mionganoni mwa malaika saba watakaopiga baragumu? Ufunuo 8:6.
8. Je, hii ni BARAGUMU ya SABA? Linganisha 1 Wathesalonike 4:15 na 1 Wakorintho 15:52. Je, Baragumu katika 1 Wakorintho 11:52 ndiyo Baragumu ya mwisho? Tambua hakuna tena baragumu iliyopulizwa baada ya Ufunuo 11:15. Je, FALME ZA ULIMWENGU HUU ZITAFANYIKA KUWA FALME ZA KRISTO pale baragumu ya saba – ya mwisho itakapolia? Aya 15.

9. Kristo alikuja safari ya kwanza akiwa kama mwanakondoo mpole aendaye kuuawa. Je, pale ajapo mara ya pili atarudi akiwa na hali gani? Je, Kristo atakuja akiwa mwenye GADHABU? Ufunuo 11:18. Je, Nabii Sefania alitabiri kuhusu KIPINDI hiki cha GADHABU YA MUNGU? Sefania 1:15. Je, SIKU KUBWA YA BWANA ndiyo SIKU YA GADHABU YA MUNGU kwa wakazi wa dunia? Aya za 14-16.

MAELEZO: “Siku ya Bwana” INAHUSISHA KUPULIZWA KWA BARAGUMU ZOTE SABA, sita mionganoni mwake zitapulizwa ndani ya kipindi cha miezi kadhaa punde tu kabla ya kurudi kwa Kristo.

10. Soma pia Isaya 13:6; Ezekieli 7:19, na Isaya 34:8. Je, aya hizi zinathibitisha pasipo mashaka juu ya “Siku ya Bwana” ni kitu gani?
11. Wengi wanaamini kwamba ulimwengu hivi karibuni utakuwa na amani. Je, Biblia yasemaje juu ya hili? Ufunuo 11:18. Pale watu wawapo na hasira, wengine hupigana. Je, kutakuwepo na MAPIGANO YA ULIMWENGU MZIMA katika nyakati hizi za mwisho? Mathayo 24:7; Ufunuo 19:19-21.
12. Ni kwanini Kristo atazichukua na kujimilkisha falme hizi za ulimwengu? Ufunuo 11:15-19 inatupatia baadhi ya sababu. Isome.

MAELEZO: MUNGU ANAHITAJI WATU WAMTII. Anasema: “Jihadharini msimsahau BWANA Mungu wenu, mkashindwa kushika maagizo yake, sheria na amri zake . . .” (Kumbukumbu la Torati 8:11). Katika Ufunuo 11:19 Mungu anatoa picha ya SANDUKU LA AGANO. Ebu na tuelewe kwa nini!

Je, Sanduku la Agano la hapa Duniani lilikuwa na vitu gani? 2 Mambo ya Nyakati 5:10; Kumbukumbu la Torati 10:4-5. Je,

Ulimwengu wa leo unashika amri za Mungu? Je, watu wa leo wanaiharibu nchi? Ufunuo 11:18. “Usiue” ni mojawapo ya amri hizi, Kutoka 20:13.

Hivyo sasa tumetambua kwamba Kristo atareje akiwa amejaajadhabu kuja kuyaadhibu mataifa kwa sababu YANAZIVUNJA AMRI ZA MUNGU!

13. Biblia inaonyesha kwamba watakatifu, pale Kristo ajapo mara ya pili, watabadirishwa na kuishi daima pamoja naye 1 Wathesalonike 4:17. Watu walio wengi leo wanaamini kwamba pale watakapobadirishwa wataishi maisha ya uvivu. Pale Kristo pamoja na majeshi yake ya malaika watakapoanza kuwadhibiti mataifa, je, watakatifu wao watakuwa hawana kabisa kitu chochote cha kufanya? Soma Danieli 7:18. Je, neno “Wataupokea” hasa linaashiria kitu gani?

Waongofu si kwamba wataishi maisha ya kukaa tu bila shughuli yoyote pale watakapobadirishwa. Watashiriki kwa kiwango kikubwa pamoja na Kristo katika kuzimilki falme za ulimwengu huu.

14. Ni nini kingine kitakachotokea wakati wa kupulizwa kwa baragumu kuu (ya saba) ambapo ndipo Kristo anakuja? Isaya 27:12-13. JE, ISRAELI WATAKUSANYWA TENA? Aya ya 12. Ni nini watakachokifanya? Aya ya 13.

Iwapo watamwabudu Mungu na kutoka kwenye huu ulimwengu wa Kibabeli ambako ndiko walikokuwa wametawanyikia; je, wataepuka mapigo yake yajayo? Ufunuo 18:4.

### Gadhabu ya Kimungu Kuja kwa Ulimwengu Usioshika Sheria

1. Ulimwengu ni muasi. Hata pale baada ya Kristo kuwa amekuja yeye binafsi hapa duniani, bado mataifa hawatampokea. Ni jambo gani moja ambalo Mungu atalifanya kuchoechea KUKUBALIWA KWA KRISTO pamoja na serkali yake? Ufunuo 16:1.
2. Ni juu ya nani hivi VITASA VYA GADHABU vitaangukia? Je, si juu ya ulimwengu wote muasi? Ufunuo 16:1.
3. Je, kuna vitasa vingapi? Ufunuo 16:2, 3, 4, 8, 10, 12, 17. Je, kuna yeyote mionganoni mwa hivi “vitasa” saba vya gadhabu ya Mungu ambavyo pia vinaitwa “Mapigo”? Linganisha aya ya 17 ya Ufunuo 16 na aya ya 21.
4. Je, Mapigo haya yataipiga Babeli ya nyakati za mwisho? Ufunuo 18:8.
5. Ni juu ya nani KITASA CHA KWANZA kilimiminwa? Ufunuo 16:2.
- MAELEZO: Pale Kristo ajapo tena, Kitamiminwa juu ya wote ambao wanashiriki katika mfumo wa ulimwengu huu wa kijamii na kidini.
6. Tunawezaje kujua kwamba kitasa cha kwanza kitamiminwa

BAADA ya Kristo kuja? (Kumbuka kwamba Kristo anarejea wakati wa baragumu/parapanda ya mwisho--Ufunuo 11: 5. Baragumu hii ndiyo inayoanzisha mapigo saba ya mwisho).

7. Mataifa wao watafanyaje pale wamwonapo Kristo akirudi? Ufunuo 11:18. Je, huo ndio pia utakaokuwa wakati wa gadhabu ya Mungu? Aya 17-18. Kwa vile vitasa vyote vinawakilisha gadhabu ya Mungu (Ufunuo 16:1), ni wazi kiasi gani kwamba vitamiminwa BAADA ya Kristo kujiingiza kwenye maswala ya ulimwengu.
8. VITASA VYA PILI na VYA TATU vitamiminwa juu ya nani? Vitasababisha madhara gani? Ufunuo 16:3-7. Tambua kwamba VITASA VYOTE HIVI VITASABABISHA MATOKEO YASIYO YA KIASILI. MUNGU ATAJIINGIZA KATIKA MASWALA YA ULIMWENGU KUPITIA MAPIGO HAYA YASIYO YA KIASILI!
9. Mungu atatumia HATUA KALI. Ebu jionee juu ya KITASA CHA NNE. Ufunuo 16:8-9 (Kuna vitasa saba kwa ujumla). Je, JOTO lake litakuwa la madhara makubwa? Ni kwa kiwango gani kikuu mwanga wa jua utakavyokuwa kwa muda mfupi? Isaya 30:26.
10. Ni madhara gani yote haya yatasababisha kwa wakazi wa dunia? Isaya 24:6. Je, kwa ujumla ni DATU WACHACHE ZAIDI NDIO WATAKAOSALIA hai wakati wa mwanzo wa utawala wa Kristo?

MAELEZO: Tambua kwamba SI WANADAMU WOTE WATAANGAMIZWA—baadhi watabaki hai. Kupitia hawa Kristo ataanzisha utawala wake.

11. NI KWANINI Mungu atafanya hili? Isaya 24:5. Kristo atatekeleza gadhabu ya Mwenyezi juu ya dunia hii kwa sababu ya uasi wao wa sheria za Mungu.
12. Ni kipi kingine kinatuonyesha kwamba gadhabu ya Mungu itatokea pale Kristo aanzapo kuusimika utawala wake duniani? Isaya 24:10. “Mji wa Machafuko” ni kitu gani?

MAELEZO: Katika Kiebrania na Kigiriki, neno “Babeli” (Babylon humaanisha “machafuko”. Babeli Mkuu—mfumo wa ulimwengu huu uliochanganyikiwa amba ni chimbuko la mfumo wa Babeli ya kale—utaanguka mapema punde baada ya kujiingiza kwa Kristo (Ufunuo 18:2).

13. Je, Ufunuo 18:21, 23 nayo pia inathibitisha kwamba tukio hili litatokea katika muda huo? Mungu kwa hiyo ataangamiza idadi kubwa ya watu waasi watoke duniani kabla Kristo hajausimika ufalme wake. Je, wengi wa wale watakaosalia WATATUBU pale watakapokabiliwa na joto hilo kali sana? Ufunuo 16:9.
14. KITASA cha TANO kitamiminwa katika eneo la nchi ambalo litakuwa likitumiwa sana na wanadamu kupambana dhidi ya ufalme wa Kristo. Je, linaitwaje? Ufunuo 16:10. Je, watu hawa watatubu dhidi ya matendo yao maovu? Je, hapo kuna nuru? Je, Kristo anajilinganisha mwenyewe na nini? Yohana 8:12.

MAELEZO: Kwa dhahiri neno “giza” la Ufunuo 16:10 lina maana

mbili—kutakuwepo na GIZA KWELI kwa kukosekana mwanga—kuwepo mawingu mazito—lakinia pia “giza la kiroho” katika eneo lote la mfumo wa Mnyama ulipo. KATIKA BIBLIA kiunabii MAMBO MENGI YAMEANDIKWA KUMAANISHA MAMBO MAWILI KAMA HILI.

Wengi wameamini kwa kuchukulia kwamba wakazi wa dunia watamkulabi Kristo mara moja japo hata kama hawatamtambua pale mwanzoni. Inashangaza kujionea kile ambacho hasa ulimwengu huu utakachokifanya. Adhabu ya kitasa cha nne itakuwa ni adhabu kali sana. Itaua sehemu kubwa ya wakazi wa dunia hii. Katika historia yote, Shetani amempiga vita Kristo. Wengi watapotea kwa kuangukia “mafundisho ya mashetani” (1 Timotheo 4:1; Ufunuo 16:14) na kushindwa kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi.

Viongozi wa mfumo huu wa Babeli watapata adhabu hii na kupitia kwenye adhabu nyininge zaidi kwenye miji yao. Lakini bado hawatatubu. NGUVU ZAIDI, NA PENGINE HATA MUDA, VITAHITAJIKA ILI KUUSHINDA UPINZANI.

## Ulimwengu Utakusanya KUMPINGA Kristo;

### Kukusanyikia Harmagedoni

1. KITASA CHA SITA cha gadhabu ya Mungu kitakuwaje? Ufunuo 16:12, 14. Je, jina la SEHEMU WATAKAYO kusanya linaitwaje? Aya ya 16.
2. NI NANI ATAKAYE IKUSANYA DUNIA YOTE KUPAMBANA DHIDI YA MWUMBAJI WAO? Ufunuo Sura ya 16, Aya za 13 na 14. Joka ndiye nani? Ufunuo 12:9. Je, wale “roho/mapepo” ni MASHETANI wa IBILISI? Marko 1:23, 34; Luka 11:18-19.
3. Wale mapepo watafanyaje ili wawakusanye wanadamu pamoja? Ufunuo 16:14. Je, Yule “Mnyama” ni kiongozi mkuu wa kijeshi na kiutowala, mwenye mamlaka makuu dhidi ya majeshi mengi? Ufunuo 17:13-14. Je, Yule “Nabii wa Uongo” ni kiongozi mashuhuri wa kidini? Ufunuo 13:11-17.
4. Ni “dhidi ya nani” wafalme wote wa dunia pamoja na ulimwengu wote kwa ujumla watakusanya kumpiga vita? Ufunuo 17:14. (Tayari tumekwisha kuona kwamba “Mwanakondoo” inamaanisha Kristo. Tambua pia kwamba Kristo anayo pia majina na nyadhifa nyininge nyinyi: Soma Ufunuo 19:11, 16 na 19.) Mandiko haya NI DHAHIRI YANATHIBITISHA KWAMBA KRISTO PAMOJA NA SERKALI YAKE HAWATAKUBALIWA WALA KUPOKELEWA NA WANADAMU WATAKAOMUUNGA MKONO YULE MNYAMA.
5. Ufunuo 16:15 inafafanua jambo gani? Je, aya hii iliyosimikwa kama nyongeza inatoa onyo kwa watu wa dunia kwamba wajitahidi kujikita kwenye nabii za Mungu ili wasije wakahadaiwa na kujikuta nao wamehusika katika vita dhidi ya Mungu, ambavyo vitafuatia kukusanyika kwa mataifa kule Harmagedoni?

MAELEZO: Aya hii ya 15 ni wazo lililochomekwa kama ziada—ni

onyo kwa SISI WOTE! Haimaanishi kwamba Kristo atarejea baada ya vitasa vitano vyta kwanza kuwa vimemiminwa. Badala yake, hii ni onyo kwamba tusihusike na maandalizi hayo ya kijeshi ambayo ni dhahiri yataanza miezi kadhaa kabla Kristo hajareja.

KITASA CHA SITA KINAWAKILISHA MAPIGO YA KUTISHA YA KRISTO DHIDI YA MATAIFA. YANAANZA MARA WAJIKUSANYAPO KULE HARMAGEDONI KUTAKA KUPAMBANA NAYE.

6. Je, Mungu atawahukumu wapagani huko? Yoeli 3:12.

MAELEZO: "YEHOSHAPHATI", neno la Kiebrania, maana yake ni "Hukumu ya Yehovah". Hivyo eneo hilo mahsusini linajulikana kwa jina la "Bonde la Hukumu ya Mwenyezi".

7. Ni lini hukumu hii itafanyika? Aya ya 14 ya Yoeli 3. Linganisha wakati wa tukio hilo (la aya ya 14) na wakati wa tukio lililoelezewa katika Ufunuo 14:19.

MAELEZO: Mapigano haya yatafanyika kwenye Siku ya Gadhabu "KUU" ya Mungu—itakuwa ni siku ambayo vitasa vyote saba vya Baragumu ya saba vitakamilika. Siku hii ambayo ndiyo miguu ya Kristo itatua na kuikanyaga dunia itaanzishwa kwa kupulizwa kwa Baragumu ya Saba. Kama ambavyo tumetangulia kuonyesha, misemo ya "Siku ya Bwana" pamoja na ule wa "Gadhabu ya Mungu" mara kwa mara imetumiwa katika Biblia kumaanisha swala lilelile na hivyo inaelezea nyakati na tukio la aina moja. Je, si kwamba matukio haya mawili yanatukia katika wakati uleule? Je, si kwamba Mungu atachukua hatua ya kujiingiza katika maswala ya ulimwengu pale lolote baina ya mambo haya yatakapotekelawa?

8. Je, matukio haya yote yatatuifikisha katika "Siki ya Bwana"? Linganisha Yoeli 3:14 na Ufunuo 14:19-20. Je, si ukweli kwamba msemo wa damu itapanda hadi katika "Hatamu za Farasi" unaonyesha kwamba tukio hili linatendeka katika bonde?

MAELEZO: Elewa kwamba msemo "damu itatoka kwenye shinikizo la divai . . . kama mwendo wa maili mia mbili hivi"! Damu iliyotokana na askari waasi itafurika na kujaa eneo lote la bonde la Megido, linalotapaka tokechi ya Palestina hadi Yerusalem na kusambaa kiasi cha maili 110 kuelekea kusini hadi kwenye nchi ya zamani ya Edomu. Linganisha hili na Isaya 63:1-6, ambako Kristo amefafanuliwa kuwa anaitekeleza gadhabu yake katika nchi ya Edomu. Langalie ramani ya Kibiblia ya eneo la Palestina ili uyaone na kuyatambua maeneo haya.

### Damu Itamwagika Kutokana na Uasi

1. Linganisha Yoeli 3:13 na Ufunuo 14:19. Je, matukio ambayo yanafafanuliwa katika aya hizi yanahuusu mavuno?

MAELEZO: Elewa kwamba hukumu kama ilivyoeliezewa katika aya hizi zote inafananishwa na mavuno ambapo zabibu (ikiwakilisha watu waovu) ya gadhabu ya Kristo zitakamuliwa. Mvinyo wake utakaotokana na kukamuliwa huko kunalinganishwa na MAVUNO YA DAMU.

2. BONDE LA YEHOSHAPHATI ni eneo lenye kina kirefu na pana lenye kingo kali, ambalo linapakana na mji wa Yerusalem

upande wa mashariki. Je, si kwamba hata mavuno ya Ufunuo 14:20 nayo yatafanyikia nje ya mji?

3. Ni nani ambaye atatekeleza jambo hili la mavuno ya Mungu? Ufunuo 14:14. "Mwana wa Mtu/Adamu" ndiye nani? Danieli 7:13-14; Mathayo 9:6.
4. Ni kipi atakachokifanya pale atakapokuja? Fungua Ufunuo 19:11. Je, si kwamba atawahukumu pia katika Bonde la Yehoshaphati? Je, atarejea akiwa na majeshi? Aya ya 14. Je, watu wa dunia watapambana dhidi yake? Aya ya 19. Si kwamba yeche, akiwa na majeshi yake, "atakanyaga SHINIKIZO la MVINYO wa hasira ya GADHABU ya MUNGU Mwenyezi"? Aya ya 19.

MAELEZO: Linganisha msemo huu wa Ufunuo 14:19 na Yoeli 3:12-13. Je, si dhahiri kwamba mapambano haya yatapiganwa katika BONDE LA YEHOSHAPHATI NA YATAKUWA NI VITA KALI YA KUHITIMISHA MAMBO? Vita vyenyewe vitatukia karibu na Yerusalem ambayo inapakana na bonde hili.

5. Isome pia Zaburi ya 2, zingatia aya ya 8. Je, si kwamba watakuweko pia wapagani kwenye Bonde la Yehoshaphati? Yoeli 3:12. Linganisha "Fimbo ya Chuma" ya Zaburi 2:9, na kile ambacho Kristo atatumia kuwavunjavanja, je, itakuwa kuititia fimbo hiihii ndiyo atakayotumia kuwatawala mataifa? Ufunuo 19:15.

Je, msemo huu hauhusishi pia majeshi? Je, haitakuwa Kristo, kuititia majeshi yake, ambaye ndiye "ATAKANYAGA MVINYO WA GADHABU YA MUNGU" KWENYE BONDE LA YEHOSHAFATI NA KUSABABISHA DAMU YA WAPAGANI WANAOMPIGA IMIMINIKE KATIKA SIKU YA VITA KUU KULIKO ZOTE ULIMWENGUNI?

6. Ni kwa nini mataifa watampiga vita Kristo? Zaburi 2:2-3; Ufunuo 11:8. Je, watahitaji aina ya serkali yake? Je KRISTO NDIYE ATAKAYESHINDA? Zaburi 2:9. Zingatia neno "kuwavunja".
7. Bonde la Yehoshaphati linapakana na YERUSALEMU. Je, Kristo ataichukua Yerusalem pia, kuititia vita hii? Zekaria 14:2-4. Je, Zekaria 14:2 inaonyesha kwamba nusu ya mji wa Yerusalem itakuwa ilikuwa imetekwa na mataifa ya dunia hii kabla Kristo hajaikombao kuititia vita hivi?

MAELEZO: Inawezekana sasa tukafahamu vema ni kwa nini vita vikubwa kuliko vyote ulimwenguni vitapiganiwa kwenye bonde la Yehoshaphati na wala si kule Harmagedoni! VITA HIVI NI KWA AJILI YA NANI AUTAWALE ULIMWENGU. Yerusalem, Makao makuu ya Serklai ijayo ya ulimwengu, ndio utakaokuwa kiini cha mapigano hayo.

"Konde/Mbuga ya Megido" ni eneo tambarare lipatikanalo kusini mwa uwanda mpana wa Esdraeloni. Ni uwanda ulioko kadri ya maili 70 kaskazini hadi magharibi mwa Yerusalem na umetumika mara kwa mara kama uwanja rasmi wa kupambanisa kwa sababu ya utambarare wake. Katika enzi za kale, ulikuwa unafanya sehemu ya njia panya kuu iunganishayo Asia na Africa. Kutokea kwenye huu uwanda mpana wa asili wa kukusanyikia, majeshi ya ulimwengu yatasongea kuelekea kusini kwa ajili ya mapigano

makubwa dhidi ya Kristo.

- Ni nani atakayemsaidia Kristo katika vita vyake vya "Siku ya Bwana"? Zekaria 14:5 pamoja na 2 Wathesalonike 1:7-10. Jionee Yeremia 25:30-33: Kristo atakanyaga "Shinikizo la Mvinyo" kila palipo na uasi! Ni kitu gani kitakachowapata wale watakaoenda kumpinga Kristo kule kwenye Vita dhidi ya Yerusalem? Zekaria 14:11-12. Kristo ndiye atakayeibuka mshindi.

Ni nini kinafuata punde tu mara ya KITASA CHA SABAS? Ufunuo 16:18-21.

### Matokeo ya Ushindi wa Kristo

- MATOKEO YA MAPIGANO YA KWENYE BONDE LA YEHOSHAPHATI YAMEELEZEWYA KATIKA MAENEYO MENGU MBALIMBALI YA BIBLIA KUTOKANA NA UMUHIMU WAKE. NI kipi ambacho Kristo amesema atakifanya dhidi ya Yerusalem na Mlima Sayuni pale arudipo? Zekaria 8:3.

MAELEZO: YERUSALEMU ni mji ambao Mungu ameuchagua uwe na sifa na matumizi makubwa zaidi mionganii mwa miji yote ya wanadamu. JINA LAKE LENYEWE LINAMAANA YA "JIJI LA AMANI".

HAPA TUNAMUONA KRISTO, "MFALME WA AMANI" (Isaya 9:6) AKIUTWAA MJI HUO WA AMANI KWA KUSUDI LA KUUFANYA UWE MAKAO MAKUU YA DUNIA (Yeremia 3:17). KUTOKEA SAYUNI, SHERIA ZA MUNGU ZITATOKA NA KUUNDEA ULIMWENGU WOTE, KITU KITAKACHOLETA AMANI KWA DUNIA YOTE! (Isaya 2:2-4). KRISTO ATAWAADHIBU WOTE WALE WATAKAOENENDA KINYUME NA MAELEKEZO YAKE.

- NI nini kitakachompata KIONGOZI WA KIJESHI wa mataifa hayo, Mnyama, ambaye atapambana na Kristo? Ufunuo 19:19-20.

MAELEZO: Hayo yanafafanua ZIWA LA MOTO NA KIBERITI lilelile, ambamo ndimo Mnyama—Kiongozi wa Kijeshi—atatupwa akiwa hai!

- "Mnyama" aliyetajwa hapa ni Kiongozi wa Kijeshi wa dunia ambaye ataungwa mkono kijeshi na wafalme madikiteta kumi ambao kwa pamoja watapambana na Kristo kwenye Bonde la Yehoshaphati? Ufunuo 17:12-14.

MAELEZO: Biblia hutumia usemi wa "wafalme kumi". Hawa watakuwa ni viongozi kumi watakaokuwa wakiiongoza Ulaya. Katika enzi za Biblia, usemi "mfalme" mara kwa mara ulitumiwa kumaanisha mtawala ambaye siku hizi tunaweza kumuita kama rais ambaye kwa siku hizi angeweza kuwa mkatili ama dicteta. Je, aya ya 14 kimsingi haithibitishi kwamba HUYU KIONGOZI WA KIJESHI ATASHINDWA?

- Sasa ebu jionee jambo jingine juu ya huyu kiongozi wa kijeshi. Ataendesa namna ya utawala usio wa kawaada. Soma Danieli 11:45. Tambua kwamba mtu huyuhuyu ametajwa mahali hapa tena kama kiongozi wa kijeshi ("naye ataondoka kwa ghadhabu nyingi ili kuangamiza na kuharibu kabisa

wengi"—aya ya 44). Pia ATAENDESZA ENEO NA SHUGHULI ZA IBADA ZA KIDINI—madhababu! Katika lugha ya kiBiblia, neno "madhababu" mara nyingi humaanisha sehemu ya kufanya ibada (mfano: Kutoka 27:21). Ni kwa nini ataendesa madhababu? Atalifanya hili kwa ajili ya KUJIPATIA WAFAUASI toka kwa wale wanadini waliopotoka, ili aweze kuendesa maswala yake ya kijeshi bila upinzani wa ndani. Yule "Nabii wa Uongo", "Mnyama atokaye katika Nchi", ataiunga mkono dini ya Mnyama huyu ya uongo (Ufunuo 13:11-17).

- Je, huyu NABII WA UONGO, ambaye ndiye atakuwa mkuu wa madhababu hiyo, ye ye naye atapokea ADHABU ILEILE kama ya Yule Mnyama aendeshaye majeshi ya vita? Ufunuo 19:20, pia Ufunuo 14:9-11. Je, bado pia upo unabii mwininge ambaao nao unathibitisha huyu mtu atapatwa na tukio hilo?
- Pale Kristo atakapowashinda na kuwateka hawa wafalme kumi, je, ataanza kutimiza ule unabii kwamba, "katika siku za wafalme hawa" (yaani wale wanaowakilishwa na vidole kumi), ndipo atakapousimika ufalme ambaao hautaangamizwa na mtu? Danieli 2:42-44.

MAELEZO: Pamoja na kwamba ni Mungu ndiye atakayempatia Kristo falme za ulimwengu wote ili azitawale pale Baragumu ya Saba Iipulizwapo, kusema kweli BADO UFALME HAUTAKUWA WAKE HADI KWANZA AWAPIGE MATAIFA NA KUWASHINDA. Linganisha Ufunuo 11:15 na Ufunuo 17:14.

---

### Ustaarabu Huu Uliobuniwa na Mwanadamu Utatupiliwa Mbali

#### Kristo Ataanzisha Ustaarabu Mpya

Muungano wa majeshi ya Ulaya sasa yatakuwa yameshindwa na kiwango kikubwa cha vifo kuwa kimetokea kwa wanadamu wote. MIJI mingi ya ustaarabu wa ulimwengu huu—"BABELI KUU"—ulimwengu wa kipagani ambamo ndimo tunaishi, bado itakuwa imesimama, hajaharibiwa, hatahivyo. HATA PIA "JIJI KUU" (Ufunuo 16:19), ambalo limeuendeleza mfumo huu wa kibinadamu tangia enzi za Milki ya Rumi, nalo bado litakuwa lipo.

- Je, Mungu ataiacha miji hii iendelee kusimama na kuwepo na atausimika utaratibu wake mpya mionganii mwake? Ama MENGU YA MAJENGO YA MFUMO WA ULIMWENGU HUU YATABOMOLEWA ILI KUUPISHA USTAARABU MPYA WA ULIMWENGU WA KRISTO? Ufunuo 16:18-21. Je, hizi ni nguvu mbili za asili ambazo atazitumia katika kutekeleza hili? RADI KUBWA PAMOJA NA MATETEMEKO MAKALI YATASAMBARATISHA NA KUBOMOA KABISA MAJENGO NA MIUNDOMBINU KARIBIA YOTE ILIYOJENGWA NA WANADAMU ULIMWENGUNI! Hiki ndicho KITASA CHA SABA!
- Mapigo ya mwisho manne mionganii mwa mapigo saba yataleta matokeo yasiyo na kifani; lakini, pamoja na haya yote, je, wanadamu watajifunza KUMCHA Mungu? Ufunuo 16:21. Je, hatimaye watajifunza na kutambua kwamba

mfumo bora zaidi ulikuwa unaanzishwa? Ama bado watataka WAENDELEE KUUNG'ANG'ANIA ULE MFUMO WA AWALI? Ufunuo 18:9, 11, 17-19. Mfumo huu mbovu ulikuwa na nini ambacho wanadamu bado wataendelea kukitamani hata baada ya Mungu kuwa ameuteketeza? Ufunuo 18:2-3, 14, 19.

3. Je huo ndio uliokuwa mtazamo siku za Lutu pale alipokimbia kutoka mji muovu wa Sodoma? Je, alitamani abakie japo kidogo ndani yake? Kwa kutazama nyuma akiuangalia? Kubakia karibu nao? Na je, ilikuwa ni kwa ajili ya mtazamo wa aina kama hii kwamba mkewe ALIUAWA? Mwanzo 19:16, 17, 20, 26.
4. Je, Mungu, ambaye ye ye anajua kwamba yapo mambo mema yanakuja, anawaamuru watu wake wafanye nini kuhusu kuanguka kwa ustaarabu wa leo kunakokuja—Babeli Kuu ya kileo? Ufunuo 18:20. HII NIA YA MWANADAMU YA KUENDELEA KUNG'ANG'ANIA USTAARABU wa leo JE, HAIONYESHI KWAMBA UTAHITAJIKA MUDA NA JUHUDI KUTOKA KWA KRISTO, WATAKATIFU, PAMOJA NA MALAIKA KATIKA KUWAELIMISHA UPYA WANADAMU JUU YA ZAMA MPYA? WATAHITAJI KUJIFUNZA KWAMBA NJIA YA MUNGU NDIYO ILIYO BORA.

**MAELEZO:** Upinzani mkuu dhidi ya Kristo utakuwa umedhibitiwa. Kiongozi mkuu wa kidini wa ulimwengu pamoja na kiongozi mkuu wake wa kijeshi watakuwa tayari wameangamizwa. Idadi kubwa ya waovu wasiotaka kutubu watakuwa wameuawa. Radi na umeme wa kiwango kikubwa pamoja na tetemeko kubwa mnno kuwahi kutokea duniani navyo vitakuwa vimeteketeza makazi ya idadi kubwa.

5. Ni kwa namna gani KRISTO sasa ATAISIMIKA AINA YAKE YA SERKALI, ambayo italeta amani duniani kote? Je, atajenga MJI WA MFANO KWA ULIMWENGU WOTE KUIGA? Jiji hili litakuwa ni lipi? Isaya 62:1-2. Je, dunia yote italijua jiji hilo? Aya ya 7.
6. Je Israeli ndio itakuwa MFANO KWA DUNIA? Yeremia 33:7-9. Ni makundi yapi mawili ambayo ndio yataunda taifa hili? Aya ya 7. Kuelimishwa kwao chini ya Kristo je, kutawaaletea nini? Aya ya 8. Je, TAIFA LA MFANO la Mungu LITASIFIWA hatimaye na MATAIFA MENGINE YOTE? Sefania 3:20 na Zekaria 8:3. Je, Yerusalem pia utaitwaje? Zekaria 8:3. Ukweli ndicho kitu muhimu zaidi kwa Mungu.
7. Taifa hili litakuwa limetoka wapi? Litakuwa linapatikana sehemu gani pale hatimaye litakapokuwa ni utukufu na sifa kwa dunia? Ezekiel 34:1, 12. ("Kondoo" ndio Israeli. Je, wametawanywa?) Je, ni wapi ambako watasimikwa kuishi? Aya ya 13. Je, si kwamba mji huu wa kuigwa utapatikana ndani ya eneo la taifa la kimfano?
8. Pamoja na kwamba Kristo atakuwa sasa ameushinda upinzani wa PAMOJA wa ulimwengu unaotawaliwa na mnyama, je, mataifa yote yatamfurahia ye ye na serkali yake? Au pengine ATAUANZA UTAWALA WAKE KATIKATI YA ADUI? Zaburi 110:2.
9. Ni kwa jinsi gani upinzani huo utakaosalia utakavyodhibitiwa? Hagai 2:22. Ataanza kufanya nini dhidi ya watawala waliosalia

wa ulimwengu huu? Zaburi 149:8. Je, vilevile ATAWAADHIBU WAPAGANI? Aya ya 7. Je, Kristo atamtumia nani katika kutekeleza mambo haya? Aya ya 5-9. Isome Zaburi yote. Je, wewe unaona hili linaonyesha kama watakatifu "wataenda mbinguni" na kuketi huko bila kazi yoyote?

Je, Kristo atachoshwa na jukumu lake hilo na kuachana nalo kwa vile LITACHUKUA MUDA NA KUHITAJI UVUMILIVU? Isaya 42:4. Ni nani yule "mtumishi wangu," aliyetajwa katika aya ya 1 ya Isaya 42? Lipate jibu lake katika Mathayo 12:15-18 na Wafilipi 2:5-7.

### Urusi na China Watajaribu Mapinduzi ya Mwishi

Urusi na China watakuwa ndio "Wafalme wa Mashariki" watakuwa mashuhuri katika nyakati za mwishi (Ufunuo 16:12). Jeshi lao walilouganisha na kuwa la askari wengi litaangamizwa kwenye Bonde Yehoshafati (Yoeli 3:12) pamoja pia na MUUNGANO wa majeshi ya Ulaya yote na mataifa mengine yaliyojikusanya dhidi ya Yerusalem.

1. Ni eneo lipi la ulimwengu litakalohusika dhidi ya Mfalme wa Kaskazini? Danieli 11:44. Tambua kwamba Mfalme wa Kaskazini (Danieli 11:40), alifadhaishwa na mamlaka iliyo kaskazini na masahariki yake. Jambo hili tunajifunza kutoka wapi pengine? Yeremia 50:41-43.

**MAELEZO:** Yeremia 50:1-3 na 51:7-11 zinaonyesha kwamba taifa toka kaskazini ama mataifa toka upande wa kaskazini (Yeremia 50:9,41) yataiangamiza Babeli na yanaweza kuwa katika mstari wa mbele wa kile kiwezacho kuwa ni mashambulizi ya nyukilia dhidi ya Rumi yenye (ona Ufunuo 18:9-10). Ni nchi za Scandinavia pekee, pamoja na zile za jumuia ya zamani ya Muungano wa Urusi (Soviet Union) ndio yaliyopo kaskazini kijiografia, mwa Ujerumani, ionekanayo kuja kuwa Mfalme wa Kaskazini. Na pamoja na kwamba ni mataifa mengi yako kaskazini mwa Yerusalem (na nabii nyangi yaonekana hutoa maelekezo ya upande kutokea mwelekeo wa Yerusalem), Maandiko mengi yanaashiria swala hili kuwalhusu wale walioko kaskazini ya mbali ya Eurasia.

Je, ni taifa lipi lenye nguvu kubwa za kijeshi lililoko kaskazini mwa Ulaya? Ni Urusi. Kinyume kabisa na madai ya wahubiri wengi wa Kiprotestant, Urusi SIYO "mfalme wa kaskazini" wa siku za mwishi, bali ndio inayohusika katika kumwangamiza!

2. Pale Urusi pamoja na washirika wake wa Eurasia watakapoona kwamba mamlaka ya Kibabeli ya mnyama yanaweza kuangamizwa, je, ndipo watakapochukua hatua? Yeremia 51:11-32; Isaya 13:1-8, 17-19. Je, si kwamba Urusi na China, tukitoa mifano miwili, ndio mataifa toka sehemu za "miisho ya nchi" (Yeremia 51:11; Isaya 13:5) kwa kuyaangalia kutokea uelekeo wa Yerusalem ama Ulaya?
3. Je, jeshi lenye askari milioni 200 litaundwa? Ufunuo 9:16.

**MAELEZO:** Nyakati za enzi ambapo kitabu cha Ufunuo kilipoandikwa, hakukuwa na idadi ya kutosha ya watu duniani kuweza kuwa na jeshi la askari milioni 200. Lakini bado Mungu alilibainisha uwezekano wa hili kadri ya miaka 2,000 kabla. Katika enzi zetu za siku hizi, itahitajika ushirikiano wa nchi za Asia ama

Eurasia kuweza kuunda jeshi la askari wengi namna hiyo—na eneo hili lenye idadi ya watu wengi zaidi kuliko pengine pote duniani ndilo linaloashiriwa na unabii wa kibiblia kuwa “wafalme wa mashariki” (ama, “wafalme toka mawio ya jua”). Kwa sababu ya eneo lake lililoko masharki ya mbali pamoja na uwepo wa idadi kubwa ya watu, jeshi lenye askari wafikiao milioni 200 linatarajiwa lihusishe China pia.

**MAELEZO: TUNAWEZAJE KUJUA KWAMBA ITAKUWA NI URUSI NA CHINA** ambazo zitadiriki kuja dhidi ya nchi ya Palestina ambako makao makuu ya Kristo ya ulimwengu ndiko yatakuwa?

Tambua kwamba neno “Gog” linamaanisha “ajaye tokea pande za kaskazini”—KASKAZINI mwa eneo la PALESTINA Ezekiel 38:15! Gog ndiye nani? Upo UFUNGOU wa kimsingi wa kutuwezesha kuelewa ni taifa lipi katika enzi zetu ndilo linaashiriwa pale linapotamkwa kwenye unabii wa Biblia. Tukielewa namna ya kuutumia ufunguo huo, TUNAWEZA KUJUA, MBELE YA TUKIO, KWA UHAKIKA NI MATAIFA YAPI YA LEO—Urusi, Ujeruman, Uturuki, Marekani, na mengine mengi—YATAKACHOKIFANYA KATIKA NYAKATI ZILIZO PUNDE TU MBELE YETU! Hili ni la muhimu sana kulijua katika siku hizi za mwisho. Ufunguo huu ni nini?

Ufunguo huo ni huu: MATAIFA YA ENZI ZA NYAKATI ZA BIBLIA NDIYO YAMEZAA MATAIFA YALIYOPO LEO. Hivyo Mungu katika nabii alitumia MAJINA YALEYALE YALIYOKUWEPO ENZI HIZO, ILI KUTABIRI KILE AMBACHO WAZAO WAO WATAKACHOKIFANYA KATIKA ENZI ZA ZAMA ZETU!

Wazao wa haya mataifa kwa sasa wamebadiri na kuchukua majina mengine katika nyakati za leo, LAKINI ni kipindi kifupi tu cha muda kimepita kati ya muda waliokuwa wakutumia majina yao ya kale na walipobadiri na kuchukua majina ya siku hizi, kiasi kwamba SI KAZI KUBWA WALA NGUMU, mara nyigi, kuchukua vitabu vya historia ya mataifa ya kale na kujionea ni jina jipi kila taifa—liliitwa katika BIBLIA!

Hivyo, kulijua JINA LA KI-BIBLIA la taifa la leo na kujua uhakika wa unabii wa Mungu—kulijua MATAIFA YATUZUNGUKAYO inawezekana. Sasa tutajionea kwa mfano utumiaji wa KANUNI HII KIUTEKELEZAJI. Hakutakuwa na kukisia. Mungu hakukusudia kwamba tukisie kuhusiana na unabii wake, sawa na wengi ya wanadamu wafanyavyo leo pale watafutapo kuufafanua!

Tambua kwamba ni ‘Gog na Magog’ (Ezekiel 38:2) ndio watakaokuja dhidi ya taifa ambako makao makuu ya Kristo anakusudia yawe (Aya ya 16). Tambua tena kwamba Gog na Magog wanakuja “KUTOKEA PANDE ZA KASKAZINI” (Aya ya 15)—ambako Urusi, Mongolia na China ndiko ziliko leo.

Je, inaweza kuonyeshwa kwa uthibitisho kwamba Urusi ndilo taifa litakalokuja kutokea pande za kaskazini kuja kuivamia nchi ya Palestina? “Kutokana na maelezo yapatikanayo kwa Waarabu, Waajemi na Waashuru”, tunajifunza kwamba mataifa haya matatu zamani yalitumia majina ya “Yajuj na Majuj” (jionee kufanana kwa matamshi katika majina ya ‘Majuj na Magog’) kuyataja “mataifa ya watu wakatili na wasiojulikana wa maeneo yote ya Kaskazini-magharibi na Kaskazini-mashariki mwa Asia”—AMBAKO URUSI NA UCHINA YA MONGOLIA ZILIKO LEO! (Imenokuriwa toka: McClintock and Strong, article “Magog”).

Jionee kwamba ‘Mesheki na Tubali (aya ya 2) nao wataungana nao katika uvamizi huu. Je, tunaweza kuthibitisha kwamba makabila haya ya kale pia kuwa ndiyo wazazi wa Warusi wa leo? Kumbuka, Urusi iliundwa kutokana na kuunganika kwa makabila kadhaa makubwa. Professor Sayce anaeleza kuhusu Meshech na Tubal: “Katika historia ya Waashuru majina haya yameandikwa kama ‘Tubla na Muska’, na walikuwa wakijulikana kuwa ni wataalamu wakubwa wa Jiografia, huku (Wagiriki) wao wakiwaita ‘Tiberani na Moskhi.’ Baada ya siku za Nebuchadnezzar, Wagiriki waliwakuta jamii hii ya makabila maeneo ya “Kaskazini zaidi ya pale walipokuwa wakiishi nyakati za enzi za Waashuru... walilazimika kuhamia kuelekeaa kaskazini karibu na Bahari Nyeus, .....” (Kutoka The Races of the Old Testament). Walihamia kuelekeaa KASKAZINI kwenda kwenye nchi tunayojua leo kuwa ni Urusi.

Baada ya kuwa WAMEVUKA HADI KWENYE MBUGA ZA URUSI watu hawa wa Meshech, walioitwa Moskhi na Wagiriki, wakaanza kujulikana kwa jina la Muskovs. Kutokana na jina hili “Muskov” jina la jiji lao la leo liitwalo MOSCOW LIMEPATIKANA. Wazao wa Tubal ndio waliobandika jina lao mto uitwao leo “Tobol River” pamoja na mji wa Tobolsk ulioko eneo la Urusi ya upande wa Asia. Hivyo tumethibitisha pasi na shaka kwa taarifa hizi kwamba mataifa yanayotajwa katika sura hii ya unabii wa Ezekiel yanalenga URUSI PAMOJA NA CHINA ZA LEO! Itakuwa ni Urusi na Uchina pamoja na washirika wake ndio watakaokuja dhidi ya Palestina baada ya Kristo kuwa ameanza kuisimika Israeli katika nchi hiyo iwe kama taifa lake la kimfano.

---

## Kristo Kuwa Mbadala wa Ibilisi Kama Mtawala wa Ulimwengu

Katika Waebrania 2:5 tunasoma kifuatacho: “Mungu hakuuweka ulimwengu ujao ambaa tunanena habari zake chini ya malaika”. Kwa maneno mengine, ufalme ambaa Kristo atausimika kwenye dunia hii hautatawaliwa na malaika walioasi, kama vile Shetani na mapepo wake. Hawa mapepo, pamoja na ibilisi ambaye ndiye kiongozi wao, wanautawala ulimwengu huu wa sasa na wanawapotosha wanadamu.

Kristo anakuja ili kuja kubadiri hali hiyo. Mwanadamu ameruhusiwa apitie na kujionea matokeo ya uovu wa kujitawala chini ya upotofu wa Shetani kwa miaka 6000. Wakati wa millenia inayokuja (utawala wa Kristo wa miaka 1000), ndipo kwa mara ya kwanza atajionea mwenyewe matokeo ya utawala wa Mungu mwenye uwezo hapa duniani.

1. Ni nani ambaye Kristo alikiri wazi kuwa ndiye MTAWALA WA SASA wa ulimwengu? Mathayo 4:8-9. SHETANI alimwonyesha Kristo tawala zote za ulimwengu, na akamwambia: “Nitakupa hivi vyote .....” Je, Kristo alikataa kwamba siyo vya Shetani wala hana uwezo wa kumpa?
2. Jionee katika Waefeso 2:2 kwamba Shetani anaitwa ni “mfalme.” Je, KRISTO AMESHINDA ILI AWE MFALME? Matendo 5:31. Je, Yohana alisema Kristo angekuwa mtawala dhidi ya nani? Ufunuo 1:5.

3. Je, Shetani anatambua wazi kwamba utawala wake juu ya dunia hii umekaribia kumalizika? Ufunuo 12:12. Ni lini ambapo SHETANI ATANG'OLEWA toka kwenye utawala wake na KRISTO kuchukua nafasi yake kama MTAWALA? Ufunuo 20:2-4. Je, hili si kwamba linafuatia mapema tu mara baada ya ushindi wa Kristo wa kwenye Bonde la Yehoshafati?
  4. Jina jingine la Shetani ni lipi? Waefeso 2:2. Je, amekuwa akiudanganya ulimwengu wote? Ufunuo 12:9. PALE SHETANI ATAkapofungiwa Kwenye SHIMO LISILO NA MWISHO, JE, BADO ATAKUWA NA UWEZO WAKE WA KUPOTOSHA DATU? Ufunuo 20:3.
  5. Ni WATAWALA WAKUU wa dunia wangapi ambaa watakuwepo baada ya Kristo kuwa ameusimika kiumara utawala wake? Zekaria 14:9.
  6. Je, MAPEPO—malaika waovu walio wafuasi wa Shetani, wenye miyo michafu—nao pia watawekwa KIFUNGONI? Zekaria 13:2.
- 

## MUHTASARI

KRISTO SHARTI AJE akiwa na UWEZO MKUU NA UTUKUFU. Ni LAZIMA ajiingize kwa nguvu za kiungu kwenye maswala ya ulimwengu huu! Hakuna kingine mbali na nguvu za kimungu kiwezacho kusitisha kasi ya wanadamu kujiangamiza wenyewe inayoikabili dunia hii! Wanadamu hawezikuiu!

Ni Mungu pekee ndiye mwenye UWEZO wa kumuondoa Shetani ambaye amewadanganya wakazi wa dunia hii kwa karne hizi zote, ambaye amewasababisha waziasi sheria za Mungu pasipo wao kujua, au amesababisha dhambi ionekane ni ya kuvutia sana kiasi kwamba wanadamu walitekwa nayo. Ni MUNGU peke yake ndiye atakayekuwa na uwezo wa kuwashinda madikiteta waovu—wa kidini na wa kiulimwengu—ambao sasa wanaibuka, na ambao, wakiwa wamevuvuwa na Shetani, wanabuni kuiweka dunia chini ya utawala WAO pasipo kujali gharama ya maisha ya watu yatakayoangamia. NI YEYE PEKEE NDIYE AWEZAYE KUIBADIRI ASILI YA MWANADAMU.

NI MUNGU PEKEE NDIYE MWENYE HEKIMA ya kuyatekeleza MAPIGO YA ADHABU KALI ambayo itakuja hivi karibuni. NI YEYE PEKEE ndiye mwenye hekima ya Kimungu. Yeye peke yake ndiye ajuaye ni nani ndiye anastahili kupita kwenye mapigo hayo. Ndiye atakayejua kwa usahihi pale uangamifu wa idadi kubwa ya wanadamu kwa gadhabu yake kama imetimia kwa kiwango na muda muafaka kiasi kwamba ni wale waliotubu pekeee toka mataifa yote ndio wasalie hapa duniani. Kupitia haya ATAANZISHA USTAARABU BORA ZAIDI chini ya MFUMO BORA WA SERKALI. Yote haya si MAONGEZI YA POROJO ZA KINDOTO tu yaliyobuniwa na “mhobiri” aliye pagawa. Wewe mwenyewe UMEMALIZA KUJISOMEA TAARIFA HIZI KUTOKA KWENYE BIBLIA yako mwenyewe! SASA UTACHUKUA HATUA GANI KUTOKANA NA HAYA?

Si jambo la kushangaza kwamba huu sasa siyo muda PEKEE wa wokovu. Mungu anawaambia watu wa taifa hili: “Wakati wangu

uliokubalika nitakujibu, nami katika siku ya wokovu nitakusaidia ... ili kurudisha nchi na kugawanya tena urithi waliokuwa ukiwa” (Isaya 49:8). DUNIA HIVI KARIBUNI ITABAKIA KARIBIA TUPU shauri ya dhambi za wanadamu zitakazosababisha Mungu amimine vitasa vya gadhabu juu yake. BAADA YA HAYA, UTARATIBU MPYA UTAANZISHWA. Ni baada ya haya kwamba NDIPO SASA ATAANZA KUWALETA WANADAMU CHINI YA UTAWALA WAKE NA KUWAOKOA!

## KWELI UPASWAZO KUZIJUA

### VITA KALI YA 3 YA ULIMWENGU INAKUJA!

Usitie shaka!—Vita ambayo hivi karibuni inakuja ambayo ni Vita ya 3 ya Dunia itakomesha vita vyote! Itaamua ni nani ndiye atautawala ulimwengu.

Vita ya Dunia ya 2 inachukuliwa ilipiganwa kwa kusudi hili, lakini haikuleta matokeo yaliyotoa uamuzi wa mwisho. Mataifa kwa sasa yanazo nguvu na uwezo—kuweza kuangamiza kabisa uhai wote utoke katika sayari dunia kuititia mabomu kama ya nyukilia, Hydrogen na zana zingine!

Vita ya 1 ya Dunia ya mwaka 1914 pamoja na Vita ya 2 ya Dunia—ambayo ilisababisha vifo Mara nne zaidi kuliko ile ya kwanza—zilikuwa ni manyunu tu ya mvua! Zilikuwa ni utangulizi peke yake wa UHARIBIFU NA MAANGAMIZI MAKUBWA ambavyo vitatokea ghafla hivi karibuni kwenye mataifa! Wanaopambania utawala wa ulimwengu hawawezi kuacha tamaa zao. Hiyo ndiyo sababu Mungu anasema: “CHUNGA!” (Luka 21:36).

Hili ni agizo toka kwa Mungu. Ebu basi na tujifunze taarifa juu ya wapambanaji hawa wenye tamaa ambao ama wataitawala dunia hii au kuiharibu. Uhai wako wenyewe utategemea uelewa wako mzuri juu ya hatari kubwa ambayo makundi ya mataifa yanavyojiandaa kutimiza kusudi lao. Unahitaji kuwa na jitihada katika kujifunza njia ya Mungu ya KUKUEPUSHA iliyofichuliwa kuititia masomo yajayo ya Kozi ya Kujifunza Biblia.

Hapa tunakupa dondo za kustaajabisha pamoja na maoni yanayokufunulia azima kali pamoja na werevu wa kiwango cha juu ambavyo kila mmoja wa hawa wadanganyaji wakuu amebuni kutekeleza ili kufikia lengo lake—kuitawala dunia—hadhi ambayo kimsingi na peke yake inamstahili Kristo!

### Ujerumani Karibia ITAUSTAAJABISHA Ulimwengu Tena!

Tangia kichwa cha habari hapo juu kilipoandikwa hapo awali, Ujerumani imeushangaza ulimwengu kwa kuinuka haraka kutoka kwenye maangamizi na uharibifu ilioupata kwenye Vita ya 2 ya Dunia na sasa imefikia kuwa ni uchumi mkubwa na muhimu ikiwa ni nchi yenye uwezo mkuu wa kiteknolojia kwa mara nyininge.

Kwa miaka mingi kupitia karne mbalimbali, Waashuru/Wasyria ambaa ndio mababu wa Ujerumani ya leo, walikuwa wakijiita “Herenvolk”—yaani “KABILA BORA.” Hadi leo bado wangali wakijiita hivyo. Je, Ujerumani ya leo imetupilia mbali azima yake ya kuifikia ndoto hii?

Kilichomo ndani ya fikra za Kijerumani kiliwekwa wazi mnamo mwaka 1950. Wakati huo, kulingana na kitabu cha T.H. Teten kiitwacho: Germany Plots with the Kremlin (yaani "Mipango ya siri ya Ujerumani pamoja na Kremlin"), Dr. Adenauer, kiongozi wa Ujerumani kipindi hicho, alisababisha wasiwasi mkuu kwa kuwaongoza mkusanyiko wa raia wa Ujerumani waimbe: "Deutschland Uber Alles"— yaani "UJERUMANI JUU YA WENGINE WOTE"—wakiwa mbele ya wawakilishi wa mataifa mengine makubwa ya dunia kipindi hicho. Kwanini wazo hili lilijitokeza ndani ya moyo wake?

## Hapa Tunakupa Dodoso Kadhaa Kuhusu MWELEKEO WA SASA WA UJERUMANI

"Hakuna, kushindwa siyo mwisho. Kushindwa kiujumla ni masomo tu ya kujifunza kwa ajili ya shambulizi lifuatelo ambalo ni kubwa," alisema Jenerari wa Ujerumani, Von Stuelpnagel mwaka 1944. Zaidi ya hayo, pia alisema, 'Katika VITA VYA DUNIA VITAKAVYOFUATA ...makosa yaleyle hayapaswi kurudiwa. ADUI WETU MKUU ATAKUWA NI MAREKANI, na jitihada zetu zote sharti tuzielekeze dhidi ya nchi hii tangia mwanzo... kushindwa kwetu katika vita ya sasa hakutakiwi kufikiriwa isipokuwa kama tukio tu Katika mwendelezo wa Ujerumani kusonga mbele kuelekea KUITEKA DUNIA"—Deutschland Uber Alles!

Kwa mara mbili zote tayari Ujerumani imesaribu kuuteka utawala wa dunia. Na mara mbili zote hizi, ni Uingereza, USA pamoja na washirika wao ndio wameizua isifanikiwe kutimiza azima yake. Safari hii itahakikisha kwamba USA haipo kabisa!

Adolf Hitler alituelezea juu ya hatua inayofuata katika mpango wa kijeshi uliobuniwa kwa uangalifu mkubwa wa kuitawala dunia alipokuwa akihitubia kupitia Mein Kampf. Alieleza kwamba Ujerumani sharti KWANZA IZISHINDE NCHI ZA MAGHARIBI ili iweze kuwa na mkono huru kwa ajili ya "Drang Nacha Osten"—gwaride la kuelekea Mashariki—kuiendea Urusi! Ni kwa usahihi kiasi gani haya yanaenda sambamba na unabii uliopo! Hitler alikuwa akiifuata mpango huuhuu wakati wa Vita ya Pili ya Dunia hadi pale Urusi ilipositisha kumpa mafuta yaliyokuwa yakimsaidia kuendeleza jitihada zake za kivita na ndipo akalazimika kumgeukia akijaribu kuuteka Urusi ili ajipatie mafuta yake.

Ujerumani imekusudia kuuteka ulimwengu. Na jinsi ilivyo muhimu KWA AJILI YA USALAMA WAKO kwamba uwe umeelewa swala hili vema, ebu na tuangalie zaidi uthibitisho mwingine. Ebu na tuangalie mipango ya ajabu ambayo ndiyo Ujerumani imeibuni ili iweze kutimiza lengo lake la kuutawala ulimwengu.

Miongo mingi iliopita wataalamu wa viwanda wa Ujerumani walianshisha chama ambacho waliamua kukiita PAN GERMAN LEAGUE. Wimbo wao ulikuwa ni "Deutschland über alles!"—Ujerumani Juu ya Wote. Walitumia alama ya kibiashara: "Made in Germany" kama uthibitisho wa ubora wa Ujerumani. Nyuma ya mbinu zao za kiuchumi na kibiashara kulikuwa na MKAKATI MKUU na wa KUDUMU—wenye LENGO LA KUITEKA DUNIA!

Ilikuwa ni wao ndio waliomshawishi kwa kiasi kikubwa Kaiser kuingia kwenye VitaKuu ya 1 ya Dunia. Ilikuwa pia ni wao ndio waliokuwa nyuma ya Vita Kuu ya 2 ya Dunia. Wakishilikiana

na Wataalamu wa Kijeshi wa Ujerumani pamoja na CHAMA CHA MIPANGO YA SIRI kilichoanzishwa na Jenerali Ludendorff, ambaye ndiye alimteua Adolf Hitler awe rais, ndio hawahawa wanaviwanda amba waligharamia mpango wa Chama cha Ki-Nazi, na kwa ujumla ndio waliomuinua Hitler na mamlaka yake. (Taarifa ya Seneta Kilgore's kwa kamati ya Maswala ya Kijeshi ya Marekani inatakiwa kuzingatiwa hapa). BAADHI WANAMINI KWAMBA HITLER ALITUMIKA KAMA CHOMBO TU. Alikuwa ni kama filimbi waliohitaji katika kuwapigia na kuwakusanya umati wa watu wa Ujerumani waungane nao katika mpango wao wa kiwendawazimu wa kuitawala dunia.

Ulimwengu ulimsikia na kumuona Hitler. Lakini wengi wa waliokuwa nyuma yake na waliobuni falsafa zake walibaki wamejificha wasijulikane, ili endapo Hitler hatafaulu wakati wa hiyo hatua ya pili ya Vita Vya Dunia, walikuwa wameazimia yeye ndiye aibebe lawama mbele ya ulimqwengu, na wao wabakie HURU KUENDELEA TENA KUBUNI KWA SIRI AWAMU YA TATU—VITA vya 3 vya DUNIA! Hivi vita ambavyo vinakuja! Pamoja na kwamba viongozi hawa kwa sasa wamekuwa, wafuasi wao mbalimbali na watoto wao wapo na wameachiwa jukumu la kulitekeleza lengo hilo.

Ilikuwa ni hawa wakuu wa viwanda amba walikutana kuchukua hatua mnamo katikati ya mwezi Mei, 1943. Walielewa vema kwamba tayari Hitler alikuwa amepoteza vita. Walibaini kwamba muda ulikuwa umewadia wa wao kwa mara ingine KUZAMA MAFICHONI—kumwachia lawama zote za Vita ya 2 ya Dunia aibebe yeye Hitler sawa kabisa na walivyokuwa wamefanya kwa kumfanya Kaiser aonekane ndiye wa kulaumiwa kwa Vita—ya 1 ya—Dunia.

Kuanzia wakati huo hadi sasa, wanaviwanda wa Ujerumani wameishi maisha ya kofia mbili. Kwa ulimwengu kwa ujumla, wameonekana kama wafanya biashara wakubwa na mashuhuri tu. LAKINI KISIRI WANAYO MIPANGO MINGINE MIKUBWA! Wajibu wao mkubwa ni kuhakikisha wanavifanya viwanda vya Ujerumani viwe tayari kuzalisha silaha, mabomu na risasi, pamoja na teknolojia sahihi kwa ajili ya vita ya tatu. Jukumu lao ni kutoa fedha za kuiwezesha hatua hii ya tatu, ambayo wao wanaiita kwa jina wajuo wenyewe, itimize lengo hili kuu mara wakati utakapokuwa tayari.

Hapa kuna maoni ya jinsi MWANAVIWANDA MKUU mmoja kwa MFANO, ambavyo amekuwa akitekeleza sehemu ya jukumu lake katika mpango huu. Ni Milionaire tajiri mkuu na mmiliki wa viwanda vingi sehemu nyingi, aitwaye Fritz Thyssen. Hili lilitifunuliwa kupitia kitabu, "The Nazis Go Underground"—yaani "Wana-NAZI Wajichimbia chini", kilichoandikwa na Curt Riess. Wakati wa mwanzo (jione ujanja na werevu mkuu walionao) wa Vita ya 2 ya Dunia, Thyssen alikimbizwa haraka kwenye nchi ya Switzerland ambayo haikuwa na upande wowowte kwenye hiyo vita, ambako huko alitangaza wazi kuwa Hitler alimdaganya akifadhili chama cha Nazi, na mara alipopanda kwenye madaraka, Hitler amemkana na kumgeuka akitaifisha utajiri wake, huko akimwacha maskini. Wana-Nazi wakajifanya wanamfukuza Thyssen toka kwenye chama chao. Thyssen akaandika kitabu juu ya "maovu" aliyyotendewa na watu hawa. Lakini baadaye pale Nazi walipoivamia Ufaransa, ambako ndiko Thyssen alikokuwa,

Wana-Nazi ambao ilitegemewa wangemchukia, walimuacha huru wala bila ya madhara yoyote na mda mfupi baada ya hapo alirudi zake Berlin ambako ndiko makao ya Nazi yalikokuwa, akiishi kwa ufahari na utajiri mkubwa. KELELE zote alizopiga ilikuwa ni kuwadanganya mataifa ya washirika ili waweke imani yao kwa Thyssen ili endapo majeshi ya hawa washirika yakishinda aweze kuiwezesha Ujerumani kifedha kwa ajili ya Vita Kuu ya 3.

Leo, shukrani kwa mpango huu uliobuniwa kwa kiwango cha juu pamoja na mingine ya aina hii, Krupp pamoja na wafanyabiasha wengine wengi mashuhuri wa Kijerumanini wamo katika harakati za kubuni na kuanzisha viwanda vikubwa ulimwenguni kote ili waweze kujipatia fedha za kuendeshea Vita Kuu ya Dunia ya 3. Mipango ya Nazi imebuniwa kwa weredi mkuu. (Cha kushangaza, baada ya dakika tano za kuipitia makala hii hapo juu, katika mwaka 2014, ambayo iliandikwa miaka ya 1950, Mimi, Bob Thiel, nilipanda ndege ili kusafairi (jet airliner) na nikabaini kwenye ngazi zake kubwa za automatiki zikiwa zinajina liitwalo "ThyssenKrupp"! — mamlaka ya kiviwanda ambayo imeendelea kuwepo hadi leo).

**WENGI WA WANA NAZI WALIJICHIMBIA MAFICHONI, MEI 16, 1943!**—miaka miwili hata kabla vita havijamalizika! Majemedari wa Kijerumanini, wanasayansi, wanaviwanda, watu wa mabenki, na wengine mashuhuri tayari walishatambua mapema kwamba Vita Vikuu vya 2 vya Dunia walikuwa wameshindwa. Hivyo wakati huo walijiandaa kwa ajili ya baadaye. Serkali ya kisiri kuliko zote katika historia ya nyakati zetu ikaanza kufanya kazi—KICHINICHINI! Katika mwaka 1951 Dr. Adenauer alikiri kuwepo kwa Wana-Nazi wa awali wapatao 134, ambao walikuwa wamefanyakazi bega kwa bega na Hitler, wakiwa katika nyazifa za juu za serkali yake huko Bonn Ujerumanini.

Ni vipi kuhusu nyakati zetu hizi? Ujerumanini ndio nchi yenyeye uchumi bora na mkubwa kuliko zote katika Ulaya. Inajulikana kote kwamba Ujerumanini ndio inayoiendesha Jumuia ya Uchumi ya Ulaya (EU)/European Union katika maswala mengi. Zaidi, hata leo watu wa Ulaya mbalimbali **WANAJITAHIDI KWA BIDII** kuunda silaha za kisasa kabisa pamoja na miradi mingine. Kuanzia mradi wa "Large Hadron" na "F.A.I.R." hadi kwenye mpango wa kuunda aina ya satellite ya kisasa zaidi iitwayo Galileo "GPS" system na hata aina ya silaha za kutumia mionzi (Laser weaponry-ELI) pia na miradi ya anga za juu iitwayo "European Space Agency", Umoja wa Uchumi wa Ulaya (EU) unaotawaliwa na Ujerumanini umechukua mwelekeo wa kijeshi zaidi.

Siku hizi utasikia zaidi juu ya European Union (EU), ambayo ni chanzo cha kuweza kuleta Serkali moja ya Ulaya (UNITED STATES OF EUROPE). Hili linaendana namna gani na mipango ya Ujerumanini ya kuuteka ulimwengu?

Dr. Adenauer alibainisha katika hotuba yake kwamba Ujerumanini ilikuwa ikichukulia kuundwa kwa Jumuia ya Uchumi ya Ulaya (EU) kama hatua ya kwanza katika kufikia kusimikwa kwa Mamlaka Kuu ya Tatu (Third Power bloc). Mnemo 1950 Dr. Adenauer aliandika, "Ulaya iliyounganishwa kama nchi moja itakuwa ni Mamlaka ya Tatu katika Ulimwengu". Baadaye alisema, "Hakuna yejote atakayenufaika kutohana na kuungana kwa Ulaya zaidi ya Wajerumanini ambao wao ndio wengi zaidi na walio na mipango

mingi zaidi mionganini mwa mataifa ya Ulaya yaliyoko nmagharibi mwa Urusi (U.S.S. R. {Russia}"). Dr. Adenauer hapa alikuwa akionyesha kwamba UJERUMANI inatamani kuwe na serkali ya Umoja wa Ulaya (United States of Europe) na akafichua kwamba yenyewe ndio ITAKAYOONGOZA pindi ikianzishwa—katika nyakati za karne ya 21, tayari tunajionea kuibuka kwa mamlaka hii inayosimamiwa na Ujerumanini.

Tunatambua ni nini ambacho Ujerumanini inakusudia. Tunajua jinsi Serkali ya Umoja wa Ulaya (United States of Europe) Itakavyotumiwa na nchi hiyo kujaribu kufikia kuutawala ulimwengu. UNABII unaonyesha wafalme 10—MADIKTETA KUMI—wataibuka katika Ulaya na kuamua kutoa madaraka ya utawala wa nchi zao kwa UJERUMANI.

Unaweza kuwa unajisemea moyoni mwako: "Kwa kuwa mengi ya yaliyotajwa hapo juu yaliandikwa miaka ya 1950, haiwezi kuwa na ukweli kwa Ujerumanini katika nyakati za karne ya 21. Wengi kwa sasa wanaamini kwamba Ujerumanini imekuwa ni mshirika wa kutumainiwa wa maswala ya amani ya dunia kwa miongo kadhaa na hivyo haiwezi kudiriki kuitawala dunia tena. Unaweza kuiamini dhana hiyo, na hata Wajerumanini wengi pamoja na watu wengine wa Ulaya wanaamini hivyo, lakini fahamu utakuwa umekosea!

Ebu ona unabii ufuatao:

"5 Ole wa Waashuru, fimbo ya hasira yangu, ambaye mkononi mwake iko rungu ya

ghadhabu yangu! 6Ninamtuma dhidi ya taifa lisilomjua Mungu, ninamtuma dhidi ya taifa linalonikasirisha, kukamata mateka na kunyaaua nyara, pia kuwakanyaga chini kama matope ya barabarani. 7Lakin hili silo analokusudia, hili silo alilonalo akilini,

kusudi lake ni kuangamiza, kuyakomesha mataifa mengi. 8Maana asema, 'Je, wafalme wote si majemadari wangu? (Isaya 10:6-8).

Isaya anazungumzia muda ambao mamlaka ya Kiashuru ya kipindi cha mwisho itatumwa dhidi ya taifa "nafiki", lisilosika maneno ya Mungu. Neno la Kigiriki lililotumiwa kutaja taifa lililo nafiki linaashiria kuwa "lililochafuka, lililoasi", na hii ndio hali halisi kwa mataifa ya asili ya Kiisraeli hususani Marekani (USA). Kuibuka kwa siri zilizofichuliwa na Snowden juu ya Marekani kuzipeleleza nchi zingine imeiongezea hasira Ujerumanini.

Si kwamba tu wanaona Marekani imekuwa wanafiki kwao, lakini pia walikasirishwa sana walipotambua kwamba kulingana na taarifa zilizovuja juu ya Taasisi ya Ujasusi ya Marekani (NSA), Ujerumanini ilikuwa ni moja ya nchi zilizopeleleza zaidi na Marekani. Taarifa nyingine ya NSA ilisema kwamba nchi pekee ambazo Marekani inazichukulia kama "marafiki wa karibu" (washirika wa kuaminiwa) ambao hawahitajiwi kupeleleza sana walikuwa ni nchi za Uingereza, Canada, Australia, na New Zealand—mataifa yenyeye asili ya Ki-anglo-Saxon-Kiceltic. Ujerumanini na wengine wamelibaini hili na watachukua hatua dhidi ya hao wajitao "marafiki wa karibu" hapo baadaye (Jione katika Danieli 11:39; Zaburi 83:3-8).

Lakini zingatia aya ya 7 ya Isaya 10. Inasema kwamba hii mamlaka ya "Kiashuru" haifikirii wala kudhamiria kwa sasa kuwa itaangamiza wengi katika nyakati za mwisho. Lakini, wazo hilo liko katika fikra zake, na historia yake, na mtazamo wake juu ya ulimwengu utaifanya ifanye hivyo.

#### KWANINI?

Kwa sababu sawa na aya ya 8 inavyoashiria, taifa hili linajichukulia kuwa lenyewe ni kabilia bora.

### Vatican Itajiingiza Katika Maswala

Je, Ujerumani inayo mipango ya kupewa usaidizi toka kwa "Kanisa Kuu" ili limsaidie kufikia kuumiliki ulimwengu? Taarifa ijulikanayo kama "Madrid Circular Letter", ambayo inaelezea juu ya mawazo ya wale walio katika utawala wa Ujerumani, inasema: "Watu wa Ujerumani, walioelimishwa vema na kuimariswa chini ya mtazamo wa uongozi wa umoja wa kitaifa (national socialist leadership), wanatawaliwa na aina mbili za mitazamo mikuu: Mtazamo wa Ubora wa Kabilia la Kijerumani, na lengo la Ujerumani la uongozi wa ulimwengu . . . jadi ya kidini iliyomo katika wazo la ubora wao kuliko wengine, ndilo linatoa msukumo wa kisiasa na ndilo linalopendelewa zaidi ndani ya ulimwengu wa Kikatholiki".

**DHANA YA KIJERUMANI YA KUFAULU KUUTAWALA ULIMWENGU INAUFURAHISHA ULIMWENGU WA KIKATHOLIKI KWA KIASI KIKUBWA!** Sasa ebu na tuelewe ni kwanini hili liko hivyo. Litaathiri maisha yetu—uhai wako—zaidi sana kuliko labda unavyodhania!

Mnamo Februari 10, 1952 wakati wa hotuba yake PAPA ALIONYA: "ULIMWENGU WOTE SHARTI UJENGWE UPYA kutoka kwenye misingi yake". Kwa siri Wawakilishi wa Vatican wamekuwa wakijenga misingi ya MPANGO ambao UTAUBADIRI USTAARABU WA NCHI ZA MAGHARIBI! Ilibidi IBUNIWE KWA SIRI ili isibainike hadi ifikie muda ambao wote wamechelewa kuuzuia! Vatican inadai kwamba amani ya dunia inaweza kupatikana tu pale kutakapokuwepo na chombo cha kimataifa KILICHOCHINI YA UKATHOLIKI kilicho na MENO YA CHUMA YA KUWEZA KUUVUNJA UPINZANI WOWOTE.

"Chombo hiki/Taasisi hii", alisema Papa Pius wakati wa hotuba yake ya sikukuu ya Christmas ya mwaka 1944, "kitakuwa na uwezo . . . na mamlaka makuu na NGUVU YA KUPONDAPONDA. . . CHOKOCHOKO". Elewa chombo hiki ambacho Papa inakiwazia kiwe na uwezo, kitakuwa na nguvu za kijeshi za kiasi kikubwa kuweza kuzima upinzani wa aina yoyote kwa hata kanisa. Chombo hiki kinachokuja kitakachotawaka ulimwengu wote kitakuwa hivyo basi ni MUUNGANIKO WA KANISA NA SERKALI ambapo Papa, ambaye nabii zote, za Kibiblia na zile za Kikatholiki zinamuashiria kwamba ye ye ndiye atakuwa namna ya papa wa kipinzani na hatimaye kuwa ndiye Mpinga-Kristo wa mwisho, analisukuma mbele hili (Ufunuo 13:11-18). Vatican haiwezi kulibuni swala hili moja kwa moja na Warusi, na Wamarekani hawana msukumo wowote wa tangu asili wa kutamani kuutawala ulimwengu kwa namna hiyo. Lakini Wajerumani mbalimbali pamoja na baadhi ya mataifa mengine ya Ulaya ni muafaka kwa malengo haya ya Papa. Ujerumani inahitaji nguvu-kazi ya mamilioni ya wanadamu ambao Vatican inaweza kuwatupa kwake ili kuusaidia uongozi

wake wa Kanisa batili na potofu la kipindi cha mwisho; uwezo wa jeshi la Ujerumani lenye makali ndio unaoweza kulifanikisha hili! Mambo haya pia yanakubaliana na unabii kwa kiwango kikubwa: Katika Somo la 3, Kipengele 'Kukusanyikia Harmagedoni', soma swali la 2. Na sehemu isemayo: 'Matokeo ya Ushindi wa Kristo', soma swali la 4 na 5. NYAKATI ZINAPITA KWA HARAKA!

Vatican, sawa na "nabii binafsi za Kikatholiki" mbalimbali inaamini kwamba Ulaya itainuka kwa mara nyingine kwa ajili ya kuifufua tena kwa mara ya mwisho, ile ambayo imekuwa ikiitwa "Milki Takatifu ya Rumi".

Jambo moja zaidi linatakiwa kuangaliwa. Je, UJERUMANI ITAENDELEA KUWA KARIBU NA URUSI hadi ifikie kuweza kuziteketeza nchi za Ulaya (magharibi)? Jibu ni "NDIYO". Katika angalau safari sita ama saba ndani ya miaka kama mia mbili na hamsini iliyopita, ambapo Ujerumani imepigana na nchi za Magharibi, ilianza kwanza kufunga mkataba na Urusi ili ijihakikishie usalama kutokea upande wake wa Mashariki. Hata safari hii haitakuwa tofauti.

Matukio ambayo yametajwa hapa ni ya uhakika na yataokea. Muungano wa kustaajabisha baina ya Jumuia ya Ulaya ikiongozwa na Ujerumani wakiungana na kanisa kuu utatokea! YASOME Magazeti yako ya taarifa za habari—Sikiliza Redio na Television nyakati za taarifa za habari. Soma makala za magazeti yanayotoa habari za kimataifa. Utajonea mambo yaliyolezewa hapa yakijitoneza na kuchukua sura taratibu, siku baada ya siku. Ulimwengu "utashangaa"—na kusimama kwa kuduwa—pale watakapouona muungano huu wa serkali na kanisa ukitokea (Ufunuo 17:8). Wewe hauhitaji kusimama katika mshangao. Kumbuka, Mungu anasema: "Kesheni (fuatilieni kwa tahadhari) na muombe ili muweze kustahiri kuepuka (kupenya na kutoroka)". Iko sababu kwa Mungu kutoa ahadi kwa watu wake kuwa wanatakiwa wapenye, watoroke.

Endelea kujisomea masomo haya kwa bidii yote. Utaongezeka katika neema na elimu ya neno la Mungu na unaweza kupata ulinzi wa Mungu katika kupenya na kuyatoroka mapigano ya Vita vya 3 vya Dunia vikali. Lakini pia unapaswa uweke umakini katika kufuatilia matukio ya ulimwengu ili ukutwe uko tayari!

### Muhimu!

YAWEKE MASOMO HAYA MUHIMU KWENYE JARIDA (FILE),

Hasa Karatasi za kurasa zifuatazo baada ya SOMO la 3. JISOMEE haya mara kwa mara. Ni muhimu mno kuuweka ukweli huu ndani ya kumbukumbu yako. "Fuatilia kwa makini!"

# Je, WAKRISTO WA LEO WANAPASWA KUISHIKA SIKUU YA BARAGUMU?



Na Bob Thiel

Je, Wakristo wanapaswa kuishika Sikuu ya Kuzipiga Baragumu, ijulikanayo kwa Wayahudi kama "Rosh Hashanah"? Je, unaelewa ni lini inapaswa kufanyika? Ni mambo yapi ambayo Wakristo wa leo wanawea kujifunza kwa kuishika?

Sikuu ya Baragumu (Rosh Hoshana) hutimia kwenye jioni ya tarehe ya kwanza ya mwezi Tishri (mwezi ambao mara nyingi huanza katika mwezi Septemba kwenye kalenda ya Kirumi— itasherehekewa kuanzia machweo ya jua ya tarehe 24 ya mwezi Septemba hadi machweo ya Septemba 25 katika mwaka 2014; na itasherehekewa kwenye jioni ya Septemba 13 hadi jioni ya Septemba 14 katika mwaka 2015).

Waumini katika Kanisa la Mungu wameishika Sikuu hiyo kwa muda mrefu.

Kiongozi mmoja wa Kanisa la Mungu, Herbert W. Armstrong, alifundisha:

"23BWANA akamwambia Musa, 24"Waambie Waisraeli: 'Katika siku ya kwanza ya mwezi wa saba mtakuwa na siku ya mapumziko, KUSANYIKO TAKATIFU, ni ukumbusho wa kupigwa kwa tarumbeta. 25Msifanye kazi zenu zo zote za kawaida." (Walawi 23:23-25).

Hapa inatolewa kwetu kama kielelezo kwamba tukio lifuatalo katika mpango wa Mungu wa ukombozi lenye baraka, ambapo ndipo Kristo ATAKAPOREJEA tena katika mawingu, kukiwa na sauti kuu na sauti ya Malaika Mkuu, pamoja na parapanda/baragumu ya Mungu (I Wathesalonike 4:14-17). Itakuwa ni wakati wa: "parapanda ya mwisho itakapolia. Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu watafufuliwa wakiwa na miili isiyoharibika, nasi tutabdalishwa" (I Wakorinto 15:52).

Sharti Kristo arejee kuja kuwafufua wafu, vinginevyo hatutaweza kuupata uzima wa milele, iwapo hakuna kufufuliwa: "18Hivyo basi wote waliolala katika Krito wamepotea (wameangamia)" (I Wakorintho 15:18).

Kristo atajiingiza moja kwa moja kwenye maswala ya ulimwengu kuanzia wakati baragumu/parapanda ya saba itakapopulizwa (Ufunuo 11:15-19). Baragumu ni kielelezo cha vita. Atarejea katika wakati ambao kutakuwa na vita ya ulimwengu mzima pale mataifa yatakapokuwa yamekasirika! Mara tu pale kazi ya kuwakusanya malimbuko (inaainishwa na Pentekoste) itakapokamilika katika kizazi hiki, ndipo Kristo atakapoanza kuisimamisha tena madhabahu ya Daudi (Matendo 15:16), ili apeleke mkono wake tena mara ya pili kujipatia mabaki ya watu wake waliosalia (Isaya 11:11), kuwatafuta na kuwapata kondoo wake waliopotea ambao wahubiri wa makanisa wameshindwa kuwatafuta na kuwaponya katika nyakati zetu hizi (Ezekieli 34:1-14).

Gundua hasa ni lini haya yanatimia: "13Katika siku ile tarumbeta kubwa italia. Wale (Israeli) waliokuwa wakiangamia ....watakuja na kumwabudu BWANA katika mlima mtakatifu huko Yerusalem". (Isaya 27:13).

Ni lini Israeli watakusanya? Ni wakati wa kupulizwa kwa baragumu/parapanda, wakati wa kuja kwa Kristo Mara ya Pili. Kwa sababu makanisa yameitupilia mbalai na kuisahau Sikuu ya Baragumu, wengi wanadhani kwamba kurejea kwa baadhi ya Wayahudi wachache kwenye Nchi Takatifu pamoja na kuundwa kwa taifa la Israeli miongo kadhaa iliyopita ndiko kulikuwa kutimizwa kwa unabii huo!

Kujiingiza kwa Kristo kwenye maswala ya ulimwengu kutakuwa ndilo tukio litakalofuata katika mpango wake wa ukombozi. (Na: Armstrong HW. Kutoka makala iitwayo: "Pagan Holidays- or God's Holy Days-Which?").

Sikuu ya Baragumu kwa hakika inaelekeza kwenye upulizwaji wa parapanda na Biblia inaonyesha matukio ya aina kadhaa yataambatana na kupigwa kwa parapanada mbalimbali.

## Agano la Kale

Maandiko ya Kiebrania yanaeleza:

2"Sikuu zilizoamuriwa za BWANA, ambazo mtazitangaza kuwa makusanyiko matakatifu, hizi ni Sikuu zangu..... 24 'Katika siku ya kwanza ya mwezi wa saba mtakuwa na mapumziko ya sabato, ukumbusho wa kupigwa kwa tarumbeta, ni kusanyiko takatifu (Walawi 23:2,24).

1 Katika siku ya kwanza ya mwezi wa saba mtakuwa na kusanyiko takatifu na msifanye kazi ya kawaida. Ni siku kwa ajili yenu ya kupiga tarumbeta. 2Mtatayarisha sadaka ya kuteketezwa kama harufu nzuri impendezayo BWANA ya fahali mmoja mchanga, kondoo mume mmoja na wana-kondoo saba wa mwaka mmoja, wote wasiwe na dosari. 3Pamoja na fahali andaeni sadaka ya nafaka sehemu ya kumi tatu za efa za unga laini uliochanganywa na mafuta, kondoo mume, unga sehemu ya kumi mbili za efa, 4pamoja

na wana-kondoo saba kila mmoja aandaliwe na sehemu ya kumi moja ya efa ya unga. 5Ongeza beberu mmoja kama sadaka ya dhambi kufanya upatanisho kwa ajili yenu. 6Hivi ni nyongeza ya sadaka za kuteketezwa ya kila mwezi na kila siku pamoja na sadaka za nafaka na sadaka za vinywaji kama ilivyoainishwa. Ni sadaka zinazotolewa kwa BWANA kwa moto, harufu inayopendeza. (Hesabu 29:1-6).

4Kisha kulingana na kile kilichoandikwa, wakaiadhimisha Sikuu ya Vibanda wakitoa idadi ya sadaka za kuteketezwa kama ilivyohitajika kila siku kama ilivyoagizwa. 5Baada ya hayo, walitoa sadaka za kuteketezwa za kawaida, sadaka za Mwandamo wa Mwezi na dhabihu zote za sikukuu takatifu za BWANA zilizoamuriwa, pamoja na zile sadaka za hiari zilizotolewa kwa BWANA. 6Ingawa bado msingi wa hekalu la BWANA ulikuwa haujawekwa, watu walianza kutoa sadaka za kuteketezwa kwa BWANA kwa moto tangu siku ya kwanza ya mwezi wa saba (Ezra 3:4-6).

(Tambua: Kwa vile sadaka za kuteketezwa za wanyama zilipita kwa kutimia katika Kristo kulingana na Waebreania 10:3-10, sisi Wakristo hatutoi aina hiyo ya sadaka—tunatakiwa tujitoe sisi wenye kama sadaka iliyo hai (Warumi 12:1). Hata hivyo, kama desturi ilivyo, siku hiyo tunatoa sadaka ya matoleo yetu ya shukrani sawa na alivyofundisha Mtume Paulo kupitia 2 Wakorinto 9:6-8, pamoja na Kumbukumbu la Torati 16:16; kama Ezra anavyoiunganisha siku ya kwanza ya mwezi wa saba pamoja na Sikukuu ya Vibanda inayofuatia).

Katika nyumba yetu, tumekuwa na jadi ya mtoto mdogo kuliko wote kwenye familia kupuliza tarumbeta kwenye mwanzo wa Sikukuu hii pamoja na muda wote unaofuata wa Sikukuu hii.

Mwezi wa saba huitwa "Tishri katika Kiebrania na Sikukuu ya Baragumu huitwa wakati mwagine katika maandiko ya historia za Kiyahudi kama "Tshiri Moja". Ijapokuwa kwa sasa Wayahudi wanaiita "Rosh Hashana", kiujumla hilo halikuwa ndilo jina lake la awali:

"Rosh Hashana, ambayo tafsiri yake ya neno kwa neno inamaanisha Kichwa cha Mwaka" {likuwa} "haikuitwa Rosh Hashanah hadi nyakati za Talmud" (Kramer, Amy J. Rosh Hashana Origins. Copyright © 1998-1999 Everything Jewish, Inc. [http://www.everythingjewish.com/RoshH/RH\\_origins.htm](http://www.everythingjewish.com/RoshH/RH_origins.htm) 9/16/04).

(Nyakati za kuanzishwa kwa Talmud (Kitabu cha Kiyahudi cha Historia ya dini yao) ilikuwa kati ya mwaka 70-500 B.K.). Kwa vile majina 'kichwa' na 'mwaka' hayamo katika maandiko ya Agano la Kale yanayoielezea Sikukuu hii, jina linalotumiwa na Kanisa la Mungu la kuitaja Sikukuu hii ndilo la Kibiblia tofauti na hili 'Rosh Hashanah' la Kiyahudi ambalo ni la hivi karibuni (ambalo haliifafanui Sikukuu kiuhalisa).

Haieleweki vema ni lini na ni kwa namna gani Wayahudi waliihusisha Sikukuu ya Baragumu na "Kitabu cha Uzima", swala ambalo walilifanya katika nyakati zilizopita.

Kutokana na kujisomea kwangu katika taarifa za Talmud, inaonekana kwamba kwa kuwa viongozi wengi wa Kiyahudi

waliyamin kwamba Mungu amefundisha kuwa uumbaji yaonekana kama ulifanyika katika majira ya Kipupwe (Autumn), kinyume na majira ya Vuli (Spring). Hii inaonekana kuwa imetokana na kuifafanua kwao aya ya Mwanzo 1:11. Katika aya hii, pale Mungu aliposema: "Ardhi na itoe mimea: miche itoayo mbegu, miti juu ya nchi itoayo matunda yenyé mbegu ndani yake, kila mmea kulingana na aina zake mbalimbali"; wao wakaona hii inawezekana ilikuwa ni kipindi cha kuelekea mwanzoni mwa majira ya Kipupwe, maana ni wakati wa majira haya ndipo huwa kuna nyasi za kijani na miti hutoa matunda katika eneo lao. Viongozi wa Wayahudi waliamini kwamba Sikukuu ya Baragumu iinaashiria mwanzo wa uumbaji, na hivyo inawakilisha uhai.

## Kitabu cha Uzima

Talmud yenye inatamka kwamba ukweli wa baragumu tatu tofauti zitakazopolizwa zilizolezewa katika Hesabu 10:1-10, zinawakilisha vitabu vitatu, kimojawapo kikiwa Kitabu cha Uzima.

Kiashilio cha kwanza cha ki-biblia cha Kitabu cha Uzima yaonekana kuwa ni katika Kutoka 32:32-34:

"32Lakini sasa, nakusihi wasamehe dhambi yao, lakini kama sivyo, basi nifute kutoka kwenye kitabu ulichoandika."

33BWANA akamjibu Musa, "Ye yote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta kutoka kwenye kitabu changu. 34Sasa nenda, uongoze hao watu mpaka mahali nilipokuambia, naye malaika wangu atakutangulia. Pamoja na hayo, wakati utakapofika wa mimi kuwaadhibu, nitawaadhibu kwa ajili ya dhambi yao".

Musa alikuwa anajua kwamba ye ye aliukwemo katika kile kitabu. Vile vile inaonekana kutokana na aya hizi juu kwamba Mungu anazungumzia vyote, kitabu cha uzima pamoja na siku ya hukumu.

Yaonekana kuwa kitabu kilekile kimetajwa tena katika Zaburi 69:27-28 ambako mawazo yote mawili yameongelewa:

27Walipize uovu juu ya uovu, usiwaache washiriki katika wokovu wako.

28Wafutwe kutoka kitabu cha uzima na wasiorodheshwe pamoja na wenye haki.

Zaidi tena, kitabu kilekile yawezekana kimetamkwa tena katika zaburi zingine tatu:

7Ndipo niliposema, "Mimi hapa, nimekuja, imeandikwa kuhusu mimi katika gombo la kitabu. 8Ee Mungu wangu, natamani kufanya mapenzi yako, sheria yako iko ndani ya moyo wangu" (Zaburi 40:7-8).

8Andika maombolezo yangu, orodhesha machozi yangu katika gombo lako, je, haya hayapo katika kumbukumbu zako? (Zaburi 56:8).

16Macho yako yaliniona kabla mwili wangu haujakamilika. Siku zangu zote ulizonipangia ziliandikwa katika kitabu chako kabla hajakuwapo hata moja (Zaburi 139:16).

Katika Malaki 3:16 inaelezwa:

16Ndipo wale waliomcha BWANA wakasemezana wao kwa wao, naye BWANA akasikiliza naye akasikia. Kitabu cha kumbukumbu kikaandikwa mbele yake kuhusu wale ambao walimcha BWANA na kulitafakari Jina lake.

Aya hizi zinaonyesha kwamba wale wanaomcha BWANA wameandikwa kwenye kitabu, lakini wale wasio wenyewe haki hawamo katika kitabu hicho.

Katika Isaya 27:13 imeandikwa:

13Katika siku ile tarumbeta kubwa itapulizwa; Wale waliokuwa karibu na kuangamia katika nchi ya Ashuru, nao wale waliokuwa uhamishoni katika nchi ya Misri watakuja na kumwabudu BWANA katika mlima mtakatifu huko Yerusalem.

Aya hizi yaonekana zinaashiria juu ya baragumu/parapanda ya mwisho, ambayo ndiyo itakayoashiria kurejea kwa Kristo na kusimikwa kwa Ufalme wa Mungu.

## Agano Jipy

Baadhi ya desturi za Kiyahudi kuhusu maana ya Sikukuu ya Baragumu zinapanana na kile ambacho Agano Jipy linaonekana kufundisha kuhusu Sikukuu hii.

Pamoja na kujadili juu ya Kitabu cha Uzima kwenye Siku hiyo, desturi za Kiyahudi zinasema kuhusu Rosh Hashana:

"Rosh Hashana...ndiyo Siku ya Hukumu...Ni Siku ya Kupulizwa Shofar (tarumbeta za asili za Wayahudi zilizotengenezwa kwa pembe za wanyama)..." (The Jewish Holiday of Rosh Hashanah. High Holy Days on the Net. <http://www.holidays.net/highholydays/rosh.htm> verified 9/12/07).

Agano Jipy mara nydingi limetaja kuhusu kupigwa kwa baragumu/parapanda.

Yesu Kristo alifundisha:

30"....Nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya angani, katika uwezo na utukufu mkuu. 31Naye atawatuma malaika zake kwa sauti kuu ya tarumbeta, nao watawakusanya wateule wake kutoka pande zote nne za dunia, kutoka mwisho mmoja wa mbingu hadi mwisho mwagine (Mathayo 24:30-31).

Hili linapatana na lile alilolifundisha Mtume Paulo:

16Kwa maana Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni, akitoa amri kwa sauti kuu pamoja na sauti ya malaika mkuu na sauti ya tarumbeta ya Mungu, nao wale walilola mauti wakiwa wanamwamini Kristo watafufuka kwanza. 17Baada ya hilo sisi tulio hai bado, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili kumlaki Bwana hewani (1 Wathesalonike 4:16-17).

Hivyo wote Yesu pamoja na Paulo walifundisha kwamba

watakatifu watakusanya pale baragumu fulani itakapopulizwa. Na kwamba kuja kwa Kristo kutaambatana na mlio wa baragumu.

Baragumu ipi? Ni parapanda ya mwisho:

51Sikilizeni, nawaambia siri: Sote hatatalala, lakini sote tutabadilishwa 52ghafla, kufumba na kufumbua, parapanda ya mwisho itakapolia. Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu watafufuliwa na miili isiyoharibika, nasi tutabadilishwa (1 Wakorintho 15:51-52).

Kwa kuwa hii inaongelea juu ya baragumu ya mwisho, basi maandiko ni yamkini hayaungi mkono dhana ya 'watakatifu/kanisa konyakuliwa' kabla ya kuanza kwa dhiki kuu, kinyume na madhehebu mengi yanavyoamini!

Pamoja na kwamba maandishi yake siyo sehemu ya Agano Jipy, Polycarp aliyejekuwa mfuasi wa Mtume Yohana alitazamia kutimilizwa kwa baragumu hii, sawa na alivyoandika:

Hivyo basi, ukijifunga mkanda wako kiunoni, "mtumikieni Bwana kwa kutetemeka" na ukweli, kama watu waliokuacha kuptokwa kwa wengi pamoja na mazungumzo yasiyo na faida, na "wanaomwamini yeze aliyemfufua Bwana Yesu Kristo kutoka kwa wafu, na kumpa utukufu", pamoja na kitu cha enzi katika mkono wake wa kuume. Kwake yeze vitu vyote mbinguni na duniani vimekishwa. Ni yeze kila roho humtumikia. Atakuja kama Hakimu wa walio hai na waliokufa. Damu yake Mungu ataidai kutoka kwa wale wasiomuamini Yeze. Lakini yeze ambaye alimfufua kutoka mautini, atatufufua na sisi pia, iwapo tutayafanya mapenzi yake, na kuenenda katika Amri zake, na kupenda yale aliyoypenda! (Polycarp. Waraka kwa Wafilipi, sura ya II. Ante-Nicene Fathers, Volume 1 as edited by Alexander Roberts & James Donaldson. American Edition, 1885).

Hii baragumu ya mwisho iliyotajwa katika 1 Wakorintho 15, ndiyo parapanda ya saba iliyotajwa katika Ufunuo 11:15:

15Yule malaika wa saba akaipiga tarumbeta yake, pakawa na sauti kubwa mbinguni iliyosema: "Ufalme wa ulimwengu umekuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala milele na milele!"

Hivyo, parapanda/baragumu, angalau kiunabii, ni lazima iwe muhimu sana kwa Wakristo!

## Kitabu cha Uzima katika Agano Jipy

Ni majina ya akina nani ndiyo yamo katika Kitabu cha Uzima?

Ya Wakristo pamoja na wengine mbalimbali wa kutokea enzi za Agano la Kale.

Yesu Kristo alifundisha:

18Yesu akawaambia, "Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme wa radi. 19Tazama nimewapa mamlaka ya kukanyaga nyoka na ng'e na juu ya nguvu zote za adui, wala hakuna kitu cho chote kitakachowadhuru kwa

namna yo yote. 20Basi msifurahi kwa kuwa pepo wachafu wanawatii, bali furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa mbinguni” (Luka 10:18-20).

Paulo aliandika:

3Naam, nawasihi ninyi pia, wenzi wangu waaminifu, wasaidieni hawa wanawake, kwa sababu walijitaabisha katika kazi ya Injili pamoja nami bega kwa bega, wakiwa pamoja na Klementi na watenda kazi wenzangu amba majina yao yameandikwa katika Kitabu cha Uzima (Wafilipi 4:3).

22Lakini ninyi mmeufikia Mlima wa Sayuni, Yerusalemu ya mbinguni, mji wa Mungu aliye hai. Mmefika penye kusanyiko kubwa la malaika maelfu kwa maelfu wasiohesabika wanaoshangilia, 23kwenye kanisa la wazaliwa wa kwanza wa Mungu, amba majina yao yameandikwa mbinguni. Mmekuja kwa Mungu, mhukumu wa watu wote, kwenye roho za wenyehaki waliokamilishwa (Waebrania 12:22-23).

Yohana aliandika:

5Yeye ashindaye atavikwa vazi jeupe kama wao, nami sitafuta jina lake kutoka katika Kitabu cha Uzima, bali nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu na mbele za malaika Wake (Ufunuo 3:5).

Hivyo, ni watakatifu ndio majina yao yameandikwa katika Kitabu cha Uzima. Na watakatifu ni wale amba watafufuliwa wakati wa parapanda ya mwisho.

Maeneo mengine katika Kitabu cha Ufunuo yanataja kwamba wale watakaomsujudu mnyama (Ufunuo 13:1, 8; 17:8), wale amba wanahuksika na machukizo (Ufunuo 21:27), pamoja na wale watakoayapunguza maneno ya Ufunuo (Ufunuo 22:19), HAWATAKUWEMO mionganoni mwa wale amba majina yao yameandikwa katika Kitabu cha Uzima.

## Kitabu cha Ufunuo Kinalezea Juu ya Baragumu Nyingi Zitakazopulizwa

Talmud inafundisha kwamba maeneo kadhaa ya Agano la Kale (Hesabu 10:1-10) yahusuyo kupulizwa kwa baragumu kutoa ishara pia yanauhusiano na Sikukuu ya Baragumu. Kwa kuwa kuna aina tatu tofauti za baragumu ambazo zimetajwa katika sehemu hiyo, wasomi wa Kiyahudi walionelea kwamba baragumu hizo tatu tofauti zinawakilisha vitabu vitatu tofauti ambavyo vitafunguliwa kwenye siku ya kwanza ya mwezi wa Tishri. Talmud pia inachukulia kwamba Sikukuu ya Baragumu inauhusiana na wakati wa hukumu.

Cha kushangaza, ni dhahiri kulingana na Kitabu cha Ufunuo wa Yohana kwamba baragumu saba zitapulizwa (Ufunuo 8:2), Adhabu itakuja kwa wale amba hawako chini ya ulinzi wa Mungu (Ufunuo 9:4), na kisha ndipo hukumu itafuata (Ufunuo 11:18).

Hapa jionee taarifa juu ya baragumu sita za kwanza (italiki zilizoonyeshwa hapo chini ni maelezo ambayo hayamo katika Biblia, bali yalionegezwa na wachambuzi wa Kitabu cha Ufunuo):

8:1Mwana-Kondoo alipoivunja ile lakiri (muhuri) ya saba,

pakawa kimya mbinguni kwa muda wa nusu saa. 2Nami nikawaona wale malaika saba wanaosimama mbele za Mungu, nao wakapewa tarumbeta saba. 3Malaika mwingine aliyekuwa na chetezo cha dhahabu, akaja na kusimama mbele ya madhababu. Akapewa uvumba mwingi ili autoe pamoja na maombi ya Watakatifu wote, juu ya ile madhababu ya dhahabu iliyoko mbele ya kile kiti cha enzi. 4Ule moshi wa uvumba pamoja na yale maombi ya watakatifu, vikapanda juu mbele za Mungu, kutoka mkononi mwa huyo malaika. 5Kisha yule malaika akachukua kile chetezo, akakijaza moto kutoka kwenye ile madhababu, akautupa juu ya dunia. Pakatokea sauti za radi, ngurumo, umeme wa radi na tetemeko la nchi. 6Basi wale malaika saba waliokuwa na zile tarumbeta saba wakajiandaa kuzipiga.

*Baragumu ya Kwanza: Mimea yateketezwa.*

7Malaika wa kwanza akaipiga tarumbeta yake, pakatokea mvua ya mawe na moto uliochanganyika na damu, vikatupwa kwa nguvujuu ya nchi na theluthi ya dunia ikateketea, theluthi ya miti ikateketea na majani yote mabichi yakateketea.

*Baragumu ya Pili: Bahari yaangamizwa.*

8Malaika wa pili akaipiga tarumbeta yake na kitu kama mlima mkubwa unaowaka moto kikatupwa baharini. Theluthi ya bahari ikawa damu, 9theluthi ya viumbe vyenye uhai viishivyo baharini vikafa na theluthi ya meli zikaharibiwa.

*Baragumu ya Tatu: Maji yanaharibiwa.*

10Malaika wa tatu akaipiga tarumbeta yake na nyota kubwa iliyokuwa ikiwaka kama taa, ikaanguka toka angani, ikaangukia theluthi ya miti na chemchemi za maji. 11Nyota hiyo inaitwa “Uchungu (pakanga)”. Theluthi ya maji yakawa machungu na watu wengi wakafa kutokana na maji hayo kwa maana yalikuwa machungu.

*Baragumu ya Nne: Anga laangamizwa.*

12Kisha malaika wa nne akaipiga tarumbeta yake na theluthi ya jua, theluthi ya mwezi na theluthi ya nyota, zikapigwa. Kwa hiyo theluthi moja ya mwanga ikawa giza. Theluthi ya mchana ikawa haina mwanga na pia theluthi ya usiku. 13Nilipokuwa tena nikitazama, nikamsikia tai mmoja akipiga kelele kwa sauti kuu wakati akiruka katikati ya mbingu, akisema, “Ole, Ole, Ole, wa watu waishio duniani, kwa sababu ya tarumbeta ambazo malaika wengine watatu wanakaribia kuzipiga.”

*Baragumu ya Tano: Nzige waja kutoka Shimo Lisilo na Mwisho.*

9:1 Malaika wa tano akaipiga tarumbeta yake, nami nikaona nyota iliyokuwa imeanguka toka angani hadi ardhini. Nyota hiyo ilipewa ufunguo wa shimo lisilo na mwisho. 2Alipolifungua hilo shimo lisilo na mwisho, moshi ukapanda kutoka humo kama moshi wa tanuru kubwa sana. Jua na anga vikatiwa giza na ule moshi uliotoka katika hilo shimo

lisilokuwa na mwisho. 3Ndipo katika ule moshi wakatoka nzige wakaenda juu ya nchi, nao wakapewa nguvu kama zile za nge wa duniani. 4Wakaambiwa wasidhuru majani ya nchi, wala mmea wala mti wo wote, bali wawadhuru tu wale watu ambao hawana alama ya Mungu kwenye vipaji vya nyuso zao. 5Wakaruhusiwa kuwatesa kwa muda wa miezi mitano, lakini wasiwaue. Uchungu wa kuuma kwao ulikuwa kama ule wa mtu aumwapo na nge. 6Katika siku hizo watwatafuta kifo lakini hawatakiona, watatamani kufa, lakini kifo kitawakimbia. 7Wale nzige walikuwa na umbo kama la farasi waliotayarishwa kwa ajili ya vita. Kwenye vichwa vyao kulikuwa na kitu kama taji za dhahabu na nyuso zao zilikuwa kama za binadamu. 8Walikuwa na nywele kama za wanawake na meno yao yalikuwa kama ya simba. 9Walikuwa na dirii kama za chuma na sauti za mabawa yao zilikuwa kama ngurumo za magari mengi ya farasi wanaokimbilia vitani. 10Walikuwa na mikia yenyenye miiba ya kuumia kama nge. Nguvu yao ya kutesa watu kwa huo wa miezi mitano ilikuwa katika hiyo mikia yao. 11Walikuwa na malaika kutoka kwenye hilo shimo lisilo na mwisho kama mfalme wao, ambaye jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni na kwa Kiyunani ni Apolioni. 12Ole ya kwanza imepita, bado nytingine mbili zinakuja.

*Baragumu ya Sita: Malaika toka Mto Frati.*

13Malaika wa sita akaipiga tarumbeta yake, nami nikasikia sauti ikitoka katika zile pembe nne za madhabahu ya dhahabu iliyoko mbele za Mungu. 14Ile sauti ikamwambia yule malaika wa sita mwenye tarumbeta, "Wafungulie wale malaika wanne waliofungwa kwenye ule mto mkubwa Eufrati." 15Basi wale malaika wanne wakafunguliwa ambao walikuwa wamekekwa tayari kwa ajili ya saa hiyo na siku hiyo na mwezi huo na mwaka huo ili wawaue theluthi ya wanadamu. 16Idadi ya majeshi wapandao farasi ilikuwa 200,000,000. 17Hivi ndivyo nilivyowaona hao farasi na wapanda farasi katika maono yangu: Wapanda farasi walivaa dirii vifuanu zenyne rangi ya moto na yakuti samawi na kiberiti. Vichwa vya hao farasi vilikuwa kama vichwa vya simba. Moto, moshi na kiberiti vilitoka vinywani mwao. 18Theluthi ya wanadamu wakauawa kwa maafa hayo matatu, yaani, huo moto, moshi na kiberiti, vilivyotoka kwenye vinywa vya hao farasi. 19Nguvu za hao farasi zilikuwa katika vinywa vyao na kwenye mikia yao, kwa sababu mikia yao ilikuwa kama nyoka; yenyenye vichwa ambayo waliiutumia kuwadhuru watu. 20Wanadamu waliosalia, ambao hawakuuawa katika maafa hayo, bado walikataa kutubu na kuacha kumwabudu shetani na vitu walivytengeneza kwa mikono yao wenyewe, yaani, sanamu za dhahabu, za fedha, za shaba, za mawe na za miti, ambazo haziwezi kuona, kusikia wala kutembea. 21Wala hawakutubu na kuacha matendo yao ya uuaji, uchawi, uasherati wala wizi wao (Ufunuo 8:1-13, 9:1-21).

Hivyo kuna baragumu nyingi zitakazopulizwa katika Kitabu cha Ufunuo, na ndiyo maana parapanda nyingi ziliamuliwa zipulizwe kwenye Sikukuu ya Baragumu (Walawi 23:24)—tunatumaini wengi watauona uhusiano huo.

Lakini iliyo ya umuhimu mkubwa zaidi, katika swala hili la baragumu zinazohusiana na Sikukuu ya Baragumu, pengine ni

ile ya mwisho, Baragumu ya Saba. Hapa ni kile ambacho Ufunuo inafundisha kuhusiana nayo (kama awali, italiki hazimo katika Biblia, bali zimeongezwa na wachambuzi).

*Baragumu ya Saba: Ufalme Unatangazwa Rasmi.*

15Yule malaika wa saba akaipiga tarumbeta yake, pakawa na sauti kubwa mbinguni iliyosema: "Ufalme wa ulimwengu umekuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala milele na milele" 16Nao wale wazee ishirini na wanne, waliokuwa wameketi mbele za Mungu, kwenye viti vyao vya enzi wakaanguka kifudifudi wakamwabudu Mungu, 17wakisema, "Tunakushukuru, Bwana Mungu Mwenyezi, uliyeko na uliyekuwako, kwa kuwa umetwaa uweza Wako mkuu na ukaanza kutawala. 18Mataifa walikasirika kwa kuwa wakati wa ghadhabu Yako umewadia. Wakati umewadia wa kuwahukumu waliokufa na kuwapa thawabu watumishi wako manabii na watakatifu wako pamoja na wale wote wanaolireshimu Jina Lako, wakubwa kwa wadogo na kuwaangamiza wale wanaoiangamiza dunia". 19Ndipo Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa na sanduku la agano lake likaonekana humo ndani. Kukatokea mianga ya umeme wa radi, ngurumo, sauti za radi, tetemeko la nchi na mvua kubwa ya mawe (Ufunuo 11:15-19).

Ufalme wa Mungu ujao ni ule ambao Yesu Kristo anawataka wafuasi wake wautangaze kwa sasa na kisha ndipo mwisho uwadie (Mathayo 24:14).

### **Je, Wakristo wa Enzi za Mwanzo Waliishika Sikukuu ya Baragumu?**

Pamoja na kwamba amri ya kuishika Sikukuu ya Baragumu haikutajwa moja kwa moja katika Agano Jipy, mbali ya kufundisha juu ya nini inamaanisha, wote Yesu pamoja na Mtume Paulo waliishika.

Biblia inafundisha kwamba Yesu Kristo aliishika Sheria na wala hakutenda dhambi (Waebrania 4:15), hivyo alizishika Sikukuu Takatifu zote za majira ya kipupwe ikiwemo na Sikukuu ya Baragumu.

Pengine ni muhimu kuelewa kwamba Mtume Paulo ni lazima aliishika Sikukuu ya Baragumu hata baada ya kuongoka kwake na kuwa Mkristo.

Ebu jionee baadhi ya maelezo kutoka kwa Mtume Paulo:

17...."Ndugu zangu, ingawa sikufanya jambo lo lote dhidi ya watu wetu au dhidi ya desturi za baba zetu.... (Matendo 28:17).

4Ingawa mimi mwenyewe ninazo sababu za kuutumainia mwili. Kama mtu ye yote akidhani anazo sababu za kuutumainia mwili, mimi zaidi. 5Nilitahiriwa siku ya nane, mimi ni Mwisraeli wa kabilia la Benyamini, Mwebrania wa Waebrania. Kwa habari ya sheria, ni Farisayo, 6kwa habari za juhud, nilikuwa nalitesa kanisa, kuhusu haki ipatikanayo kwa sheria, mimi nilikuwa sina hatia (Wafilipi 3:4-6).

Kwa kuwa Mtume Paulo alisema kwamba alizishika desturi za watu wake, basi ni dhahiri, alizishika Sikukuu Takatifu zote za majira ya Kipupwe ikiwemo na Sikukuu ya Baragumu. Kama sivyo, asingeweza kujigamba kama alivyobainisha kwenye maelezo hayo hapo juu ya Matendo 28:17 wala ya Wafilipi 3:4-6.

Wengine hujiuliza endapo labda baada ya nyakati za akina Mtume Paulo, ikiwa Wakristo waliendelea kuishika Sikukuu ya Baragumu. Jibu ni NDIYO, Wakristo waaminifu waliendelea kufanya hivyo. Na walifanya hivyo hata wale waliokuwa kwenye maeneo ya watu wa mataifa.

Kwa mfano, Polycarp wa Smyrna alizishika Sikukuu Takatifu za majira ya Kipupwe:

"Nitayatoa maelezo kwa mfuatano, hivyo kufikia hadi kwenye historia ya Polycarp mbarikiwa... Hivyo pia alifuata usomaji wa Maaandiko Matakatifu tangia utoto wake hadi izeeni, yeze mwenyewe akiyasoma kanisani na kuwaasa wengine nao wafanye hivyo, akiwaelea kwamba kuvisoma vitabu vya Sheria na vya Manabii ilikuwa ndiyo msingi wa kuipokea neema, kuandaa na kunyoosha njia za Bwana, ambayo ni miyo, iliyo kama vitabu ambamo aina fulani za imani na mitazamo potofu ambayo ilikuwa imeandikwa kabla elimu sahihi haijaja, hunyooshwa na kusawazishwa kupitia kulielewa neno la Agano la Kale, pamoja na tafsiri sahihi juu yake, ambapo, pale Raho Takatifu ya Mungu inapokuja kama kalamu juu ya miyo hii, neema na shangwe iletwayo na sauti ya Injili pamoja na mafundisho ya kutokufa naya Kristo aliyeo mbinguni yataweza kuandikwa vema ndani yao. Na aliwaambia kwamba wasingeweza kuipokea chapa ya mhuri wa Mungu itolewayo kupitia ubatizo na wala wasingeweza kudhihirisha utayari wao utokanao na kufanya wana kupitia tendo hilo, hadi kwanza nta iwe imeyeyushwa na kujazwa kwenye nyufa walizokuvanazo ndani yao. Hivyo pia alifikiri kwamba miyo ya waliomsikiliza inapaswa kwanza ilainishwe na ikubali kutiwa chapa ya Neno. Kwani alieleza kwamba, miyo ya wale walioingia kwenye imani hivi karibuni ilifunguka sawa na milango iliyokuwa imefungwa; na ndivyo manabii walivyoamliwa na Mungu: "Pigeni kelele kwa nguvu wala msiache, inueni sauti zenu kama baragumu". Ni nini mtu awezacho kusema, pale hata yeze ambaye alikuwa mpole kuliko watu wengine wote atokeapo akisihi na kuhubiri kwa sauti kuu wakati wa Sikukuu ya Vibanda? Maana imeandikwa; Na katika siku ya mwisho, ile siku kuu ya sikukuu, Yesu alisimama na kusema kwa sauti kuu akisema: Mtu yeyote akiona kiu, na aje kwangu anywe. (Imenekuliwa toka makala iitwayo: Pionius, Life of Polycarp (1889) from J. B. Lightfoot, The Apostolic Fathers, vol. 3.2, pp.488-506).

Hivyo Polycarp, kulingana na maelezo hapo juu, yaonekana alikuwa akifundisha juu ya Sikukuu Takatifu za majira ya Kipupwe ambazo huanza na Sikukuu ya Baragumu, na hufuatiwa na Sikukuu ya Vibanda na baadaye kumalizia na Sikukuu Takatifu ya Mwisho.

Vilevile katika Asia Ndoto kunataarifa zilizoandikwa kwamba, hadi kufikia mwishoni mwa karne ya nne, John Chrysostom aliwalaamu waumini wa Kristo waliokuwa wakiishika Sikukuu ya Baragumu, imeandikwa:

Sikukuu za Wayahudi walio waovu na wakuhurumia karibu zitawadia dhidi yetu moja baada ya nyingine na kwa mfaatano wa haraka: Sikukuu ya Baragumu, Sikukuu ya Vibanda, Sikukuu ya Kufunga (Mfungo). Wapo wengi mionganini mwetu ambaao husema wao wanaamini sawa na sisi tunavyoamini. Lakini baadhi ya hawa wataenda kuzishuhudia sikukuu hizi na wengi wataungana na Wayahudi katika kusherehekeea Sikukuu hizi ikiwemo pia hata kushiriki katika Mfungo wao. Kwa sasa ninatamani kuziondolea mbali desturi hizi potofu kutoka kwenye kanisa ...Maana iwapo sikukuu hizi za Wayahudi ni tukufu na bora, basi za kwetu ni za uongo... Je Mungu anazichukia sikukuu zao nanyi mnashiriki katika kuzishika? Mungu hajasema sikukuu hii ama ile, bali kazikataa zote. (Imenekuliwa toka hotuba ya John Chrysostom. "Homily I Against the Jews" (Tuhuma Dhidi ya Wayahudi) I:5;VI:5;VII:2. Ilihubiriwa huko Antiochia, Syria kwenye majira ya Kipupwe ya mwaka wa 387 B.K.; Medieval Sourcebook: Saint John Chrysostom (c.347-407): Eight Homilies Against the Jews. Fordham University. <http://www.fordham.edu/halsall/source/chrysostom-jews6.html> 12/10/05).

Mfungo mwovu na usio safi wa Wayahudi sasa tayari umewadia muda wake. Mnafikiri ni mfungo, wala msishangae kwanini nimeuita kuwa ni mchafu...Lakini sasa mwovu huwavuta wake zenu wahudhurie Sikukuu ya Baragumu nao huyaelekeza masikio yao kwa kuuitikia wito huu, wala hamuwazui. Mnawaachia wajichanganye kwenye dhihaka ya wasio-wacha Mungu, mnawaruhusu wavutwe kuzifuata njia za upoto. (Mahubiri ya John Chrysostom. "Homily II against the Jews" (Tuhuma Dhidi ya Wayahudi) I: 1; III: 4. Yalihubiriwa kule Antiochi, Syria; siku ya Jumapili, Septemba 5, 387 B.K.).

Sasa, wakati mengi ya madai ya John Chrysostom ni ya kimakosa, ukweli ni kwamba asingeliweza kutoa hotuba hizo zinazohusu kuwalaamu Wakristo waliokuwa wanazishika hizi sikukuu iwapo hakuna aliyekuwa anamkiri Kristo aliyekuwa akiishika Sikukuu ya Baragumu pamoja na Sikukuu Takatifu zingine za majira ya Kipupwe katika kipindi hiki cha karne ya nne.

Zaidi ya hapo, waumini wa kanisa la Rumi, Jerome na Epiphanius, kuelekeea muda huohuo, waliandika kwamba Wakristo, ambaao wao waliwaita kuwa ni wa kundi la "Wanazarayo" walizishika Sikukuu Takatifu za majira ya Kipupwe.

Pamoja na hayo, tambua kwamba Wakristo washika Sabato wa maeneo ya nchi ya Transylvania, katika miaka ya 1500 (na inaaminwi kuwa hata baada ya hapo) walizishika Sikukuu Takatifu za majira ya Kipupwe kama vile Sikukuu ya Upatanisho pamoja na Sikukuu ya Baragumu (inayoitwa Sikukuu ya Ukumbusho hapo chini):

Wasabato hawa walijichukulia kuwa wao ni Watu wa Mataifa walioongoka..Waliendelea kuzishika sikukuu za kibiblia... Sikukuu ya Upatanisho ilikuwa kwao ni siku ya mfungo, ijapokuwa walisisitiza kwamba kitubio kinapatikana zaidi pale mtu anapojiweka katika mazingira ya amani, utulivu na kutafakari zaidi juu ya sheria na maisha yake hata kuliko kufunga. Sikukuu ya Ukumbusho (ambayo kwao ndiyo ilikuwa Mwaka Mpya, ambayo waliisherehekeea wakati wa

majira ya Kipupwe) ilikuwa ndiyo siku ambayo walimshukuru Mungu hasa kwa uumbaji wake wa ulimwengu. Hakukutajwa lolote juu ya kutahiriwa, hivyo ni dhahirki hawakuwa wanafuata tohara (Imenekuliwa toka makala ya Liechty D. "Sabbatarianism in the Sixteenth Century" (Usabato katika enzi za Karne ya Kumi na Sita). Andrews University Press, Berrien Springs (MI), 1993, pp. 61-62).

Watu waliojitalidi kuwa waaminifu kwa Biblia wamekuwa wakiishika Sikukuu ya Baragumu katika nyakati zote za historia na sisi tulio katika Kanisa la Continuing Church of God tunaendelea kufanya hivyo katika enzi hizi za karne ya 21.

### **Vipengele vya Imani ya Kanisa la Continuing Church of God: Sikukuu ya Baragumu**

Katika Vipengele vya Imani ya Kanisa letu, Continuing Church of God inaeleza:

Sikukuu ya Baragumu inasaidia kutoa picha ya "Kupigwa kwa Baragumu Saba" kulikofafanuliwa katika kitabu cha Ufunuo (Ufunuo 8,9,11:15-18), ikiwemo "Parapanda ya Mwisho". "Maana parapanda italia, nao wafu watafufuliwa wakiwa bila ya uharibifu, nasi tutabadirishwa" (1 Wakorintho 15:52). "Maana Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni akiambatana na mliong mkuu, pamoja na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu Baba. Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza" (1 Wathesalonike 4:16). Kila mwaka wa saba, mwaka mba ni wa sabato kwa ardhi (kuiacha ardhi ipumzike) na kuachilia madeni huanzia kwenye siku hii (Walawi 25:1-7; Kumbukumbu la Torati 15:7-11).

Sikukuu ya Baragumu ni ya muhimu sana na inatakiwa ichukuliwa kwa umakini na wale wanaomkiri Kristo.

Biblia inafundisha wazi kabisa kwamba Yesu Kristo atarejea akiambatana na mliong mkuu wa baragumu (Mathayo 24:30-31; 1 Wathesalonike 4:16-17), na inaiita baragumu hiyo kuwa ni "parapanda ya mwisho" (1 Wakorintho 15:51-52). Wale ambao hawazishiki sikukuu takatifu za kibiblia, kwa ufupi hawawezi kuzielewa vema nabii za kibiblia, na wengi wajiiitao wapentekoste wameipokea dhana potofu ya "Kunyakuliwa kwa Kanisa" klabla Kristo hajarejea, ambayo kamwe haipo wala haitatokea, kulingana na unabii wa 1 Wathesalonike 4:16-17; ambapo haya hayatatokea hadi parapanda ya mwisho ipulizwe, ambayo Wakristo inawabadiri baada ya kuwafufua toka kaburini, na ndiyo inamleta Kristo (1 Wakorintho 15:51-52).

Biblia inakubaliana na fundisho kwamba wale ambao kwa sasa wameandikwa katika Kitabu cha Uzima watafufuliwa wakati wa mliong wa parapanda ya mwisho (1 Wakorintho 15:51-52), ambao ndio unaoashiriwa na Sikukuu ya Baragumu (ambayo hutimia kila mwezi Tishri 1 unapofika).

Waumini wa Kristo wa enzi za mwanzo wa Kanisa katika maeneo ya watu wa mataifa, waliishika Sikukuu ya Baragumu. Wakristo waaminifu wameendelea kufanya hivyo hadi leo.

Sisi tuliomo katika Kanisa la Continuing Church of God

tumebarikiwa kwa kuwa tunaliamini Agano Jipyaa na tunazishika Sikukuu Takatifu za kibiblia-hivyo tumeweza kuwa na uelewa sahihi zaidi (ona Matendo 18:26) wa mpango wa kweli wa Mungu.

# IMANI: NI KITU GANI? IMANI HUONYESHWA JINSI GANI?

Na Bob Thiel

Yesu alisema kwamba, pamoja na rehema na hukumu (uamuzi wa haki), imani ndiyo iliyo kuwa moja ya mambo mazito zaidi, muhimu zaidi, katika sheria (Mathayo 23:23).

Siku moja:

5Wanafunzi Wake wakamwambia Bwana, "Tuongezee imani" (Luka 17:5).

Badala ya kuwaelezea namna ya kuiongeza imani yao, Yesu aliwafahamisha kwamba walikuwa na imani ndogo tu.

Lakini katika maeneo mengine ya Biblia, Yeye pamoja na waandishi wengine walitoa maelezo ya kina kuhusu imani namna iwezavyo kuongezwa. Makala hii fupi itajadili maswala kadhaa ya imani. Kujaribu kujadiri yote itahitaji mada ndefu sana. Kwa mfano, nakala ya Kiingereza ya New King James Version (NKJV) imelitaja neno "imani" takribani mara 243 katika Agano Jipyä, (mara 2 katika Agano la Kale) na neno "aminifu" mara 53 katika Agano Jipyä (na mara 32 katika Agano la Kale).

## Tafsiri ya Biblia ya Imani ni Ipi?

Biblia inatoa tafsiri ya imani kama ifuatavyo:

1Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni udhahiri wa mambo yasiyoonekana. 2Maana kwa imani baba zetu wa kale walishuhudiwa. 3Kwa imani tunafahamu kwamba ulimwengu uliumbwu kwa neno la Mungu, na vitu vyote vinavyoonekana vilumbwa kwa vitu visivyoonekana.

6Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana ye yote anayemjia Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko na ya kuwa huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii "(Waebrania 11:1-3,6).

Je unaamini kwa dhati kwamba Mungu anawapa tuzo wale, ambao amewaita na kuwateua, wale wamtafutao kwa bidii? Ikiwa ni hivyo, hilo linamatokeo gani katika maisha yako? Neno la Kigiriki ambalo mara nyingi limetafsiriwa katika Agano Jipyä kama 'Imani' ni πίστις, ambalo limetafsiriwa katika Kiingereza kama pistis. Kamusi ya kiingereza ya BibleSoft inalifafanua kuwa linamaanisha:

πίστις pistis (pis'-tis) ushawishi, mfano kusadiki; kujithibitisha moyoni (juu ya ukweli wa kidini, au ukweli juu ya Mungu au juu ya mwalimu wa dini), hasahaha kuwa na matumaini juu ya Kristo kwa wokovu; kifikra, kuwa na uthabiti wa kutumaini katika utaalim wa kazi; kwa kuongeza, ni mfumo wa ukweli wa kidini (Injili) wenyewe: (Biblesoft's New Exhaustive Strong's Numbers and Concordance with Expanded Greek-Hebrew Dictionary. Copyright © 1994, 2003, 2006 Biblesoft, Inc. and International Bible Translators, Inc).

Kwa mfumo wa ukweli, angalau mhubiri mmoja wa Kanisa la Mungu alidhani kwamba inahusu pia dhana ya kazi, na kwa vile Wakristo nao ni sehemu ya kazi ya Mungu, ni halali kusema kwamba imani ni sehemu ya kazi. Na ni dhahiri inahitaji kiwango kikubwa cha imani nyakati zingine ili kuweza kuifanya kazi. Ebu jionee kitu ambacho Wakristo wanategemewa kukifanya:

3.... mwishindanie imani iliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu (Yuda 3).

Yuda anaandika kwa Wakristo waweke jitihada katika imani, wale ambao wameitwa na kuteuliwa (1 Wakorintho 1:26-28; Mathayo 22:14). Siyo kwamba tu tunatakiwa kuwa na imani, bali pi tunatakiwa kuiwekea jitihada (Mathayo 24:14; 28:19-20). Na hilo ndilo ambalo sisi tulio wa Continuing Church of God tunajitahidi kulifanya.

## Onyesha Imani kwa Kutenda, Si kwa Kudai Unaamini tu

Paulo aliandika:

7"Kwa maana twaenenda kwa imani wala si kwa kuona "(2 Corinthians 5:7).

Katika uhalisia, hili linamaanisha kwamba tunaishi katika njia ya Mungu ya maisha hata pale tuwapo katika majaribu na vishawishi, pale mambo yaonekanapo kuwa hayaendi, au pale wengine wajaribupo kutulaghai. Paulo pia aliandika:

"Je, tunaibatilisha sheria kwa imani? La, hasha! Badala yake tunaithibitisha sheria" (Warumi 3:31).

Kwa kuongeza, Yakobo aliandika:

17Vivyo hivyo, imani peke yake kama haikuambatana na matendo, imekufa. 18Lakini mtu mwingine atasema, "Wewe unayo imani, mimi ninayo matendo." Nionyeshe imani yako pasipo matendo nami nitakuonyesha imani yangu kwa matendo. 19Unaamini kwamba kuna Mungu mmoja. Vema! Hata mashetani yanaamini hivyo na kutetemeka.

20Je, wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani bila matendo haifai kitu? 21Je, Abrahamu baba yetu hakuhesabiwa haki kwa kile alichotenda, alipomtoa mwanawе Isaka madhabahuni? 22Unaona jinsi ambavyo imani yake na matendo yake vilikuwa vinatenda kazi pamoja, nayo imani yake ikakamilishwa na kile alichotenda. 23Kwa njia hiyo yakatimizwa yale Maandiko yasemayo, "Abrahamu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki," naye akaitwa rafiki wa Mungu. 24Mnaona ya kwamba mtu huhesabiwa haki kwa yale anayotenda wala si kwa imani peke yake. 25Vivyo hivyo, hata Rahabu, yule kahaba, hakuhesabiwa haki kwa yale aliyyotenda alipowapokea wale wapelelezi na kuwaambia waende njia nyininge? 26Kama vile ambavyo mwili pasipo roho umekufa, kadhalika nayo imani pasipo matendo imekufa (Yakobo 2:17-26).

Hivyo basi, imani inaenda zaidi ya kusadiki peke yake. Imani iliyo hai inahusisha pia matendo ambayo Mungu anayakubali. Si tu

kuishika Sabato ama Sikukuu ya Vibanda pale ionekanapo kuwa kuna ugumu, bali pia ni kwa kulipa zaka, kwa kuepuka sikukuu za kipagani kama vile Christmas, na kwa kuwa mwaminifu katika ulimwengu usio na uaminifu. Lakini pia ni kwa kuwapenda wale ambao hawakupendi wewe (Mathayo 5:44-48).

Yesu alifundisha:

48Kwa hiyo iweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu” (Mathayo 5:48).

Hatuokolewi kwa matendo, bali kwa imani:

8Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, 9si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. 10Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo (Waefeso 2:8-10).

Jionee kwamba, Biblia yaonyesha kwamba pamoja na kwamba tunaokolewa kwa neema, hata hiyo nayo ni zawadi kutoka kwa Mungu. Gundua kwamba tuliumbwa katika Kristo Yesu kwa ajili ya matendo mema.

## Walioitwa na Kuteuliwa Wanapaswa kuwa Waaminifu

Wakati karibia wote walio kweli kwenye Kanisa la Mungu wanaamini kwamba wameitwa na kuteuliwa, wote sharti watambue kwamba wanatakiwa pia kuwa waaminifu. Pale Yesu atakaporejea, ebu jionee ni yupi atakayekuwa naye:

14... Yeye ni Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme; na hao walio pamoja naye ndio walioitwa, wateule, na waaaminifu (Ufunuo 17:14).

Sisis tulioitwa na kuchaguliwa tunahitaji kubakia waaminifu. Si kwamba tumtii Mungu pekee, bali pia tunatakiwa tuwe na imani kwamba njia zake ndizo bora kwetu.

Ebu jionee maeneo mengine mawili katika Maandiko:

18Nayahesabu mateso yetu ya wakati huu kuwa si kitu kulinganisha na utukufu utakaodhihirishwa kwetu. 19Kwa maana viumbe vyote vinangoja kwa shauku kudhihirishwa kwa watoto wa Mungu (Warumi 8:18-19).

28Nasi tunajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hutenda kazi pamoja na wote wampendao, katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi Lake. 29Maana wale Mungu aliowajua tangu mwanzo, pia aliwachagua tangu mwanzo, wapate kufanana na mfano wa Mwanawe, ili Yeye awe mzaliwa wa kwanza mionganoni mwa ndugu wengi (Warumi 8:28-29).

Pale mambo yaendapo mrاما, tunahitaji imani tuweze kustahimili hadi mwisho.

## Imani dhidi ya Hisia

Wengi huidhania hisia kuwa ndiyo imani! Wakati waaminifu wanatakiwa wawe na matumaini kwa Mungu, imani siyo hisia ambazo humjaa mtu kifkra na kwa mda mfupi.

Sasa, ni ukweli kwamba iwapo Shetani anamsumbuwa mtu, hatua za maramoja zapaswa kuchukuliwa:

7Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia. 8Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, ninyi wenyenye dhambi na kuisafisha mioyo yenu, ninyi wenyenye nia mbili (Yakobo 4:7-8).

5.... “Mungu huwapinga wenyenye kiburi bali huwapa wanyenyekevu neema.”

6Basi, nyenyekeeni chini ya mikono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati Wake. 7Mtwikeni Yeye fadhaa zenu zote kwa maana hujishughulisha sana na mambo yenu. 8Muwe na kiasi na kukesha, maana adui yenu Ibilisi, kama simba angurumaye huzungukazunguka akitafuta mtu ili apate kummeza. 9Mpingeni huyo mkiwa thabiti katika imani, mkiija ya kwamba mateso yayo hayo yanawapata ndugu zenu pote duniani. 10Nanyi mkiisha kuteswa kwa kitambo kidogo, Mungu wa neema yote aliyewaita kuingia katika utukufu Wake wa milele ndani ya Kristo, Yeye mwenywewe atawatengeneza upya, atawasaidia, atawatia nguvu na kuwathibitisha (1 Petro 5:5-10).

Na kwa kuchukua hatua hizo za kibiblia ni lazima kutuongezee imani. Lakini hilo silo lilelile sawa na namna ya fikra za hisia za kumfanya mtu kwa muda ajisikie anayo imani!

## Mwenyehaki Ataishi kwa Imani

Wakristo wameteuliwa ili wawe matajiri katika imani:

5Ndugu zangu, sikilizeni: Je, Mungu hakuwachagua wale walio maskini machoni pa ulimwengu kuwa matajiri katika imani na kuurithi Ufalme aliowaahidi wale wampendao? (Yakobo 2:5).

Biblia, katika maeneo matatu inafundisha kuwa wenyehaki wataishi kwa imani.

Sehemu ya kwanza ni katika Habakuki 2:4:

4“Tazama, amejaajaa majivuno, anavyovitamani si vya unyofu. Lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake.

Mfananisho baina ya wenyenye majivuno na wenyehaki unaonyesha kwamba waaminifu hawamo katika kundi la wenyenye majivuno, bali ni mionganoni mwa wema. Wenyenye majivuno wanajitumainia wao wenywewe kwa kiwango kikubwa.

Paulo aliandika:

11Basi ni dhahiri kwamba hakuna mtu ye yote anayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa sheria, kwa maana, “Mwenye haki ataishi kwa imani”. 12Lakini sheria haitegemei imani,

kinyume chake, "Ye yote atendaye matendo ya sheria ataishi kwa sheria (Wagalatia 3:11-12).

Hii aya ya mwisho yaonyesha kwamba ijapokuwa sheria siyo imani, lakini bado mwenyehaki anatakiwa kuishika.

Katika Warumi 1:17-19, Mtume Paulo aliandika:

17Kwa maana katika Injili haki itokayo kwa Mungu imedhihirishwa, haki ile iliyo kwa njia ya imani hadi imani. Kama ilivyoandikwa: "Mwenye haki ataishi kwa imani."

18Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu wao, 19kwa maana yote yanayoweza kujulikana kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa sababu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao.

Kuhusu haki ya Mungu, Zaburi 119:172 inaeleza:

172Ulimi wangu na uimbe kuhusu neno lako, kwa kuwa amri zako zote ni za haki.

Waebrania inaeleza yafuatayo kuhusu baadhi ya wenyehaki waliokuwa waaminifu:

13Watu hawa wote wakafa katika imani bila kuzipokea zile ahadi, lakini waliziona kwa mbali na kuzishangilia. Nao walikubali kwamba walikuwa wageni na wasiokuwa na maskani hapa duniani. 14Watu wasemao mambo kama haya, wanaonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe. 15Kwa kweli kama wangkuwa wanafikiru kuhusu nchi waliyoiacha, wangalipata nafasi ya kurudi huko. 16Lakini badala yake wanamatmani nchi iliyo bora zaidi, yaani, nchi itokayo mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wao, kwa kuwa amekwisha kuandaa mji kwa ajili yao (Waebrania 11:13-16).

Hivyo waaminifu, pamoja na kuishi kwa kufuata njia ya Mungu ya maisha hapa duniani, wametilia mkazo zaidi kwenye tumaini la tuzo yao inayokuja baadaye kutoka kwa Mungu. Wanau "tafuta kwanza ufalme" (Mathayo 6:33). Lakini pia hapa duniani wanazishika amri:

12Hapa ndipo penye subira na uvumilivu wa watakatifu, yaani, wale wanaozishika amri za Mungu na imani ya Yesu (Ufunuo 14:12).

Lakini siyo kirahisi siku zote kuwa sehemu ya waaminifu. Neno 'subira na uvumilivu wa watakatifu' linaashiria kupitia taabu adha na dhiki kubwa katika nyakati zingine.

Kumbuka kwamba Biblia inaihusisha imani na matumaini/matarajio, "iman ni kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo". Tumaini ni swala ambalo tunatakiwa tuwe nalo:

15Nami ninalo tumaini kwa Mungu, ambalo hata wao wenyewe wanalikubali kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, kwa wote wenye haki na wasio na haki. 16Kwa hiyo ninajitahidi siku zote kuwa na dhamiri safi mbele za Mungu na mbele za wanadamu (Matendo 24:15-16).

Si kwamba tu tumaini linatakiwa lidhihirishwe, imani ni ya umuhimu mkubwa. Mtu huonyesha imani yake kwa kuishi katika hiyo. Na hii siyo ile 'iman ya ukipofu'. Elewa kile ambacho Biblia inafundisha:

21Thibitisheni kila kitu. Yashikeni yaliyo mema. 22Jiepusheni na uovu wa kila namna (1 Wathesalonike 5:21-22).

Biblia inafundisha kwamba mtu anatakiwa athibitishe kwamba Mungu yupo na pia ayathibitishe yote anayojifunza kuhusu Mungu:

20Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili ya Mungu asiyonekana kwa macho, yaani, uwezo Wake wa milele na asili Yake ya Uungu, umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na udhuru.

21Kwa maana ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza Yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru, bali fikira zao zimekuwa batili na miyo yao ya ujinga ikatiwa giza (Warumi 1:20-21).

Ni dhahiri, tunapaswa tutafiti pia zaidi ya mambo ya kimwili:

16Kwa hiyo, hatukati tamaa. Ingawa utu wetu wa nje unachakaa, utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. 17Kwa maana dhiki yetu nyepesi iliyo ya kitambo inatutayarisha kwa ajili ya utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi kupita kiasi, 18kwa sababu hatuangalii yale yanayoweza kuonekana bali yale yasiyoweza kuonekana, kwa maana yale yanayoweza kuonekana ni ya kitambo tu, bali yale yasiyoweza kuonekana ni ya milele (2 Wakorintho 4:16-18).

Kwa kuishi kulingana na imani, mtu pia atanufaika kwa kukuta anathibitishe kwamba maelekezo na maamrishi yaliyomo katika neno la Mungu ni ya kweli –Wakristo hawana aina ya imani iliyo ya kiupofu, itokanayo na hisia tu na yenye msukumo usio wa kimantiki yoyote. Imani ni kitu halisi—ni uhakika wa mambo yatarajiwayo (Waebrania 11:1).

Ebu jionee kitu kingine ambacho Mtume Paulo aliandika:

12Pigana vile vita vizuri vya imani. Shika uzima wa milele ambao ndio ulioitiwa ulipokiri kule kukiri kuzuri mbele ya mashahidi wengi (1 Timotheo 6:12).

Walioitwa wanapaswa kuwa na imani na mifano ya wale waliotutangulia itatusaidia. Pale ninaposoma baadhi ya ulaghai kwenye internet unaolezwa kunihusu, ama iwapo utakutana na baadhi yake, kumbuka kile ambacho Yesu Kristo pamoja na Stefano mfiadini walichosema:

11Mna heri ninyi watu watakapowashutumu na kuwatesa na kunena dhidi yenu mabaya ya aina zote kwa uongo kwa ajili yangu. 12Furahini na kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kuu mbinguni, maana hivyo ndivyo walivyowatesa manabii waliokuwepo kabla yenu (Mathayo 5:11-12).

51“Ninyi watu wenyewe shingo ngumu, wasio tahiririwa mioyo wala masikio, daima hamwachi kumpinga Roho Mtakatifu, kama walivyofanya baba zetu. 52Je, kuna nabii gani ambaye baba zetu hawakumtesa? Waliwaua wale waliotabiri habari za kuja kwake yule Mwenye Haki, nanyi sasa mmekuwa wasaliti wake na wauaji? (Matendo 7:51-52).

Yesu anaeleza kwamba vielelezo vy a wale waliotutangulia vinapaswa kutusaidia kuyaelewa yale yanayotutokea leo. Naye Stefano alieleza wazi kwamba viongozi wa kidini siku zote hawatawasikiliza manabii wa Mungu.

### **Imani Huja Kwa Kusikia Neno la Mungu Kupitia Kwa Wale Mungu Aliowatuma Kuhubiri**

Imani ni fundisho la Mungu la kimsingi:

1 Kwa hiyo, tukiachana na mafundisho yale ya awali kuhusu Kristo na tusonge mbele ili tufikie utimilifu, si kuweka tena msingi wa mafundisho ya kuzitubia kazi zisizo na uhai na imani katika Mungu (Waebrania 6:1).

Je, imani hutoka wapi?

Paulo aliandika:

2 Je, mlipokea Roho wa Mungu kwa kushika sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani? (Wagalatia 3:2).

Paulo pia aliandika:

6Lakini ile haki itokanayo na imani husema hivi:... 8“Lile neno li karibu nawe, li kinywani mwako na moyoni mwako,” yaani, ni lile neno la imani tunalolihubiri. 13Kwa maana, “Kila mtu atakayeliitia Jina la Bwana, ataokoka.” 14Lakini watamwitaje Yeye ambaye hawajamwamini? Nao watawezaje kumwamini Yeye ambaye hawajamsikia? Tena watamsikiaje bila mtu ku wahubiria? 15Nao watahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyaoadikwa, “Ni mizuri mno miguu ya hao wanaohubiri Injili ya amani na kuleta habari ya mema!” 16Lakini si wote walioiti Habari Njema. Kwa maana Isaya asema, “Bwana, ni nani aliyeamini ujumbe wetu?” 17Basi, imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Mungu. 18Lakini nauliza, Je, wao hawakusikia? Naam, wamesikia”, (Warumi 10:6,8,13-18).

Kisha alisema kwamba sehemu ya tatizo la Israeli ilikuwa ni kutokuwa na utii (Aya ya 21). Hivyo Paulo anasema wazi kwamba ili watu waweze kuwa na imani, ni lazima kwanza wawasiklize wahubiri ambao Mungu amewatuma. Wahubiri hawa ni lazima wawe wakweli katika neno la Mungu (Aya ya 17). Kwa vile kusikia huja “kwa kulisikia neno la Mungu”, makala hii, sehemu kubwa ya mahubiri, pamoja na taarifa zingine ambazo sisi tulio katika kanisa la Continuing Church of God tumeziweka mbele zinanukuru kwa kiwango kikubwa toka Biblia, ambayo ndiyo neno la Mungu.

Umuhi muhi wa kuhubiri na wa neno la Mungu umethibitishwa katika maelekezo yafuatayo kutoka kitabu cha Matendo ya Mitume:

10Usiku ule ule, wale ndugu walioamini wakawapeleka Paulo na Sila waende zao Beroya. Walipowasili huko wakaenda kwenye sinagogi la Wayahudi. 11Hawa Wayahudi wa Beroya walikuwa waungwana zaidi kuliko wale wa Thesalonike, 12Wayahudi wengi wakaamini pamoja na wanawake na wanaume wa Kigiriki wa tabaka la juu (Matendo 17:10-12).

Kuyasoma Maandiko kila siku nalo, ni swala muhimu na lenye msaada katika kuiongeza imani. Lakini baadhi hudhani kwamba hilo peke yake ndilo wanalohitaji kulifanya!

### **Mungu Atatukirimia Mahitaji Yetu IWAPOTutamtanguliza Yeye na Kuwa na Imani**

Wengi mionganoni mwa wale ambao hawajaitwa ama kuteuliwa huwa na wasiwasu juu ya mambo mengi. Yesu alisema kwamba wafuasi wake hawapaswi kuwa namna hiyo:

24“Hakuna mtu ye yote aezaye kuwatumikia mabwana wawili, kwa kuwa ama atamchukia huyu na kumpenda yule mwingine, au atashikamana sana na huyu na kumdhara huyu mwingine. Ninyi hamwezi kumtumikia Mungu na mali.”

25“Kwa hiyo nawaambia, msiwe na wasiwasu kuhusu maisha yenu: mtakula nini au mtakunywa nini, au kuhusu miili yenu, mtavaa nini. Je, maisha si zaidi ya chakula na mwili zaidi ya mavazi? 26Waangalieni ndege wa angani, wao hawapandi wala hawavuni au kuweka ghalani, lakini Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Je, ninyi si wa thamani zaidi kuliko hao ndege? 27Ni nani mionganoni mwenu ambaye kwa kujitaabisha kwake aweza kuiongezea hata saa moja zaidi katika maisha yake au kuiongeza dhiraa moja kwenye kimo chake?

28“Nanyi kwa nini kujitaabisha kwa ajili ya mavazi? Fikirini maua ya shambani yameavyo. Hayafanyi kazi wala hayafumi. 29Lakini nawaambia, hata mfalme Solomoni katika fahari yake yote hakuvikwa kama mojawapo ya hayo maua. 30Lakini ikiwa Mungu anayavika hivi majani ya shambani, ambayo leo yapo na kesho yanatupwa motoni, je, hatawavika ninyi vizuri zaidi, enyi wa imani haba?

31Kwa hiyo msiwe na wasiwasu, mksema, ‘Tutakula nini?’ Au ‘Tutakunywa nini?’ Au ‘Tutavaa nini?’ 32Kwa maana watu wasiomjua Mungu ndio wanaoshindania hayo, lakini Baba yenu wa mbinguni anafahamu kwamba mnahitaji hayo yote. 33Lakini utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake yote na haya yote mtaongezewa. 34Kwa hiyo msiwe na wasi wasi kuhusu kesho, kwa sababu kesho itajitaabikia yenye. Yatosha kwa siku masumbufo yake” (Mathayo 6:24-34).

Je wewe unayo imani katika ahadi za Mungu? Yesu alisema kwamba walikuwepo wale waliokuwa na imani ndogo (haba), je, nawe unataka uchukuliwe na Yesu kuwa uko sawa na hao?


### **Maoni juu ya Imani**

Kuiongeza kiwango cha imani ni swala linalohitaji muda wa uhai wetu wote. Wakati mwingine huonekana kama jambo gumu


sana. Vipo vipengele vyake vingi sana, kiasi kwamba haviwezi kukamilishwa kwa makala fupi tu. Lakini kutokana na Biblia tunaona kwamba wale walioitwa na Mungu walikuwa na imani na waliishi kwa imani. Tumeona kwamba imani ni uhakika wa mambo yatarajiwayo. Kwamba imani huja kwa kulisikia neno la Mungu kuititia kwa wahubiri ambao Mungu amewatuma. Tumeona kwamba wenye haki waliyachunguza Maandiko ili wawe na uhakika kwamba wanaowahubiri kweli wametumwa na Mungu. Kwamba wenye haki walikuwa watiifu, kwamba hawakuacha kukusanya na wenzao, kwamba walifundishana na kutiana moyo, kwamba walisali, na pia kwamba walifunga (soma Mathayo 17:20-21).

Imani ni zawadi (karama) kutoka kwa Mungu (Waefeso 2:8) na ni kipengele muhimu cha sheria (Mathayo 23:23). Wenye haki wanategemewa waishi kwa imani (Habakuki 2:4; Warumi 1:17; Wagalatia 3:11). Biblia inaonyesha kwamba wenye haki wameidhihirisha imani yao kwa kuzishika amri na pia kwa kufanya yale ambayo Mungu anayataka wayafanye, hata ingawa bado walikuwa wakiishi katika ulimwengu usiomfuata Mungu.

Kwa kumwamini Mungu na kuyafanya mambo yote haya, Imani yaweza kuongezeka. Tafadhali jaribu kujitahidi uwe mtu ambaye kweli anayo imani Kristo arudipo.



*This booklet and others are available online at [www.ccog.org/booklets](http://www.ccog.org/booklets)*



Katika kijitabu kiitwacho: "Imani ni Nini", kilichoandikwa na Bwana Herbert W. Armstrong kimejadiri yafuatayo:

## KWANINI WATU HUPUNGUKIWA IMANI

Na sasa, kwa ufupi tu, Ni KWANINI hatuna IMANI, na tutawezaje kuipata, na itawezaje kuongezeka? Wengi sana husema, "Haielekei – Sijisikii, sijashawishika – kwamba nitalipata jibu."

Wanataka wasubiri hadi pale watakapopata USHAWISHI fulani, hali fulani ya KUJISIKIA, namna fulani ya uthibitisho ambayo wanawenza KUIHISI-kabla kwanza hawajaamini kwamba kweli watalipata jibu.

Lakini HIYO siyo imani! Hiyo ni HISIA!

Kujisikia kwako, ushawishi unaosubiri kuwa nao, msisimko wako, kwa dhahiri hauna hata sehemu moja ama nyingine katika kuhusiana na IMANI. IMANI INAHUSIKA NA NENO LA MUNGU PEKE YAKE! Swali moja unalohitaji ni, Je, Mungu ameliahidhi hilo katika Biblia? Iwapo ameahidi, basi yamkini, uwezekano, kujisikia, ushawishi, hisia, vyote hivi havina uhusiano wowote na swala hilo. Mungu anazo zaidi ya maelfu ya njia ambazo sisi hatuzijui, pale anapohitaji kujibu ama kutupatia chochote ambacho ametuahidi. Hatuhitaji tufahamu jinsi atakavyotekeleza ahadi hizo. Na hilo ni jambo jingine—ambalo kwa uhakika hatalitenda kwa NAMNA ambayo sisi tunaitarajia. Hivyo usijisumbue kutafakari uwezekano ambao Mungu atalifanya hilo. Umeweka tumaini lako kwa MUNGU MWENYE UWEZO WA AJABU! Basi UAMINI uwezo huo. Mungu hutenda kazi katika njia zisizojulikana na ni mtenda

miujiza. Kile ambacho amekiahidi, atakitekeleza; lakini elewa atakitenda kwa njia YAKE mwenyewe, na kwa WAKATI WAKE. Mwachie yote hayo YEYE na wewe WEKA IMANI tu. Litumainie Neno lake.

## Ni Zawadi Kutoka kwa Mungu

Na ni sharti tukumbuke, IMANI ni ZAWADI (Karama) KUTOKA KWA MUNGU.

Hivyo wengi hudhani kwamba kilakitu kingine chochote kinachotoka kwa Mungu ni zawadi yake, lakini IMANI inayohitajika kuvipokea vitu hivi ni kitu ambacho sisi wenyewe lazima kwa namna fulani tuitafute, tuwenayo, ama tujitahidi kuipata. Lakini tunatakiwa tustarehe tu na KUMTUMAINIA MUNGU, hata katika IMANI ambayo ndiyo hutuwezesha kupokea vingine vyote! (Waefeso 2:8).

Katika Ufunuo 14:12 tunakuta ufanuzi wa Kanisa la kweli la KIPINDI CHETU. Wale waliomo katika Kanisa hili wanayo IMANI YA YESU. Jionee, ni IMANI YA YESU! Siyo tu imani yetu sisi wenyewe katika YEYE, bali ni imani yake ye ye mwenyewe—yaani ni ileile imani ambayo yeye ndiyo aliyoitumia kutenda miujiza yake—iwemo ndani yetu na itende kazi ndani yetu!

Ni kwa jinsi gani utaweza kuipata? Mkaribie Mungu. Jitahidi umjue. Salimisha njia zako zote kwake YEYE, na uyatende mapenzi yake. Na kisha SALI. UNAFIKIA kumjua yeye kila uwapo katika KUSALI. Tumejiweka karibu mno na vitu vya kimwili. Kupitia MAOMBI, maombi ya mara kwa mara, unafikia kuwa karibu na MUNGU pamoja na mambo ya kiroho. Na ni hali ya furaha na ya shangwe kiasi gani, pale utakapokuwa umeifanya kiukweli!

Imani ni zawadi ya Mungu (Waefeso 2:8), lakini ni zawadi ambayo Wakristo wa kweli wanaweza kuistawisha. Siyo kupitia kujiskia kihisia, bali kupitia katika kuishi sawa na Yesu mwenyewe alivyioishi na kwa kumtumainia Mungu kuwa atahakikisha tunavuka majoribu na dhiki. Hisia zaweza kukupotosha, imani ni ya ukweli.

# HATUA YA MWISHO YA KAZI: KUIFIKIA AFRICA



Africa Conference, Nairobi, Kenya

Na Bob Thiel

Kanisa la Continuing Church of God linapaswa lielekee wapi?

Yesu alifundisha:

"18....Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. 19Kwa sababu hii, enendeni ulimwenguni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, 20nanyi wafundisheni kuyashika mambo yote niliyowaamuru ninyi. Hakika Mimi niko pamoja nanyi sikuzote, hadi mwisho wa nyakati" (Mathayo 28:18-20).

Vilevile alifundisha:

14Injili hii ya Ufalme itahubiriwa ulimwenguni pote, kuwa usuhuhuda kwa mataifa yote. Ndipo ule mwisho utakapokuja (Mathayo 24:14).

Hivyo, haya yanahusikaje na Africa?

Kiujumla yanahusika sana kwani hiyo ni mojawapo ya maeneo ambako Yesu anao wafuasi wengi. Tofauti na maeneo kama vile Ulaya na Amerika ya kaskazini, mawasiliano ya internet yapo kwa kiwango hafifu katika Africa, hivyo kuitekeleza vema Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19-20, mkutano wa viongozi wa Kanisa la Mungu kutoka Africa ya Mashariki ulifanyika, baada ya kuwa nimetua kwa muda huko Uingereza.

Nilifanikiwa kumbatiza mtu mmoja kutoka Msumbiji kule London kwenye siku ya Ijumaa (Machi 29, 2014) na baadaye kufanya ibada ya Sabato kwa mara ya kwanza kwa Kanisa la Continuing Church of God (CCOG) katika Uingereza kwenye siku ya Jumamosi. Asubuhi ya siku ya Jumapili nilisafiri kwa ndege kutoka uwanja wa ndege wa London hadi Nairobi, Kenya.

Usiku wa Jumapili, Mwakilishi wetu wa Kanda, Mchungaji Evans Ochieng, akiwa na mke wake Rose (ambaye ni shemasi) walikuja kunilaki kwenye uwanja wa ndege wa Nairobi. Tuliingia jijini Nairobi pamoja.

Mkutano wa Viongozi katika Nairobi

Siku ya Jumatatu, Mchungaji Evans Ochieng pamoja na mimi tulikutana kujadiri juu ya maswala mbalimbali yanayohusu kazi ya Mungu katika Kenya na Africa Mashariki kwa ujumla. Mwakilishi wa Kampuni ya Uchapishaji ya Nairobi alikuja kukutana nasi na tukajadiri kuhusu uwezekano wa kuchapisha baadhi ya mahitaji yetu ya vijitabu na magazeti na tukajadiriana juu ya gharama kwa kazi hiyo.

Baadaye siku hiyo, viongozi wa kanisa kutoka sehemu mbalimbali za Kenya walianza kuwasili jioni ya siku hiyo ya Jumatatu, na tulikutana na baadhi yao muda huo. Kesho yake ambayo ilikuwa ni Jumanne, watu wawili waliungana nasi kutoka Tanzania.

Ijapokuwa wengi wa viongozi hawa walikuwa tayari wameshakuwa na mahusiano na Kanisa la Continuing Church of God, hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa ameshakutana na mimi kabla ya mkutano huu. Viongozi kutoka kwenye vikundi vyenye mahusiano na Continuing Church of God nao pia walikuwa wamealikwa na walihudhuria.

Mkutano ulifanyikia kwenye ukumbi wa Hotel Karibu, Nairobi, Kenya. Karibu ni neno la Kiswahili lenye maana ya "unakaribishwa", na tuliwakaribisha viongozi mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali ya Kenya na pia kutoka Tanzania. Karibia wote waliohudhuria walilazimika kusafiri kutoka mbali kwa bus ili kuhudhuria.

Wazee, mashemasi, mashemasi wa kike, pamoja na wale ambao wamejitoa nyumba zao kufanya ibada kwa vikundi vidogo wote walihudhuria mkutano huo. Kulikuwa na jumla ya viongozi 34 waliohudhuria. Viongozi hawa ni wawakilishi wa watu zaidi ya 400 wa kwenye mikusanyiko ya ibada mbalimbali, ambayo si yote ni sehemu ya Kanisa la Continuing Church of God.

Katika Kenya, kulingana na maneno ya Yesu ya "muwafundishe kuyashika yote nilyowaamuru ninyi", mada nyngi mbalimbali zilijadiriwa kuanzia kutoa maelezo juu ya umuhimu wa upendo kwa kanisa, kuelezea historia ya Kanisa la Mungu, juu ya Uungu ulivyo hadi juu ya tarehe na wakati wa kuishika Pasaka; na pia juu ya maswala ya ndoa na taraka, juu ya ubatizo na juu ya Zaka hadi juu ya unabii na juu ya kipindi cha mwisho cha kazi ya Mungu. Katika Kenya kuna mahitaji mengi ya hali ya kimaisha, ambayo pia tunajaribu kuyatatua baadhi yake.

Mkutano huu ulifanyika siku ya Jumanne pamoja na siku ya Jumatano, ambapo siku ya mwisho ya mkutano majadiriano yaliendelea hadi karibia usiku wa manane. Kwa ujumla, mkutano wenyewe ulifanikiwa sana.

Wengi waliondoka siku ya Alhamisi asubuhi kusafiri tena kwa basi kwa masaa mengi (wengine hadi kufikia masaa 10) kurudi nyumbani kwao. Wengine walisalia kwa muda zaidi, na nilijikuta ninakuwa na vikao nao siku nzima hadi jioni. Kutokana na maswala ya ndege pamoja na dharura za kuharibika kwake, ilinibidi nipande ndege tano tofauti, magari manne, na nisafiri kwa jumla ya masaa 50 kwenda na kurudi nyumbani, kwa kadiri ilivyowezekana.

## **Watendakazi kwa ajili ya Mavuno**

Ndugu zangu, mara kwa mara nimekuwa nikiwasihii mfuate

maonyo ya Yesu ya:

38 mwombeni Bwana wa mavuno, ili apeleke watenda kazi katika shamba lake la mavuno (Mathayo 9:38).

Vema, katika mkutano huu wa Nairobi, nilikutana na watendakazi wengi wa sasa na wale watakao faa kwa mavuno hapo baadaye. Mkutano ulitoa fursa ya ziada ya mafunzo kwao ili waweze kusaidia kazi ya Mungu.

Viongozi ambao hapo mwanzo walikuwa sehemu ya makanisa ya GCG, LCG, WCG, COGALC, COGIT, COGTE, CG7, SDA, na/ama VWCG, bali sasa wamekuwa sehemu ya CCOG nao pia walihudhuria. Hii kwangu ndiyo ilikuwa safari ya kwanza ambayo nimeweza kukutana ana kwa ana nao (baadhi yao wamekuwa na mawasiliano ya email nami kabla).

Kuhusu wale viongozi waliokuwa wageni kwa Kanisa la CCOG, baada ya mkutano, baadhi yao waliomba wawe sehemu ya CCOG. Mchungaji Evans na/ama mimi, tulijadiri nao juu ya kutofautiana katika uongozi, uelewa wa unabii, pamoja na kazi ya Mungu baina ya CCOG na makundi mengine. Na tuliwahimiza wote waliokuwa wamevutiwa, waisome na kuilewa vema makala yetu ya Vipengele vya Imani, ambayo tunatarajia kuitafsiri katika angalau lugha mbili zaidi za Kiafrica—Kiluo na Ekegusii (ambacho pia huitwa Kikisii). Makala yetu ya Vipengele vya Imani kwa sasa inapatikana katika lugha za Kiingereza, Kiswahili, Kihispania, na Kitagalag (lugha ya Kifilipino).

Kwa sababu ya Mkutano, kuwatemblea ndugu kihuduma, imani yetu, pamoja na machapisho; wale walio na mahusiano na CCOG wameongezeka. CCOG kwa sasa inayo makusanyiko 30 au zaidi katika Africa ya Mashariki. Tunao zaidi ya watu 500 wenye mahusiano na CCOG katika Kenya, Tanzania, pamoja na Uganda.

Viongozi wa CCOG kwenye mkutano walionyesha kuthamini kwa kiwango kikubwa uwingi wa mafundisho, historia ya kanisa, mada za kiunabii na zingine ambazo zilizungumziwa. Uelewa wao juu ya maswala mbalimbali yahusuyo CCOG pamoja na hatua ya mwisho ya Kazi ulikuwa ni wa kuvutia. Wengi katika Africa wanaonekana kuwa na umakini zaidi katika mambo ya kiimani kuliko wengine wa sehemu zingine na tumaini langu na maombi yangu ni kwamba wale walio nje ya Africa wafanane nao, wayachunguze maandiko ili kujiona ikiwa kile tunachokifundisha ndivyo kilivyo (soma Matendo 17:10-11), na waweze kuwa na kiu sahihi ya kuisaidia hatua ya mwisho ya kazi. Wengine pia walibainisha kwamba namna fulani ya ujasiri katika kuitangaza Injili kunahitajika, kitu ambacho wengi hawakukiona katika makundi mengine ya Makanisa ya Mungu, bali waliuona katika Kanisa la Continuing Church of God.

Evans Ochieng alibainisha kwamba umoja baina ya makanisa ya Mungu pamoja na ule wa mafundisho, wa kihistoria na katika habari za unabii ulikuwa umerejeshwa katika Africa kupitia CCOG. Mimi binafsi nilihamasishwa nilipoona jinsi wengi wao walivybainisha kuwa wameyasoma machapisho ya CCOG kwa kiwango kikubwa na ndiyo sababu walikuwa wamefikia kuamua kwamba CCOG yaweza kuwa ndiyo inayoongoza hatua ya mwisho ya Kazi ya Mungu.

## Mipango kwa Ajili ya Kazi katika Africa

Katika safari yangu hii, nilichukua kiasi kikubwa cha Biblia kama ilivyowezekana, Magazeti ya Habari za Unabii wa Biblia, pamoja na kijitabu kipyä kihusucho historia ya kanisa, ili nitumie vema uzito unaoruhusiwa katika ndege kwa mizigo ya kila msafiri, kuleta masomo Kenya,. Nilibeba kiasi kikubwa hadi kwamba sanduku langu laonekana kuwa limechanika kutokana na uzito wake. Kwa makusudi, nilchukua aina ya sanduku jepesi ili niweze kubeba kiasi kikubwa zaidi cha masomo na vijitabu ili kuwapeleke. Kijitabu kipyä cha historia ya kanisa kilikuwa ni hamasa kuu kwenye mkutano huo.

Hali kadharika nilimletea Mchungaji Evans Ochieng laptop mpya pamoja na mabango mawili ya kuonyesha Sikukuu ya Kanisa la CCOG ambayo yanaweza kutumika wakati wa Sikukuu ya Vibanda inayokuja. Kwa kuwa na computer kutawenza kumsaidia aweze kusimamia vema maswala mbalimbali ya kazi katika Africa, ikiwemo kuchapisha mafundisho na mawasiliano.

Kutokana na mahitaji makubwa kwa eneo hili, vilevile tulituma idadi kubwa ya Biblia, vitabu vya nyimbo, vijitabu juu ya unabii, vitabu, magazeti, pamoja na vijitabu vya historia ya kanisa, ambavyo vitawasili baada ya mkutano; kwa Mchungaji Ochieng na kwa wengine katika Africa. Kuna umasikini mkubwa katika eneo hili la ulimwengu, na wengi hawamudu kujinunulia Biblia wenyewe au hata uwezo wa kuwa na Maandiko kupitia vyombo vya Kielectroniki kama computer, kiasi kwamba sisi kuwatumia Biblia na machapisho mengine kutasaidia kulipunguza.

Washiriki wetu huko wanakabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa wanandugu wao na kutoka kwa jamii pale wanapoachana na imani zao za awali na kuukubali ukweli wa Biblia na kuishi kama Wakristo wa kweli. Utayari wao wa kukubali kuteseka na kujitoo kwa ajili ya ukweli na kwa ajili ya kazi kunapaswa kuwe ni mfano wa kuigwa na wote wanaoamini kwamba wao ni Wakristo wa sehemu ya Wanafiladefia wa kipindi cha mwisho (Ufunuo 3:7-13).

George Lemi, kiongozi wa kundi la CCOG katika Tanzania, ambaye pia ndiye mtafasiri wetu mkuu wa masomo kwa Kiswahili, yeye naye aliweza kuhudhuria mkutano huu katika Nairobi, Kenya. Tulijadiriana naye juu ya mipango mingine kuwezesha kuipanua kazi ya CCOG na waumini katika Tanzania. Tulijadiriana pia jinsi ya kufanya hivyo huko Uganda na kwingineko. Mimi pia alikuwa upendeleo kubatiza mtu kutoka Tanzania (Paulo Makinda Jumatano waliokuja pamoja na George Lemi.

Kwenye mkutano nilibaini kwamba wengi wa viongozi walikuwa wakizungumza lugha mbili au tatu (Kwa kawaida Kiingereza, Kiswahili, na/ama lugha yao ya kikabila).

Karibia wote katika Kenya wanaongea vema lugha ya Kiingereza. Wengi pia wa Kenya na Tanzania wanaongea Kiswahili kwa ufasaha. Lakini, katika maeneo hayo, na pia katika Uganda, wengi wanapendelea zaidi kuzungumza lugha zao za kikabila. Kwa kuwa wengi mionganii mwa waumini wa CCOG katika eneo hili wanapendelea zaidi kuzungumza lugha ya Kiluo, nilipendekeza kwa viongozi kwamba tuenze kuyatasafiri mafiundisho na machapisho kama vile Vipengele vya Imani ya Kanisa la Continuing

Church of God, ama kijitabu chetu cha Historia inayoenedlea ya Kanisa la Mungu katika lugha ya Kiluo, na hatimaye hata na gazeti letu la Habari za Unabii wa Biblia.

Kwa sasa tunachapisha gazeti letu la Habari za Unabii wa Biblia katika lugha za Kiingereza, Kiswahili, Kichina cha ki-Mandarin, Tagalog, na pia kwa Kihispania. Ijapokuwa kitabu chetu cha nyimbo, The Bible Hymnal, mwanzoni kilikuwa kinapatikana katika lugha ya Kiingereza pekee, kabla ya mkutano wa Nairobi tulikuwa tumeanza kazi ya kuandaa kukichapisha kwa lugha ya Kiswahili pia, na tunatarajia hili litakuwa limefanyika kufikia wakati unalisoma gazeti hili. Kitabu cha nyimbo katika lugha ya Kiluo ni mradi ambaa tayari kwa sasa uko mbioni, na tunatarajia pengine kitakuwa tayari kabla ya Sikukuu ya Vibanda ya mwaka 2014.

Wakati wa kikao hicho, niliainisha mipango ya kuifikia Africa kwa mahubiri. Hii ni pamoja na kupitia upya na kuangalia jinsi tovuti zetu kwa sasa, huduma ya mahubiri, pamoja na mahojiano ya kwenye radio yanalifikiaje eneo hili la ulimwengu. Pia nilibainisha mipango yetu kwa ajili ya Africa hususani kuwa na tovuti maalum, inayotarajiwa kubeba machapisho yetu kwa njia ya mtandao katika angalau lugha tatu, huku tukitarajia lugha zingine kuongezeka hapo baadaye. Nilibainisha kwamba ni lazima tuwe na taarifa sahihi juu ya pale makusanyiko yalipo, mawasiliano ya email ya kila kiongozi, na hata picha za kila ukumbi ama sehemu ambapo kusanyiko hukutanikia ili iwe rahisi kwa wale ambaa wanakusudia kujumuika na makundi yetu ya CCOG waweez kufanya hivyo kwa urahisi.

Viongozi kutoka Kenya na Tanzania walitoa ushirikiano mzuri kuhusu mipango yetu hii na walionekana kuifurahia na kutiwa moyo kwamba CCOG ilikuwa na nia ya dhati juu ya Africa katika kazi ya Mungu.

## Mlango Ulio katika Harakati za Kufunguliwa Zaidi

Ijapokuwa kwa wakati huu, yaonekana ni wachache tu katika Kenya na Tanzania ambaa wanayo fursa ya mawasiliano ya internet bila ya kuhitaji kwenda kwenye kibanda kitoacho huduma hiyo (ambapo ni wachache wanaweza kumudu gharama zake), nilibaini kwamba karibia wote walikuwa na simu za mkononi.

Pale simu za kisasa (smart phones) zitakaposhamiri katika eneo hili (sikuona yeoyote aliyekuwa nayo wakati wa Mkutano), itatuwezesha tuweze kuwafikia wengi, wengi kuliko ambavyo tumeweza kwa kutumia internet. Mipango yetu ya tovuti pamoja na makusanyiko inatakiwa iwe tayari kufikia wakati ambapo wengi katika Africa Mashariki watakafokia kuwa na uwezo wa kuzifikia. "Mlango" umewekwa wazi kwa wanafiladelfia (Ufunuo 3:7-8) waweez kuihubiri Injili (soma Matendo 14:28; 1 Wakorintho 16:9; 2 Wakorintho 2:12) ya ufalme (Mathayo 24:14) na unazidi kufunguliwa zaidi kwa ajili yetu, na tunatarajia tuutumie kuwafikia wengi zaidi. Tafadhalii, muombe Mungu aufungue wazi zaidi mlango huu kwa ajili yetu (soma Wakolosai 4:3).

Mambo meni ya hatua ya mwisho ya kazi kwa sasa yanasonga mbele kamyakimya, na sawa na hali ilivyo kule Kenya, jiweke tayari pale muda utakapokuwa muafaka kwa wengine nao kuusikia

ujumbe wa Ufalme wa Mungu.

Africa kwa namna fulani inatekeleza jukumu la kuwa kama "eneo la kuthibitishia" kwamba jinsi kazi hii inavyotekelawa ndio njia ambayo Yesu Kristo anavyotaka tuifanye. Sisi tulio katika CCOG pia tunategemea kuongoza katika kutimiza lile ambalo Biblia inaliita kuwa ni "kazi fupi" (ya haraka) katika Warumi 9:28 na ni hatua nydingi zinachukuliwa kulingana na swala hilo pia.

Kwa kuongezea, kulingana na mtazamo wa kimwili, yapo mahitaji makubwa katika Africa na siku zote tunajaribu kutafakari ni jinsi gani bora tutaweza kuyatatua mahigtaji ya ndugu zetu hawa, ikiwemo wajane na yatima, walioko huko.

Pamoja na umasikini wa kimaisha, Africa ni sehemu muhimu ya hatua ya mwisho ya Kazi ya Mungu. Ni tumaini langu na maombi kwamba mawaidha, maoni na ushirikiano ulioko huko utasaidia kama hamasa kwa wale walioko katika maeneo mengine ya ulimwengu ili waweze kuufuata mfano wao wa Kifiladefia kwa kuisaidia na kuiunga mkono CCOG katika harakati hizi za kuongoza hatua ya mwisho ya kazi.

Kazi ya Mungu kupitia Kanisa la Continuing Church of God inazaa matunda (soma, Mathayo 7:15-20) ulimwenguni kote (Mathayo 28:19-20) na Africa inathibitisha kwamba hili ndivyo lilivyo.



Bw na Bi Evans Ochieng Kisienyo



Mkutano Picha



Mkutano Picha



Ubatizo wa Paulo Makinda ya Tanzania katika pool katika Kenya na Dk Thiel.

# Kuitekeleza Mathayo 24:14 Pamoja na Mathayo 28:19-20



*Website ya Kanisa la Continuing Church of God: [www.ccog.org](http://www.ccog.org)  
Website ya Taarifa za Unabii wa Biblia za Kilasiku: [www.cogwriter.com](http://www.cogwriter.com)*

**CCOG.ASIA:** Hii ni Website ilengayo wasomaji kutoka Asia. Inazo makala katika lugha ya Kichina cha Mandarin pia na katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za Kiasia.

**CCOG.IN:** Hii ni Website inayolenga wale walio wa asili ya kihindi.

**CCOG.EU:** Hii ni Website kwa wale wa Ulaya. Inazo makala katika lugha nyingi za Ulaya.

**CDLIDD.ES:** Hii ni website ya Continuing Church of God katika lugha ya Kihispania.

**PNIND.PH:** Hii ni Website kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.



***Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia***  
[www.youtube.com/BibleNewsProphecy](https://www.youtube.com/BibleNewsProphecy)

***Chaneli ya kanisa la ContinuingCOG***  
[www.youtube.com/continuingcog](https://www.youtube.com/continuingcog)

---

Mchungaji Mwandumizi wa Continuing Church of God ni mgeni mwalikwa mara kwa mara kwenye radio, akitumia radio kuwafikia wasikilizaji wa maeneo mengi.

Kanisa la Continuing Church of God pia hutumia majarida pamoja na magazeti ya kielectronic, vitabu na barua za kila juma kwa waumini wake katika nkutekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19—20

